

**RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA  
HESABU ZA SERIKALI**

**KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA MAMLAKA  
ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA ULIOISHIA  
TAREHE 30 JUNI, 2010**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Simu: 255(022)2115157/8  
Nukushi: 255(022)2117527  
Barua pepe: [ocag@nao.go.tz](mailto:ocag@nao.go.tz)  
Tovuti: [www.nao.go.tz](http://www.nao.go.tz)  
Unapojibu tafadhalii taja  
Kumb. CA.4/37/01/2009/2010  
na tarehe



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa  
Hesabu za Serikali,  
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Barabara ya Samora /Ohio,  
S.L.P. 9080,  
DAR ES SALAAM.

31 Machi, 2011

Mh. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete,  
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
Ikulu,  
S.L.P. 9120,  
DAR ES SALAAM.

**Yah : KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA UKAGUZI WA  
HESABU ZA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA  
MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 30 JUNI, 2010**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na kifungu cha 48 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), pamoja na kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha ripoti tajwa hapo juu kwa taarifa yako na hatua zinazopaswa kuchukuliwa.

Nawasilisha,

Ludovick S. L. Utouh  
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

### *Imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara namba 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Kazi na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) kama ilivyofafanuliwa zaidi na vifungu Na. 45 na 48 vya sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na kifungu Na.10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

#### **Dira ya Ofisi**

Kuwa kituo cha ubora katika ukaguzi wa hesabu katika sekta za umma.

#### **Lengo la Ofisi**

Kutoa huduma bora za ukaguzi zenyenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Katika kutoa huduma zenyenye ubora unaostahili, Ofisi inaongozwa na vigezo vya msingi vifuatavyo:**

**Kutopendelea**      Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi isiyopendelea, inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.

**Ubora**                  Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni ya kitaalamu inayotoa huduma bora za ukaguzi wa hesabu kwa kuzingatia viwango vya kitaaluma.

**Uadilifu**                Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inazingatia na kudumisha haki kwa kiwango cha juu na kuheshimu sheria.

**Ubunifu**                Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi bunifu ambayo wakati wote inaimarisha na kukaribisha mawazo mapya ya kimaendeleo toka ndani na nje ya taasisi.

**Matumizi bora ya rasilimali za umma**      Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni taasisi inayozingatia matumizi bora ya rasilimali zilizokabidhiwa kwake.

© Taarifa hii ni kwa ajili ya matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, baada ya taarifa hii kuwalishwa Bungeni, taarifa itakuwa ni kumbukumbu ya umma na usambazaji wake hautakuwa na kikomo.

## Dibaji

Ninayo heshima kuwasilisha taarifa yangu ya mwaka ya ukaguzi wa hesabu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

Ripoti hii ni ujumuisho wa taarifa za ukaguzi katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kwa muhtasari, ambapo maelezo ya kina ya taarifa hizo yanapatikana katika taarifa za Halmashauri husika zilizotumwa kwa uongozi wa Halmashauri husika.

Ripoti hii inawasilishwa kwa Mh. Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), kifungu Na.48 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na kifungu Na.34(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Nia ya ripoti hii ni kuwajulisha wadau wetu wa Serikali za Mitaa, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Serikali, Mahakama, wahisani, mashirika na jamii kwa ujumla muhtasari wa matokeo ya ukaguzi kutokana na ukaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

Ripoti hii inatoa tathmini ya jumla ya ukaguzi kuhusu hali ya utoaji taarifa za fedha, kufuata sheria na kanuni, na juu ya masuala ya uwajibikaji na utawala zinazohusiana na uendeshaji wa Serikali za Mitaa nchini.

Ukaguzi wa mwaka huu wa fedha umegusa jumla ya Mamlaka za Serikali za Mitaa 134 katika nchi ikilinganishwa na 133 katika mwaka wa ukaguzi uliopita, hii ni baada ya uanzishwaji wa Halmashauri ya Mji wa Masasi tarehe 1 Julai 2010 na kutangazwa kwenye Tangazo la Serikali Na. 393 la tarehe 15 Oktoba 2010.

Nina furaha kukuarifu kuwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa nchini zimekaguliwa na ofisi yangu.

Ni vema ikaeleweka kwamba wakati Ofisi yangu inatoa taarifa juu ya utekelezaji wa sheria mbalimbali, kanuni na miongozo, na udhaifu katika mifumo ya taarifa za kifedha na udhibiti wa ndani

katika taasisi ya sekta ya umma na hasa Serikali za Mitaa, wajibu wa mwisho kwa ajili ya kutengeneza mfumo wenye ufanisi wa udhibiti wa ndani na mfumo wa ufuataji sheria uko chini ya uongozi na usimamizi wa kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zina majukumu mbalimbali kwa ajili ya utoaji wa huduma muhimu na utawala bora kwa wananchi wa maeneo yao. Ili kutimiza majukumu haya, wanapaswa kukusanya mapato kwa njia ya kodi, vyanzo vya leseni, ada na mapato mengineyo. Katika suala hili, usimamizi wa fedha ni muhimu ili Serikali za Mitaa ziweze kuleta ushawishi kwa umma kuwa mapato hayo yamepokelewa kwa kufuata sheria na kutumika ipasavyo kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Ningependa kutambua mchango wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, hii ni moja ya kamati muhimu ya uangalizi ya Bunge kwa ajili ya kufuatilia taarifa za ukaguzi zilizopita.

Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa watu wote waliotengeneza mazingira mazuri kwa ajili ya kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba na kukamilika kwa wakati taarifa ya jumla ya Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010.

Natumaini kwamba Bunge litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za muhimu katika kufanya Serikali kuwajibika kwa ajili ya usimamizi wake wa fedha za umma na utoaji wake wa huduma bora za umma kwa Watanzania ambao inawahudumia, katika suala hili, nami nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa taarifa hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.



Ludovick S. L. Utouh

#### **MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

---

**Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,  
Dar es Salaam,  
31 Machi, 2011**

## **Shukrani**

Ripoti ya mwaka ya ukaguzi kwa hesabu za 2009/10 imekamilika kwa mafanikio. Mafanikio haya yamefikiwa kwa sababu ya msaada na ushirikiano nilioupata kutoka kwa wadau mbalimbali.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake yote, Bunge na Kamati za Bunge za Uangalizi kwa ajili ya kusaidia ofisi yangu na kuchukua kwa umakini masuala yaliyoyoitokeza kwenye ripoti zangu za ukaguzi kwa lengo la kuboresha uwajibikaji wa fedha nchini.

Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa wale ambaو walinitengenezea mazingira mazuri ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Napenda kuwashukuru watumishi wote wa ofisi yangu kwa juhudhi zao na kwa mara nyingine tena, kuwezesha ripoti kutoka ndani ya muda wa kisheria. Kwa moyo wa shukrani nyngi , nina wajibu wa kulipa fadhila kwa familia yangu na kwa familia za watumishi wa ofisi yangu kwa uvumilivu waliokuwa nao kwa kipindi chote ambacho hatukuwa nao ili kutimiza majukumu haya ya Katiba.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziende kwa jumuiya ya wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia SIDA, Benki ya Dunia kupitia mradi wa PFMRP, Sekretarieti ya AFROSAI - E na wote wanaotutakia mema ambaو wana mchango mkubwa sana kuelekea mabadiliko ya ofisi yangu. Michango yao katika kuendeleza rasilimali watu, mifumo ya IT na mali za kudumu vina athari kubwa katika mafanikio yetu. Bado tunahitaji msaada zaidi kwa ajili ya kuboresha kazi ya ukaguzi katika sekta ya umma na kuwa ya kisasa zaidi, ambayo kasi yake ingekuwa imeongezeka endapo angepatikana mfadhili mwenye nia ya kufadhili ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya ukaguzi kinachotegemewa kujengwa Dar es Salaam.

Pia ninawiwa kuwashukuru wadau wetu wengine wote ikiwa ni pamoa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Maafisa Masuuli wote wa

Serikali za Mitaa kwa ajili ya ushirikiano mkubwa, msaada na kwa ajili ya kutoa taarifa muhimu zilizowezesha kuandaa taarifa hii. Napenda pia kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchapishaji wa haraka wa taarifa hii na kuhakikisha kuwa inatoka kwa wakati.

Kwa kuhitimisha, napenda kuwashukuru watumishi wote wa umma nchini katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa bila kusahau wajibu wa walipa kodi ambao ripoti hii imelengwa kwao na pia vyombo vya habari. Michango yao ya thamani katika ujenzi wa Taifa haiwezi kutothaminiwa.

Mungu mwenyezi awabariki wote, nami najitoa mwenyewe kwa ajili ya kutoa huduma za ukaguzi wa ufanisi ili kuimarisha uwajibikaji na thamani ya fedha katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

## TAFSIRI/VIFUPISHO

|                  |  |
|------------------|--|
| <b>AFROSAI-E</b> | Muungano wa Asasi Kuu za Ukaguzi katika nchi za Afrika zinazotumia lugha ya Kiingereza |
| <b>ASDP</b>      | Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo  |
| <b>BoQ</b>       | Mchanganuo wa gharama za kazi za ujenzi  |
| <b>CAG</b>       | Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali   |
| <b>CBG</b>       | Ruzuku ya Kujenga Uwezo  |
| <b>CDCF</b>      | Mfuko wa Kuhamasisha Maendeleo wa Jimbo  |
| <b>CDG</b>       | Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo  |
| <b>CDG</b>       | Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo  |
| <b>CHF</b>       | Mfuko wa Afya wa Jamii   |
| <b>D by D</b>    | Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi  |
| <b>DCI</b>       | Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai   |
| <b>GPSA</b>      | Wakala wa Huduma za Manunuzi Serikalini  |
| <b>H/W</b>       | Halmashauri ya Wilaya  |
| <b>IFAC</b>      | Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu  |
| <b>IFMS</b>      | Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha  |
| <b>IFRS</b>      | Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha                                 |
| <b>INTOSAI</b>   | Shirika la Kimataifa la Asasi kuu za Ukaguzi   |
| <b>IPSASs</b>    | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma                                    |
| <b>ISA</b>       | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi  |
| <b>ISSAIs</b>    | Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi kuu za Ukaguzi                               |
| <b>IT</b>        | Teknolojia ya Habari   |
| <b>LAAC</b>      | Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa   |
| <b>LAAM</b>      | Muongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa, 1993                                 |
| <b>LAFM</b>      | Memoranda ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997                               |
| <b>LAPF</b>      | Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa                                     |
| <b>LGAs</b>      | Mamlaka ya Serikali za Mitaa   |

|                     |  |
|---------------------|--|
| <b>LGDG</b>         | Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa           |
| <b>LGLB</b>         | Mfuko wa Mikopo wa Serikali za Mitaa                         |
| <b>MMAM</b>         | Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi                        |
| <b>MMEM</b>         | Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi                       |
| <b>MSD</b>          | Bohari Kuu ya Madawa   |
| <b>MTEF</b>         | Mpango wa Kati wa Matumizi ya Fedha za Umma                  |
| <b>NAO</b>          | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi                                    |
| <b>NMSF</b>         | Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI                         |
| <b>OWM-TAMISEMI</b> | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa  |
| <b>PAA</b>          | Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya 2008                     |
| <b>PEPFAR</b>       | Mpango wa dharura wa Rais wa Marekani unaoshughulikia UKIMWI |
| <b>PMU</b>          | Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi                            |
| <b>PPRA</b>         | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma                      |
| <b>RAS</b>          | Katibu Tawala wa Mkoa  |
| <b>TAKUKURU</b>     | Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa                     |
| <b>TASAF</b>        | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania                         |
| <b>UKIMWI</b>       | Ukosefu wa Kinga Mwilini                                     |
| <b>URT</b>          | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania                              |
| <b>USAID</b>        | Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani                |
| <b>VC</b>           | Kamati ya KiJiji   |
| <b>VFC</b>          | Mratibu wa Mfuko wa KiJiji                                   |
| <b>VFJA</b>         | Mratibu Msaidizi wa Mfuko wa KiJiji                          |
| <b>VVU</b>          | Virusi Vya Ukimwi  |
| <b>WSDP</b>         | Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji                       |

## YALIYOMO

|  |            |     |
|--|------------|-----|
| Dibaji.....  | ii         |     |
| Shukrani .....   | iv         |     |
| Tafsiri/Vifupisho.....   | vi         |     |
| Yaliyomo .....   | viii       |     |
| Muhtasari wa Taarifa ya Ukaguzi .....  | xiii       |     |
| <br>SURA YA KWANZA..... 1  |            |     |
| <b>1.0 Utangulizi na Mambo ya Jumla .....</b>  | <b>1</b>   |     |
| 1.1 Madhumuni ya Ukaguzi na Mwongozo wa Kisheria.....  | 1          |     |
| 1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa ya Ukaguzi .....  | 5          |     |
| 1.3 Idadi ya ofisi zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya<br>Ukaguzi.....  | 7          |     |
| 1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa<br>Taarifa za Fedha.....   | 9          |     |
| <br>SURA YA PILI..... 11   |            |     |
| <b>2.0 Aina, Vigezo na Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi .....</b>   | <b>11</b>  |     |
| 2.1 Vigezo vya hati za ukaguzi zilizotolewa .....  | 11         |     |
| 2.2 Hati za Ukaguzi .....  | 11         |     |
| 2.3 Misingi ya kutoa hati mbali na hati inayoridhisha .....  | 15         |     |
| 2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi katika Halmashauri.....  | 18         |     |
| <br>SURA YA TATU..... 37   |            |     |
| <b>3.0 Ukaguzi wa Taarifa za Fedha na Masuala ya Udhibiti wa Ndani.....</b>  | <b>37</b>  |     |
| 3.1 Utendaji Wa Kifedha.....   | 37         |     |
| 3.2 Tathimini ya mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Mamlaka za<br>Serikali za Mitaa .....  | 40         |     |
| 3.3. Utayarishaji wa Taarifa za Fedha.....   | 56         |     |
| 3.4 Udhibiti wa matumizi.....  | 81         |     |
| 3.5 Ukaguzi wa Mishahara .....   | 86         |     |
| 3.6 Matumizi ya fedha zilizotolewa kwa watu waliopata maafa.....   | 89         |     |
| 3.7 Ukaguzi wa Maduhuli ya Halmashauri.....  | 95         |     |
| 3.8 Usimamizi wa Mali na Madeni ya Muda Mfupi .....  | 99         |     |
| 3.9 Usimamizi wa mali za kudumu .....  | 107        |     |
| 3.10 Uendeshaji wa Mifuko Maalumu .....  | 113        |     |
| 3.11 Ufuutiliaji wa utekelezaji wa mapendeleko ya ukaguzi kwa miaka<br>iliyopita kwa ripoti ya jumla na ripoti ya kila Halmashauri husika .. | 122        |     |
| <br>SURA YA NNE .....  |            | 129 |
| <b>4.0 Kupitia Mikataba na uzingatiaji wa taratibu za manunuza katika<br/>Mamlaka za Serikali za Mitaa .....</b>                             | <b>129</b> |     |
| 4.1 Ufuataji wa Kanuni za manunuza .....   | 129        |     |
| 4.2 Ufanisi wa Utendaji kazi wa Kitengo cha Usimamizi Manunuza (PMU)   | 129        |     |

|            |   |            |
|------------|---|------------|
| 4.3        | Mapitio ya Mikataba na Uzingatiaji wa Taratibu za Ununuzi katika Halmashauri .....        | 135        |
|            | <b>SURA YA TANO .....</b>   | <b>139</b> |
| <b>5.0</b> | <b>Ukaguzi wa miradi iliyopata fedha toka kwa wahisani.....</b>                           | <b>139</b> |
| 5.1        | Mwelekeo wa Fedha.....  | 139        |
| 5.2        | Uhakiki wa utekelezaji wa Miradi .....  | 146        |
| 5.3        | Utekekezaji wa Kilimo Kwanza .....  | 152        |
|            | <b>SURA YA SITA .....</b>   | <b>161</b> |
| <b>6.0</b> | <b>Matokeo ya kaguzi maalum.....</b>  | <b>161</b> |
| 6.1        | Utangulizi .....  | 161        |
| 6.2        | Mtiririko wa mabadiliko baada Kaguzi Maalum.....  | 161        |
| 6.3        | Muhtasari wa masuala yaliyojiteze katika kaguzi maalumu zilizofanyika mwaka 2009/10 ..... | 161        |
|            | <b>SURA YA SABA .....</b>   | <b>179</b> |
| <b>7.0</b> | <b>Hitimisho na Mapendekezo.....</b>  | <b>179</b> |
| 7.1        | Hitimisho .....   | 179        |
| 7.2        | Mapendekezo.....  | 187        |
|            | Kiambatisho .....   | 193        |

## MUHTASARI WA TAARIFA YA UKAGUZI

Madhumuni ya ripoti hii ya jumla ni kuwasilisha muhtasari wa mambo muhimu yaliyojiteza wakati wa ukaguzi wa Serikali za Mitaa kwa hesabu za mwaka 2009/2010. Sehemu hii ya ripoti inatoa maelezo ya jumla ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu na kufuatiwa na mambo muhimu kwa yaliyobainika wakati wa ukaguzi pamoja na muhtasari wa mapendekezo.

### A. Masuala ya Jumla yaliyojiri

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010 umekamilika. Muhtasari wa masuala muhimu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi yapo katika ripoti hii na masuala haya kwa kirefu yamefanuliwa katika taarifa zilizopelekwa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Idadi ya Halmashauri imeongezeka kutoka 133 kwa mwaka uliopita hadi kufikia 134 kwa mwaka 2009/2010. Halmashauri mpya kwa mwaka huu ni Halmashauri ya Mji wa Masasi. Hii imetokana na kupandishwa daraja kwa Halmashauri hiyo kutoka Mamlaka ya Mji mdogo na kuwa Halmashauri ya Mji.

Kiwango cha utendaji kwa mwaka 2009/2010 kimeshuka ikilinganishwa na mwaka 2008/2009. Tathmini ya matokeo ya ukaguzi kwa miaka miwili ni kama ilivyoainishwa katika jedwali hapa chini:

| Halmashauri              | Hati zinazoridhisha |           | Hati zenye shaka |           | Hati Isiyoridhisha |           | Jumla   |           |
|--------------------------|---------------------|-----------|------------------|-----------|--------------------|-----------|---------|-----------|
|                          | 2008/09             | 2009/2010 | 2008/09          | 2009/2010 | 2008/09            | 2009/2010 | 2008/09 | 2009/2010 |
| Halmashauri za Jiji      | -                   | -         | 4                | 4         | -                  | -         | 4       | 4         |
| Halmashauri za Manisapaa | 10                  | 8         | 7                | 9         | -                  | -         | 17      | 17        |
| Halmashauri za Miji      | 4                   | 1         | 2                | 6         | -                  | -         | 6       | 7         |
| Halmashauri za Wilaya    | 63                  | 56        | 42               | 46        | 1                  | 4         | 106     | 106       |
| Jumla                    | 77                  | 65        | 55               | 65        | 1                  | 4         | 133     | 134       |
| Asilimia                 | 58%                 | 48.5%     | 41%              | 48.5%     | 1%                 | 3%        | 100%    | 100%      |

Kama inavyoonekana hapo juu, idadi ya hati zinazoridhisha imepungua toka 77 (58%) katika mwaka 2008/2009 hadi 65 (48.5%) katika mwaka wa ukaguzi (2009/2010).

Wakati huo huo idadi ya hati zenye mashaka imeongezeka kutoka 55 (41%) kwa mwaka 2008/2009 hadi kufikia 65 (48.5%) katika mwaka wa ukaguzi (2009/2010).

Idadi ya Hati zisizoridhisha pia zimeongezeka kutoka 1 (1%) katika mwaka 2008/2009 hadi kufikia 4 (3%) katika mwaka wa ukaguzi (2009/2010). Halmashauri zilizopata Hati zisizoridhisha katika mwaka wa ukaguzi ni Halmashauri za Wilaya za Mwanga, Kishapu, Rombo na Kilwa.

Kama ilivyokuwa katika mwaka uliopita, hakuna Halmashauri iliyopata hati mbaya kwa mwaka huu wa ukaguzi.

Kushuka kwa kiwango cha utendaji katika Halmashauri kumechangiwa kwa kiasi kikubwa na sababu zifuatazo:

- Taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi kutoqua sahihi kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) hivyo kupelekea kuwa na ugumu katika kupima utendaji wa Halmashauri. Mfano,

Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ilionyesha katika taarifa za fedha ruzuku ya maendeleo ya kiasi cha Sh.1,911,447,792 kama ruzuku ya matumizi ya kawaida.

- Halmashauri kutokuwa na usimamizi na ufuatiliaji wa karibu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ilitekelezwa katika ngazi za chini za Serikali yaani kata na Vijiji.
- Ongezeko la fedha zinazohamishwa na Halmashauri kwenda katika ngazi ya chini ya utekelezaji yaani Vijiji na kata chini ya utaratibu wa ugatuaji wa mamlaka kwa wananchi (D by D). Utaratibu huu una uhitaji mkubwa wa uwezeshaji katika uwezo wa kutunza fedha, hivyo kukosekana uwezeshaji huo kunaongeza hatari ya utunzaji fedha hizo kuwa mbaya.
- Halmashauri kutozingatia kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani. Hii ikiwa ni pamoja na kuwa na vitengo vya ukaguzi wa ndani vilivyo dhaifu, vitengo vya manunuvi visivyo madhubuti, kamati za ukaguzi kutofanya vikao vya kutathimini utendaji wa Halmashauri na hivyo kutotoa ushauri upasao kwa menejimenti ya Halmashauri husika.

#### **B. Mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi**

Mapungufu makubwa pamoja na madhaifu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi yanajumuisha yafuatayo:

- Baadhi ya Halmashauri hazikutengeneza taarifa za matumizi za fedha za maendeleo na ugharimiaji kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2010. Kutotengenezwa kwa taarifa hizo, ukaguzi haukuweza kuthibitisha vyanzo vya mapato, miradi iliyo tekelezwa, bajeti ya miradi, salio anzia, mapato kwa mwaka husika, matumizi na bakaa ya fedha za miradi kwa mwisho wa mwaka wa fedha.
- Baadhi ya taarifa za fedha za Halmashauri zilizowasilishwa kwa ukaguzi zili kuwa na mapungufu makubwa. Mfano ni uwekaji

wa tarakimu zisizo sahihi kwenye taarifa za fedha, kuweka taarifa za mali bila thamani, kutoonesha mali za Halmashauri katika mizania ya hesabu na vielekezi vytaarifa za fedha au majedwali yanayoonesha mchanganuo.

- Matokeo ya ukaguzi wa fedha za miradi ya maendeleo na ruzuku umeonesha kwamba, Halmashauri 133 (isipokuwa Halmashauri ya Mji wa Masasi) ilikuwa na jumla ya Sh.507,866,599,666 kwa ajili ya kufadhili miradi ya maendeleo za Halmashauri. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 kiasi cha Sh.332,092,443,562 kilikuwa kimetumika na kuacha bakaa ya Sh.175,774,156,104 au 33% ambayo imehusisha Halmashauri 132.
- Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliajiri kampuni ya ushauri ya KPMG-Tanzania katika kazi ya kukagua Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) kati ya Agosti 2009 na Juni 2010. Tathmini hii imeibua udhaifu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumika chini ya kiwango kwa IFMS, ukosefu wa mafunzo ya rejea na mafunzo ya kawaida kwa watumiaji wa mfumo, mfumo wa Epicor kutoendana na IPSASs na utekelezaji wa toleo la Epicor 7.2 haukukidhi mahitaji ya Serikali za Mitaa.
- Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri 34 kati ya 134 zilizokaguliwa zilifanya malipo ya Sh.2,830,338,208 bila hati za malipo kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi hivyo kuzuia mawanda ya ukaguzi. Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu inaongoza kwa kuwa na hati za malipo zilizokosekana za Sh.1,393,123,804 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa yenye hati za malipo zilizokosekana ni za Sh.411,876,806.
- Malipo ya Sh.5,515,453,908 kutoka katika Halmashauri 71 yalifanyika yakiwa na nyaraka pungufu ili kuwezesha uhakiki wa uhalali wa malipo haya. Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa iliongoza kwa kutowasilisha nyaraka zenye thamani ya

Sh.803,959,615 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa kutowasilisha nyaraka zenyenye thamani ya Sh.449,681,752.

- Mishahara isiyolipwa kiasi cha Sh.1,185,252,606 ikihusisha Halmashauri 55 haikuweza kurudishwa Hazina. Halmashauri ambayo haikurejesha pesa nyingi zaidi ni lleje ambayo haikurejesha Sh.109,698,842 ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Mwanza Sh.106,142,575.
- Ukaguzi katika hati za malipo ya mishahara haufanywi mara kwa mara na menejimenti za Halmashauri. Kutokana na upungufu huu mishahara imekuwa ikilipwa katika akaunti za benki za wafanyakazi waliofariki, waliostaafu, waliotoroka, walioacha kazi na walifukuzwa kwa kuwa majina yao hayajaondolewa katika orodha za mishahara. Malipo ya namna hii ni vigumu kurudishwa kwa kuwa waliolipwa isivyo halali hawapo kazini. Halmashauri 38 zimelipa malipo ya jumla ya Sh.583,221,297, ikiongozwa na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo Sh.72,356,016 na ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni Sh.56,014,740.
- Ukaguzi wa mishahara na nyaraka zake umebaini kwamba kiasi cha Sh.290,174,973 kililipwa kwa taasisi mbalimbali za fedha ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyochukuliwa na waliokuwa watumishi wa Halmashauri. Hata hivyo ukaguzi wa taarifa za mishahara ulibainisha kuwa, watumishi hao walishaacha utumishi hivyo hawakustahili kuendelea kulipwa mishahara. Halmashauri yenye kiasi kikubwa cha malipo hayo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba yenye Sh.227,569,484 ikifuatiwa na Kibondo yenye Sh.22,271,871.
- Ukaguzi ulibaini kuwa baadhi ya mishahara ya watumishi wa Halmashauri inakatwa makato yanayozidi kiwango cha 2/3 ya mishahara halisi kutokana na mrundikano wa madeni uliotokana na mikopo kutoka kwenye taasisi mbalimbali za fedha. Katika hali isiyokuwa ya kawaida watumishi wamekuwa wakikatwa mshahara wote. Mfano ni Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma; kati ya watumishi 198 waliohakikiwa, watumishi 45 ambaao ni 23% wamekuwa wakikatwa mshahara wote. Hali

hii ya mikopo isiyodhibitiwa inaweza kuathiri utendaji kazi wa watumishi na hivyo kuathiri utendaji wa Halmashauri kwa ujumla kutokana na kukosekana kwa morali ya kufanya kazi. Utaratibu huu ni kinyume na waraka Na.CCE.45.271/01/87 wa tarehe 19 Machi 2009 uliotolewa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambao unazuia mtumishi kubakiwa na mshahara chini ya 1/3 ya mishahara.

- Vitabu 948 vya kukusanya mapato katika Halmashauri 48 havikuweza kutolewa kwa wakaguzi kwa ajili ya uhakiki, hivyo kupelekea wakaguzi kushindwa kuthibitisha kiasi cha mapato kilichokusanya kuititia vitabu hivyo. Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro iliongoza kwa kuwa na vitabu 168 ambavyo havikuwasilishwa ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Lindi yenye idadi ya vitabu 101.
- Katika mwaka wa ukaguzi, Halmashauri 43 hazikukusanya mapato yenye jumla ya Sh.2,756,763,702 kutoka kwa mawakala wa kukusanya mapato. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni iliongoza kwa kutokusanya mapato ya kiasi cha Sh.1,132,294,000 ikifuatiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Arusha yenye kiasi cha Sh.627,244,100 ambacho hakikukusanya.
- Masuala kadhaa yakihuisha usuluhisho wa benki yalikuwa hayajatatuliwa katika hesabu za Halmashauri. Hii inajumuisha Sh.9,612,413,862 zikiwa ni mapato yaliyo kwenye vitabu vya Halmashauri lakini hayakuonekana katika taarifa ya benki. Kiasi cha Sh.805,665,694 kutoka Halmashauri mbalimbali kilikuwa ni fedha ambazo hazijapelekwa benki. Hakuna juhudi zozote zilizoonekana katika kuhakikisha kuwa fedha hizo zinaingia kwenye taarifa za benki. Pia kiasi cha Sh.2,586,187,823 zilitolewa kwenye akaunti ya benki bila kuingizwa kwenye vitabu vya Halmashauri.
- Katika kuhakiki usimamizi wa mikataba mbalimbali katika mwaka wa ukaguzi umebainisha idadi ya mikataba yenye nyaraka zenye mapungufu ambapo taarifa muhimu zilikosekana

kwenye mafaili ya mikataba ikiwa pamoja na makubaliano ya mikataba, mchanganuo wa gharama za ujenzi, makadirio ya mhandisi, hati za kuidhinisha kazi na manunuzi yaliyofanyika nje ya mpango. Mikataba ya manunuzi ya Sh.1,763,343,294 ikihusisha Halmashauri 10 zilizohakikiwa.

- Wakati wa ukaguzi wa fedha za mfuko wa maendeleo ya Jimbo (CDCF), nilibaini kuwa baadhi ya Halmashauri hazikutumia kabisa fedha zilizokuwa zimepelekwa kwenye Halmashauri hizo, sababu zikiwa ni pamoja na kutofunguliwa kwa akaunti maalum kwa ajili ya madhumuni hayo na pia fedha hizo zilitolewa wakati wa mwishoni mwa mwaka yaani kati ya mwezi Mei na Juni, 2010. Hivyo malengo ya mfuko huo katika mwaka wa fedha 2009/2010 hayakuwa la mafanikio
- Ilibainika wakati wa ukaguzi wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) kwamba katika sampuli ya Halmashauri zilizochaguliwa, fedha zilizopokelewa katika ngazi ya Halmashauri zilitofautiana na fedha zilizorekodiwa kwamba zimelipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa taarifa za Mpango wa Maboresho wa Serikali za Mitaa (LGRP) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Pia kulikuwa ucheleweshaji wa kutoa fedha kwa ajili ya shughuli za Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF). Katika baadhi ya matukio yasiyo ya kawaida, fedha zilizotengwa kwa ajili ya mwaka 2009/2010 zilipokelewa katika mwaka wa fedha 2010/2011.
- Masuala mbalimbali yalidhihirika wakati wa kaguzi maalum zilizofanyika katika Halmashauri za Wilaya za Rombo, Kilosa, Rorya, Tarime na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:
  - (i) Posho ya safari za kiasi cha Sh.7,280,000 zilizolipwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rombo zilikuwa si halali kwani kwa siku hizo walizolipwa, daftari la mahudhurio linaonesha kuwa watumishi hao walikuwepo ofisini.

- (ii) Katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo mafuta ya magari yenye thamani ya Sh.64,581,030 yalinunuliwa na kugawanywa kwenye magari ya Halmashauri. Hata hivyo, mafuta hayo hayakuthibitika kutumika kwenye magari hayo kutokana na taarifa hizo kutokuwa kwenye vitabu vya safari za gari pia madereva wa magari husika walikana kupokea mafuta hayo.
- (iii) Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo walitumia vibaya fedha za Elimu kiasi cha Sh.31,020,000, ikijumuisha tuhuma za wizi wa wino wa mashine ya chapa wenye thamani ya Sh.14,635,000 na wino wa mashine ya kutolea nakala wenye thamani ya Sh.16,385,000.
- (iv) Hati za malipo zenyetmene ya thamani ya Sh.766,489,920 hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, hivyo uhalali wa malipo yaliyofanyika kuititia hati hizo haukuweza kuthibitika.
- (v) Matukio sita yalibainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa yanayohusiana na ubadhirifu wa fedha kiasi cha Sh.277,026,849 uliosababishwa na udhaifu katika udhibiti wa mfumo wa ndani wa Halmashauri ambapo, usuluhisho wa benki ulifanywa na watumishi wasio waaminifu, pia haukutengenezwa kwa wakati
- (vi) Baadhi ya wakandarasi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa walikuwa wakipewa malipo ya awali kwa kiwango cha 30% hadi 70% ya fedha ya mkataba kinyume na kiwango cha 15% kilichoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma.
- (vii) Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imetumia jumla ya Sh.119,614,000 ili kukusanya kiasi cha Sh.57,226,690 hivyo kusababisha hasara ya Sh.62,387,110.
- (viii) Kiasi cha Sh.7,380,000 kilichopatikana kutokana na mauzo ya viwanja katika Mji wa Holili uliopo katika Halmashauri ya

Wilaya ya Rombo hazikuingizwa katika vitabu vya fedha vya Halmashauri. Kiasi hiki kinajumuisha Sh.2,785,000 ambazo zilitokana na wizi wa kutumia kalamu na Sh.4,595,000 zilizowekwa kwenye akaunti ya mtu binafsi.

**C. Muhtasari wa Mapendekezo**

Pamoja na mapendekezo ya kina yaliyotolewa kwenye ripoti za kila Halmashauri kwa mwaka wa ukaguzi, yafuatayo ni mapendekezo ya jumla:

**(i) Ukosefu wa mwongozo wa msingi wa mfumo wa udhibiti wa ndani**

Inapendezwa kwamba OWM-TAMISEMI iandae mfumo sahihi wa kuzisaidia Halmashauri katika kuandaa mfumo bora wa udhibiti wa ndani ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Hii inajumuisha utengenezaji wa sera za tekonomojo ya habari, Mfumo wa kujikinga na vihatarishi, Mkataba wa utendaji wa kamati ya Ukaguzi, mkataba wa utendaji wa ukaguzi wa ndani na miongozo mingine ya udhibiti wa ndani.

**(ii) Udhafu ulioonekana wakati wa ukaguzi maalum**

Pamoja na uimarishaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani kama ilivyopendekezwa hapo juu kama kipimo cha kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi wa kawaida na kaguzi maalum, Halmashauri zinashauriwa kuimarisha mfumo wa manunuza katika Halmashauri zao. Hii inajumuisha uandaaji wa tarifa za manunuza kwa mujibu wa sheria, kuzishauri Halmashauri kutumia huduma zinazotolewa na Wakala wa Manunuza wa Serikali (GPSA) ambao wana jukumu la kupanga na kusimamia manunuza ya bidhaa na huduma muhimu na huduma za manunuza kuitia mfumo wa makubaliano. Kwa ujumla, mfumo wa udhibiti wa fedha ndani ya Halmashauri unahitaji kusimamiwa mara kwa mara na kutathiminiwa.

**(iii) Mfuko wa maendeleo ya jimbo (CDCF)**

Huu ni mwaka wa kwanza wa uendeshaji wa mfuko wa maendeleo ya jimbo. Halmashauri inashauriwa kuhakikisha kuwa mfumo wa uwajibikaji unatekelezwa kwa mujibu wa sheria ya mfuko wa maendeleo ya jimbo Na. 16 ya mwaka 2009 na sheria zilizopo sasa kwa ajili ya kusimamia mali za umma. Kwa majimbo ambayo hayakutengeneza wala kuwasilisha taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo kuitia Halmashauri, OWM-TAMISEMI inashauriwa kulazimisha utekelezaji wa sheria husika kwa kuhakikisha kwamba hakuna matumizi yatakayofanyika kwa mwaka unaofuata kabla ya kuandaa taarifa ya mwaka uliotangulia.

**(iv) Kutowiana kwa taarifa za fedha na miongozo ya Serikali za Mitaa iliyopitwa na wakati**

Kama ilivyoshauriwa katika ripoti yangu iliyopita, OWM-TAMISEMI ifanye marekebisho ya sheria zilizopo na miongozo ili kuendana na Viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma pamoja na njia bora nyingine za utunzaji fedha.

Uongozi wa Halmashauri uwezeshwe na kuendelezwa kwa kufahamu wajibu wa pamoja juu ya uandaaji wa taarifa za fedha za Halmashauri husika. Hii inaweza kufanyika kama ilivyofanyika mwezi Agosti 2009 wakati Halmashauri zilipoingia kwenye Mfumo wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya umma (IPSSAs) kwa mara ya kwanza na OWM-TAMISEMI waliweza kuandaa mafunzo kwa baadhi ya maafisa.

**(v) Uandaaji wa taarifa za fedha na ukaguzi wa hesabu za Vijiji**

Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuchukua jukumu la kuongoza kuhakikisha masharti ya Sheria ya fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 inazingatiwa. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa uongozi wa kijiji husika unandaa taarifa za fedha na Halmashauri imteue mkaguzi

kwa ajili ya kutoa uhakika juu ya taarifa za fedha zilizotayarishwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria. Utaratibu huu unatarajiwa kuimarisha usimamizi na kuboresha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika viji.

- (vi) **Kujenga uwezo kwa uongozi wa serikali ngazi za chini**  
Uongozi wa Halmashauri unapaswa kuanzisha mpango wa mafunzo ambayo yatasaidia viongozi wa Vijiji na kamati za maendeleo za Miradi kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi ya maendeleo na wakati huo huo kuhakikisha kwamba kuna udhibiti sahihi juu ya ukusanyaji na matumizi ya mali ya umma.
- (vii) **Miradi iliyokamilika lakini haitumiki**  
Kuwepo kwa miradi iliyokamilika lakini haitumiki kunaashiria mipango duni na ukosefu wa taratibu za ufuatiliaji na tathmini katika ngazi ya Halmashauri. Uongozi wa Halmashauri ni vema uimarishe ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara ambayo itahakikisha kwamba ufuatiliaji unaimarishwa na changamoto zinatatuliwa haraka kwa ajili ya utekelezaji rahisi wa miradi iliyopangwa.
- (viii) **Mikopo ya watumishi iliyovuka kiwango isiyodhibitiwa na uongozi**  
Kukopa zaidi siyo tu ni uvunjaji wa sheria lakini pia ni kushusha morali kwa wafanyakazi wasiweze kufanya kazi kwa ufanisi. Viongozi wa Halmashauri waelimishwe ili kuhakikisha kuwa maombi ya mikopo ni lazime yapitishwe na Afisa Masuuli na kwamba makato ya kila mwezi ya mikopo yasizidi 2/3 ya mishahara halisi ya watumishi kwa mwezi. Pia, menejimenti iweke utaratibu wa kuhakikisha kwamba ufahamu kwa watumishi unaongezwa ili waelewe kwamba hawaruhusiwi kukopa mikopo zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa.
- (ix) **Uwajibikaji katika mifuko ya LGDG na NMSF**  
Taarifa juu ya fedha kuhamishiwa/kupelekwa Serikali za Mitaa lazima itolewe na taasisi husika (mfano Hazina) kwa

Halmashauri mara tu pesa hizo zinapopelekwa. Taarifa hii lazima iwe na ufanuzi wa wazi juu ya malengo ya fedha zilizotumwa. Utoaji wa fedha zilizoidhinishwa kwa wakati ni muhimu ili kuhakikisha shughuli zilizopangwa zinatekelezwa kwa wakati muafaka

- (x) **Uunganishaji wa taarifa za fedha za Serikali za Mitaa**  
Kutokana na ukweli kwamba zaidi ya 93% ya fedha za Serikali za Mitaa hupatikana kutoka Serikali Kuu na ukweli mwingine ni kwamba kuna hoja ya kuwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali anayeshughulikia Serikali za Mitaa; ni wakati muafaka kwamba taarifa ya utendaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwekwa wazi katika ujumla wake kama kianzio. Hii itakuwa ni nyongeza ya taarifa ambazo zimekuwa zikitengenezwa kwa kila Halmashauri. Mkusanyiko wa takwimu hizo itakuwa ni mchakato wa hatua ya maandalizi kwa ajili ya uunganishaji wa taarifa za fedha za serikali za mitaa kwa hapo baadae.
- (xi) **Haja ya Kuimarisha na Kuratibu Majukumu ya Usimamizi wa Sekretarieti za Mikoa**  
Kutokana na udhaifu mbalimbali uliobainika katika usimamizi wa fedha katika Serikali za Mitaa, kuna haja ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI kuhakikisha hatua sahihi zinachukuliwa dhidi ya maofisa ambao sio waadilifu au ambao wanashindwa kusimamia vizuri rasilimali za Serikali za Mitaa. Hatua zitakazochukuliwa zitasaidia kuimarisha utamaduni wa nidhamu ya fedha ndani ya Halmashauri. Pia, chini ya mageuzi ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi (D by D) Serikali kuu imegawa rasilimali kwa wingi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Serikali katika hali hii inafanya kazi katika falsafa ya “kusimamia bila kuingilia maamuzi” ili kuhakikisha uwepo halisi wa Ugatuaji wa madaraka kwa Wananchi.
- Ili kuwa na matokeo yanayotarajiwa katika Serikali za Mitaa, Serikali inatakiwa kuimarisha uratibu na majukumu ya usimamizi wa Makatibu Tawala wa Mikoa. Hii ni pamoja

na kuhakikisha kwamba, Sekretarieti za mikoa zinakuwa na uwezo unaotakiwa katika suala la kuwezesha ukuaji, kuinua maendeleo na kuzisimamia Serikali za Mitaa na utambuzi wa malengo na shabaha za Serikali za Mitaa kwa kulinganisha na malengo ya maendeleo ya Taifa.

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI NA MAMBO YA JUMLA

#### 1.1 Madhumuni ya Ukaguzi na Mwongozo wa Kisheria

##### 1.1.1 Madhumuni ya ukaguzi

Madhumuni ya kufanya ukaguzi wa hesabu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, ni kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa maoni ya kitaalamu kuhusiana na hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikiwa ni pamoja na:

- Kuhakikisha kuwa fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge na baraza la madiwani la Halmashauri husika zimepokelewa na kutumiwa kama ziliyyoidhinishwa.
- Kujiridhisha kuwa fedha zimekusanya vizuri na zimetumika kisheria kwa matumizi halali kama yalivyoidhinishwa katika bajeti na kwa kuzingatia taratibu za matumizi ya serikali yenye nia ya kuleta ufanisi na gharama zinazolingana na thamani ya fedha.
- Kuhakikisha kuwa taarifa za hesabu za mwisho za Serikali za Mitaa zimetayarishwa kwa kuzingatia miongozo na kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) pamoja na sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Memoranda ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1997.
- Kuhakikisha kuwa nyaraka zote muhimu, vitabu, rejesta, hesabu na taarifa mbalimbali zimehifadhiwa kwa ajili ya utendaji wa kila siku.
- Kuhakikisha kuwa kuna uwazi katika kuonyesha mali za kudumu na dhima katika taarifa za hesabu za Halmashauri.
- Kuhakikisha kuwa vifaa na huduma za Halmashauri zimenunuliwa kwa kufuata taratibu za manunuza na

kama zilivyoelezwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004, pamoja na Kanuni za mwaka, 2005.

- Kujiridhisha kuwa kitengo cha Ukagazi wa Ndani na Kamati ya Ukagazi inatekeleza majukumu yake vizuri kwa uhuru na kwamba udhibiti wa ndani unaridhisha na unategemewa.
- Kujiridhisha kuwa Bodi ya Zabuni na Kitengo cha Manunuzi kinatekeleza majukumu yake yaliyoainishwa na kwamba taratibu za manunuzi zinafuatwa katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
- Kuhakikisha kuwa malengo yaliyotegemewa au mafanikio yamepatikana na kwamba malengo yaliyowekwa na Bunge au chombo kingine kilichoidhinishwa yamefikiwa na endapo Halmashauri imetumia njia mbadala ya kufikia malengo kwa gharama nafuu zaidi.
- Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mapendekezo ya ukagazi kuhusu masuala ya ukagazi ya miaka ya nyuma pamoja na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) na kuona kuwa hatua sahihi zimechukuliwa kutohana na maswala yote ya ukagazi yaliyojitokeza.
- Kuona kuwa utawala bora umejengeka katika kufanikisha shughuli za kila siku za Halmashauri na katika kutekeleza malengo yote kwa ujumla.

#### **1.1.2 Msingi wa Kisheria unaomwongoza Mdhibiti na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Ukagazi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), na kifungu 45 cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) pamoja na kifungu Na.9 cha Sheria ya Ukagazi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, vinampa mamlaka Mdhibiti na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukagazi wa kawaida kwa nia

ya kujua jinsi matumizi ya fedha na rasilimali za Halmashauri zilivyotumika.

Ripoti hii imetayarishwa kwa mujibu wa Ibara 143 (4) ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005).

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara 143 (2) (c), ninatakiwa kukagua na kutoa taarifa, angalau mara moja kila mwaka, juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hesabu zinazotengenezwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hesabu zinazotengenezwa na Katibu wa Bunge.

Kwa upande mwingine, kifungu 45 (1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinabainisha kuwa, hesabu za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinapaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia, Kifungu Na. 10 (1) ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2008 kimempa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Zaidi ya hayo, kifungu cha 45 (5) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) kinaitaka kila Mamlaka kumruhusu Mkaguzi kukagua fedha, vitega uchumi au rasilimali nyingine ambazo zinamilikiwa au zilizo chini ya udhibiti wa Halmashauri ambazo ni hesabu, vitabu, hati za malipo na nyaraka zote zinazohusiana.

Aidha, kifungu cha 48 (1), (2) na (4) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 kinabainisha kwamba “Mkaguzi ataandaa na kusaini ripoti ya Ukaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhusu mizania ya hesabu ya mwaka na taarifa nyingine zinazohusiana nazo, ambapo nakala moja

ya kila ripoti pamoja na mizania ya hesabu na taarifa nyingine zinazo husiana nazo zitapelekwa kwa Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkurugenzi ambaye ataziwasilisha kwenye Baraza la Madiwani”.

Kifungu hiki pia kinanitaka kufanya yafuatayo:

- (a) Kubainisha kila kipengele cha matumizi ambacho kimefanyika bila kuidhinishwa na sheria au ambacho hakikuruhusiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- (b) Kubainisha mapungufu au hasara ambayo imetokea aidha kwa uzembe au mtu yejote kushindwa kutoa taarifa ya matumizi ya fedha alizokabidhiwa;
- (c) Kuthibitisha kiasi cha matumizi batili, upungufu au hasara ambayo haijaoneshwa vitabuni;

Matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa yamewasilishwa kwa wenyeviti husika na nakala zimepelekwa kwa Wakurugenzi ambao pia ni Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Taarifa hii ni muhtasari wa matokeo ya mambo yaliyojitekeza katika taarifa za Ukaguzi kwa kila Halmashauri.

Huu ni mwaka wa pili kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kutengenezwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs), pamoja na kipengele cha (iv) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na pia kulingana na Agizo Na. 53 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka, 1997 kama msingi wa utayarishaji wa taarifa za hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Seti ya kwanza ya taarifa za fedha ziliyowasilishwa kwa kutumia IPSASs ni zile za mwaka 2008/2009.

Seti kamili ya taarifa za fedha zinazotayarishwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma ni pamoja na:

- a) Mizania ya hesabu

- b) Taarifa ya mapato na matumizi
- c) Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji;
- d) Taarifa ya mtiririko wa fedha;
- e) Taarifa ya uwiano wa bajeti na hali halisi ya aina ya matumizi kama yalivyojitekeza
- f) Taarifa ya uwiano wa bajeti na hali halisi ya matumizi ya kiidara
- g) Vielekezi vyta taarifa za fedha

Kwa sababu za uwazi na uwajibikaji, Kifungu Na.49 cha Sheria ya Fedha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, 1982 (iliyorekebishwa 2000) kama ilivyofafanuliwa katika Agizo Na.90 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 ambalo linaitaka Halmashauri kutangaza katika ofisi zake na katika gazeti la eneo lake mambo yafuatayo:

- (i) Mizania jumuifu na taarifa ya mapato na matumizi (muhtasari wa hesabu) iliyokaguliwa na
- (ii) Ripoti yoyote ya Ukaguzi iliyosainiwa na Mkaguzi kuhusu hesabu hizo

Aidha, kuridhia na kuchapishwa hesabu na ripoti za ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni fursa nyingine kwa Mamlaka hizo kuongeza mawasiliano kwa upana zaidi na wakazi wa maeneo yao, kuhusu mafanikio na mwelekeo wao wa baadae.

## **1.2 Viwango na taratibu zinazotumika kutoa taarifa ya Ukaguzi**

### **1.2.1 Viwango vinavyotumika wakati wa Ukaguzi**

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi za Ukaguzi (INTOSAI) na Shirika la Afrika la Asasi Kuu za Ukaguzi zinazotumia lugha ya Kiingereza (AFROSAI-E). Ikiwa kama mwanachama wa mashirika hayo ya Kimataifa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inawajibika kutumia

viwango vya ukaguzi vilivyotolewa na INTOSAI na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) kama vilivyotolewa na Shirikisho la Wahasibu la Kimataifa (IFAC) wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilikagua na kuhakiki kwa undani taarifa za fedha pamoja na viambatanisho vyake kuweza kubaini uhalali wa matumizi hayo katika Halmashauri. Mwishoni mwa ukaguzi hati mbalimbali zilitolewa kuhusiana na taarifa za fedha kulingana na matokeo ya ukaguzi.

Kwa kuzingatia Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005), ripoti hii imewasilishwa kwa Rais wa Jamhuri wa Tanzania na baadae kuwasilishwa Bungeni.

### **1.2.2 Taratibu zinazotumika kutoa taarifa**

Wakati wa ukaguzi wangu, utoaji taarifa na ufuatiliaji ni maeneo muhimu ambayo hayawezi kutenganishwa na yanapewa uzito sawa.

Kabla ya kutoa ripoti ya mwaka, hatua mbalimbali zimefuatwa. Ni vyema kuzionesha wazi hatua hizi kwa watumiaji wa ripoti hii waweze kuielewa vizuri ripoti ya mwaka na kuafiki hatua zilizofuatwa.

Hatua hizi zinahitaji kuwe na mawasiliano ya kutosha na uongozi wa taasisi inayokaguliwa, ikiwa ni utaratibu muhimu katika kufanya ukaguzi shirikishi. Baadhi ya hatua zilizofuatwa wakati wa ukaguzi ni kama ifuatavyo:

- Kutoa barua ya kuanza ukaguzi kwa mkaguliwa inayoeleza aina na mawanda ya ukaguzi.
- Kuandaa mpango mkakati wa ukaguzi unaoonesha mwelekeo mzima wa ukaguzi na vigezo vitakavyotumika katika hatua za mwanzo za kutathmini taasisi inayo kaguliwa.

- Kufanya kikao cha kwanza na uongozi wa taasisi inayokaguliwa kabla ya kuanza ukaguzi. Kikao hiki kinanipa nafasi ya kuueleza uongozi madhumuni na malengo ya kufanya ukaguzi. Kikao hiki pia kinanipa nafasi ya kukutana na watendaji kwa ajili ya mawasiliano muhimu.
- Kutoa barua au hoja za ukaguzi kwa uongozi kwa kipindi cha kati inayoonesha matokeo ya ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kuzijibu wakati wa ukaguzi na hata baada ya ukaguzi.
- Kutoa barua ya ukaguzi ya mwisho inayoonesha mapungufu yote yaliyojitekeza wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kuyashughulikia mapungufu hayo. Hatua hii pia ni ya msingi katika kutayarisha ripoti ya mwaka.

Taratibu zinazotumika kutoa taarifa katika sekta ya umma zikiwemo mamlaka ya Serikali za mitaa haziishii kutoa ripoti ya ukaguzi tu ni pamoja na ufuatiliaji wa taratibu zenyewe. Kifungu cha 40 cha Sheria ya Ukaguzi ya Umma, 2008 inatoa mwongozo wa ufuatiliaji Tanzania. Madhumuni ya ufuatiliaji wa taratibu hizo ni kuweza kutambua na kutoa taarifa endapo mkaguliwa anao mpango wake wa kazi au amezingatia ushauri uliotolewa katika ripoti ya ukaguzi. Kutokana na kifungu cha 40(4) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 inanitaka kuonesha hali halisi ya utekelezaji katika kaguzi zinazofuata.

### **1.3 Idadi ya ofisi zinazokaguliwa na mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

#### **1.3.1 Idadi ya ofisi zinazokaguliwa**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010, kulikuwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa 134 katika Tanzania bara ambazo zilikaguliwa na kutolewa ripoti ya ukaguzi kwa kila Halmashauri husika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina


hadhi tofauti kuanzia Halmashauri za Wilaya hadi Halmashauri za Jiji kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| <b>Na.</b> | <b>Halmashauri</b>      | <b>Jumla</b> | <b>Asilimia</b> |
|------------|-------------------------|--------------|-----------------|
| 1.         | Halmashauri za Jiji     | 4            | 3               |
| 2.         | Halmashauri za Manispaa | 17           | 13              |
| 3.         | Halmashauri za Miji     | 7            | 5               |
| 4.         | Halmashauri za Wilaya   | <u>106</u>   | <u>79</u>       |
|            |                         | <u>134</u>   | <u>100</u>      |

### **1.3.2 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Wateja wangu (Mamlaka za Serikali za Mitaa) wana hudumiwa na ofisi 24 za ukaguzi zilizopo mikoani kote Tanzania bara ambazo zinawajibika kukagua hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ofisi hizi za mikoani zinaongozwa na Wakaguzi Wakazi ambao wanasmamiwa na Wakaguzi wa Kanda. Kwa madhumuni ya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, mikoa imegawanyika katika kanda chini ya uangalizi wa Wakaguzi wa Kanda ambao nao pia wanasmamiwa na Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu (Mikoa). Kutokana na muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu (Mikoa) anawajibika moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa madhumuni ya ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi hivi sasa inazo Kanda tano (5) kama inavyoonekana katika sehemu ya muundo wa ofisi hapa chini.



#### **1.4 Majukumu ya kisheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuandaa Taarifa za Fedha**

Menejimenti ya kila Halmashauri inawajibu wa kuandaa na kuonesha kwa usahihi taarifa za fedha kwa kufuata udhibiti wa ndani ambao menejimenti imejiwekea katika kuandaa taarifa za fedha ambazo hazina dosari kutokana na udanganyifu au makosa mengine.

Kifungu Na.40(1) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za mitaa Na.9 ya 1982 (Iliyorekebishwa 2000) inaeleza kuwa kila Mamlaka ya Serikali za mitaa ina wajibu wa, kuwa na kutunza vitabu vyta hesabu na rekodi zinazohusu:

- (a) Mapato na matumizi ya fedha na miamala mingine ya fedha ya Mamlaka.
- (b) Mali na dhima za Mamlaka, na kutayarishwa kila mwaka wa fedha, mizania inayoonesha maelezo ya mapato na matumizi ya mamlaka na mali zake zote na dhima.”

Kifungu kilichotajwa hapo juu kimehuishwa na Agizo Na.9 mpaka 16 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 inayotaka Halmashauri kuanzisha na kusimamia udhibiti wa ndani wa shughuli za Halmashauri. Kwa nyongeza, Agizo Na.53 inaweka majukumu kwa menejimenti ya Halmashauri kuandaa taarifa za fedha kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo inayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuzingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu kwa sekta ya umma (IPSASs).

Pamoja na majukumu ya uaandaaji wa taarifa za hesabu, Kifungu Na.49 Sheria ya fedha ya Serikali za mitaa Na. 9 ya 1982(Iliyorekebishwa 2000) inaitaka kila Mamlaka ya Serikali ya mtaa kuchapisha taarifa za fedha zilizokaguliwa ndani ya maeneo yao ya uwajibikaji. Mahitaji ya uchapishaji yameainishwa Agizo Na.90 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997.

## SURA YA PILI

### 2.0 AINA, VIGEZO NA MWELEKEO WA HATI ZA UKAGUZI

#### 2.1 Vigezo vya hati za ukaguzi zilizotolewa

Katika kutekeleza matakwa ya Kisheria, ninawajibika kutoa uhakika kwa wadau wa Halmashauri kwamba taarifa za fedha zilizotayarishwa na Halmashauri zinatoa picha halisi ya matokeo ya shughuli zilizofanyika, matokeo ya matumizi ya fedha, mtiririko wa fedha na mizania ya fedha za Halmashauri kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. Maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa mtumiaji kama uhakikisho wa usahihi wa hesabu za fedha za Halmashauri pamoja na uzingatiaji wa taratibu zinazotakiwa.

Kulingana na viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi (ISA) na Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) hati za Ukaguzi zifuatazo zinatolewa kama kipimo cha kutathmini usahihi wa hesabu za fedha. Hati hizi ni; hati zinazoridhisha, hati zinazoridhisha zenyе masuala ya msisitizo na masuala mengine, hati zenyе shaka, Hati Zisizoridhisha na hati mbaya. Sura hii inajumuisha idadi za Halmashauri zilizopata aina ya hati za ukaguzi katika mwaka uliokaguliwa. Sababu za kina za kutoa aina ya hati ya ukaguzi zimeelezwa kwa kina katika kila ripoti iliyotolewa kwa Halmashauri husika.

#### 2.2 Hati za Ukaguzi

##### 2.2.1 Maana ya Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi ni maoni ya mkaguzi yanayoeleza iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa zimetayarishwa kwa kutumia sera za hesabu za fedha kwa mujibu wa sheria zinazohusika, kanuni au viwango/misingi ya hesabu za fedha vinavyotumika.

Maoni hayo hayana budi kuonesha iwapo kuna maelezo ya kutosha au la, juu ya mambo muhimu kwenye taarifa za fedha kuzifanya zieleweke vizuri na kwa upana zaidi.

Kwa madhumuni ya uwajibikaji na uwazi kwa Bunge, bila ya kujali aina ya maoni yaliyotolewa kwa taarifa husika za ukaguzi, matokeo ya ukaguzi yametolewa pamoja na athari zake, mapendekizo, jibu la mkaguliwa na maoni ya wakaguzi juu ya jibu lililotolewa. Naamini kwamba aina hii ya utoaji wa matokeo ya Ukaguzi unasaidia kutekeleza majukumu ya Afisa Masuuli katika utayarishaji wa taarifa za fedha na kwangu pia.

### **2.2.2 Aina za Hati za Ukaguzi**

Hapa natoa maelezo ya kina juu ya aina za hati za Ukaguzi zinazotolewa kama ifuatavyo:

#### **2.2.2.1 Hati Inayoridhisha**

Hati ya aina hii inatolewa wakati nimeridhika kuwa, taarifa za hesabu za Halmashauri, Idara au Wakala hazina makosa kwa maeneo yote muhimu; na pia zimetayarishwa kulingana na kanuni na viwango vya uhasibu.

Hata hivyo, utoaji wa hati inayoridhisha haina maana kwamba Halmashauri ina mfumo safi kabisa wa udhibiti wa ndani, bali aina hii ya hati ina maana kwamba hakuna jambo lolote nililoliona ambalo lingesababisha kutolewa kwa hati yenye shaka. Kila Halmashauri iliyopata aina hii ya hati imeandikiwa taarifa nyingine kwa ajili ya menejimenti inayoeleza masuala ambayo yasipoangaliwa, yanaweza kuisababishia Halmashauri kupata hati yenye shaka miaka ijayo.

### **2.2.2.2 Masuala yenyé msisitizo na masuala mengine**

Masuala ya msisitizo na masuala mengine ni mambo ya ziada kuitia ripoti za ukaguzi wakati mkaguzi anapoona inafaa:

- (a) Kuwaelewesha watumiaji wa taarifa za fedha zilizoandaliwa katika suala au masuala yaliyooneshwa ndani ya taarifa hizo ambazo ni muhimu na ni za msingi.
- (b) Kuwaelewesha watumiaji wa taarifa za fedha zilizoandaliwa katika suala au masuala ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuelewa vizuri mambo yaliyojiri katika ukaguzi, mbali na yale yaliyooneshwa kwenye taarifa za fedha.

#### **(i) Masuala yenyé msisitizo**

Katika nyakati nyingine nimeongezea aya ya masuala yenyé msisitizo katika masuala yaliyoonesha vizuri katika tarifa za fedha lakini kuna mambo muhimu na ya msingi kwa watumiaji ambayo yanahitaji maelezo ya ziada kwa ufanuzi.

Aya ya msisitizo wa masuala inambatisha kwa kila hali, maelezo ya uzingativu wa suala au masuala yaliyooneshwa katika taarifa za fedha na kwamba ni muhimu na yenyé msingi kwa watumiaji kuweza kuelewa taarifa za fedha. Lengo kuu la msisitizo wa suala ni kuleta karibu uelewa wa hali halisi wa taarifa za hesabu hususani yale masuala yaliyooneshwa katika taarifa za fedha.

Aya ya msisitizo wa masuala inatakiwa ijumuishwe katika mazingira yafuatayo:

- Kuweka angalizo juu ya mambo yanayoweza kuwa na athari katika taarifa za fedha baadae na ambayo yako

nje ya uwezo wa Halmashauri kuyadhibiti yasitokee, mfano madeni yasiyolipika na kesi zilizopo mahakamani.

- Kuweka angalizo katika mambo yasiyowiana kwa maelezo yaliyomo ndani ya taarifa za fedha ya mwaka ambapo dosari hizo zinahitaji marekebisho na Halmashauri ikashindwa kufanya marekebisho hayo.
- Kuweka angalizo katika masuala yaliyooneshwa na yanayoathiri taarifa za fedha ambayo ni muhimu yaeleweke kwa watumiaji wa taarifa hizo kama vile majanga makubwa yanayoweza kutokea na kuleta madhara makubwa ya hali ya kifedha katika Halmashauri.

#### (ii) **Masuala mengine**

Aya ya masuala mengine inahusu masuala ambayo hayakuoneshwa katika taarifa za fedha na kwamba kwa mtazamo wa mkaguzi ni muhimu mtumiaji wa taarifa za fedha kuelewa ukaguzi, majukumu ya mkaguzi au ripoti ya mkaguzi.

Endapo mkaguzi ataona inafaa kuwasilisha masuala mengine kuliko yale yaliyooneshwa katika taarifa za hesabu, mkaguzi anatumia aya ya masuala mengine iliyopo baada ya aya ya hati ya ukaguzi yenyewe masuala ya msisitizo. Haya maswala mengine yapo katika sehemu tofauti ya ripoti ya mwaka ya ukaguzi ili kutenganisha wazi wazi kutoka katika majukumu ya mkaguzi, na hati ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha na masuala mengine yaliyokuwa na angalizo katika aya zilizotangulia za msisitizo wa masuala.

Mifano ya masuala mengine ni pamoja na kutofuata sheria na udhaifu katika udhibiti wa ndani.

### **2.3 Misingi ya kutoa hati mbali na hati inayoridhisha**

Katika hali ya kawaida, misingi ya kutoa hati mbali na hati inayoridhisha ni kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Hali ya mazingira                                  | Muhimu lakini si ya msingi | Muhimu na ya msingi |
|--|----------------------------|---------------------|
| Kutokukubaliana                                    | Hati yenyeshaka            | Hati Isiyoridhisha  |
| Isiyotegemewa<br>Vizuizi katika mawanda ya ukaguzi |                            | Hati Mbaya          |

#### **2.3.1 Hati yenyeshaka**

Hati yenyeshaka inatolewa iwapo ninaridhika kuwa hati inayoridhisha haiwezi kutolewa lakini kutokana na kutokubaliana na menejimenti au kuzuiwa kwa mawanda ya ukaguzi ambapo athari yake ni muhimu lakini si ya msingi na kwamba ukiacha athari zilizopelekeza kutoa hati yenyeshaka, taarifa za hesabu zitakuwa zimetengenezwa kulingana na misingi ya utayarishaji wa hesabu na hazipotoshi. Kwa upande mwingine, ninatoa hati hiyo nisipokubaliana na menejimenti katika eneo moja au jingine la tarifa za fedha, lakini dosari hizo hazina athari katika tarifa zote za fedha kuwa hazijatayarishwa kama inavyotakiwa.

#### **2.3.2 Hati Isiyoridhisha**

Hati Isiyoridhisha inatolewa ninapothibitisha kwamba kuna utofauti amba ni muhimu kiasi cha kutokubaliana na menejimenti na ni ya msingi kwenye taarifa za fedha kiasi kwamba taarifa hizo hazikutayarishwa kulingana na misingi inayokubalika ya utayarishaji wa taarifa za fedha au zinapotosha kabisa.

Hati Isiyoridhisha hutolewa pale ambapo hati yenyeshaka haitoshelezi kuonesha maeneo yaliyopotoshwa katika taarifa za fedha.

### **2.3.3 Hati mbaya**

**2.3.3.1**Hati mbaya hutolewa wakati ninaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusiana na tarifa za fedha zilizoandaliwa na kutayarishwa kwa ajili ya ukaguzi na hivyo kushindwa kutoa maoni juu ya taarifa za fedha zilizowasilishwa. Hali hiyo inaathiri kwa kiasi kikubwa taarifa za fedha kiasi ambacho ninashindwa kutoa maoni yangu juu ya tarifa hizo.

Aina hii ya hati, inatolewa pale tu ambapo kuna mapungufu makubwa katika taarifa za fedha ambayo yanapelekea mkaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha zilizowasilishwa.

Wakati hati mbaya inapotolewa juu ya taaarifa za fedha, mambo ambayo hayajulikani au kutoridhisha kuhusu uwasilishwaji wa taarifa za fedha kwa kuzingatia mfumo wa utayarishaji wa taarifa husika yanahitaji kuoneshwa

### **2.3.4 Hali inayosababisha kupata hati mbali ya hati inayoridhisha**

#### **(a) Vizuizi katika mawanda ya Ukaguzi**

Pale ambapo nashindwa kupata taarifa za kutosha au nyaraka zinazohusiana na uandaaji wa taarifa za fedha au vizuizi katika mawanda ya ukaguzi na kushindwa kutoa maoni, na kwa sababu hizo, mambo yafuatayo yanaweza kujitokeza:

- Malipo kufanywa bila hati za malipo;
- Vifaa au huduma kununuliwa bila kuwa na hati za mapokezi ya vifaa hivyo kutothibitisha kupokelewa kwa vifaa au huduma hizo
- Malipo kufanywa bila kuwa na viambatisho sahihi;

- Vitabu vya kukusanya maduhuli kutowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi;
- Mali inayomilikiwa au iliyonunuliwa kutokuwa na mchanganuo wa mali hizo. Hii inaleta shaka juu ya uwepo wa mali hizo;
- Kutopatikana kwa ushahidi wa kupokelewa kwa fedha toka kwa walipwaji (Kukosekana kwa nyaraka za kukiri kupokea malipo);
- Kutopatikana kwa nyaraka muhimu za fedha;
- Vifaa vilivyonunuliwa na kulipiwa bila kuingizwa kwenye leja ya vifaa.
- Kutoonesha bakaa ya fedha iliyopo benki katika vitabu vya hesabu.

**(b) Kutokubaliana katika namna bora ya utunzaji wa kumbukumbu na kutokuzingatia sheria na kanuni**

Agizo Na.9 hadi 16 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaagiza Halmashauri kuanzisha na kusaidia mfumo wa udhibiti wa ndani ulio madhubuti. Pia Agizo Na.53 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 linaitaka menejimenti ya Halmashauri kuzingatia kanuni zinazokubalika za uhasibu wakati wa kutayarisha taarifa za fedha kwa kufuata Sheria, Kanuni, Maagizo yanayotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Kutokubaliana na menejimenti kuhusu kanuni bora za utunzaji wa kumbukumbu na kuzingatia sheria kunajitokeza katika hali zifuatazo:

- Mali zinazomilikiwa na Halmashauri kutoingizwa Katika rejista ya mali za kudumu
- kumbukumbu za hesabu kuachwa, kukosewa au kutokamiliaka.
- Mapungufu katika kuonesha sera za uhasibu zinazotumika;

- Halmashauri kutumia njia na kanuni za uhasibu zisizo sahihi kama vile utumiaji wa viwango visivyo sahihi vyatuchakavu;
- Manunuzi ya mali, ujenzi na huduma bila kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 na kanuni zake.
- Menejimenti imeshindwa au haikubaliani na marekebisho ya dosari zilizoonekana na mkaguzi

#### **2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi katika Halmashauri**

Sehemu hii ya ripoti inaonesha mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa miaka miwili 2008/2009 na 2009/2010. Madhumuni ya taarifa hii ni kulinganisha hali ya utendaji wa kifedha katika Halmashauri kwa kipindi cha miaka miwili.

Sababu za Halmashauri kuendelea kupata hati zenyeshaka na zisizoridhisha kunasababishwa na mambo makubwa yafuatayo:

- Taarifa za hesabu zilizowasilishwa zinakosa maeleo ya kutosha na kwamba baadhi ya vipengele havikuoneshwa ipasavyo kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu wa Sekta ya Umma, na kuleta ugumu katika kupima ufanisi wa Halmashauri husika.
- Kukosekana kwa usimamizi wa karibu kwa upande wa menejimenti katika utekelezaji na uendelezaji wa miradi inayoanzishwa katika ngazi za chini za Serikali kama vile Vijiji na Kata. Halmashauri zinapeleka fedha nyingi Vijijini na kwenye Kata bila kufutilia.
- Ongezeko la fedha zinazopelekwa Halmashauri chini ya mpango wa ugatuaji madaraka kwa wananchi (D by D) ambao unahitaji kuwepo na uwezo wa kutosha wa usimamizi wa fedha.
- Kuongezeka kwa kutofuata mifumo ya udhibiti wa ndani iliyopo.

Kulingana na mchanganuo huu, ninaweza kuhitimisha kama ifuatavyo:

- (i) Idadi ya hati inayoridhisha imepungua kutoka 77 (58%) kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2008/09 hadi 65 (48.5%) kwa kipindi cha mwaka (2009/2010).
- (ii) Idadi ya hati zenyе shaka imeongezeka kutoka 55 (41%) mwaka imeongezeka kutoka hadi 65 (48.5%) kwa kipindi cha mwaka (2009/2010).
- (iii) Idadi ya Hati Zisizoridhisha imeongezeka kutoka 1 (1%) mwaka 2008/2009 hadi 4 (3%) kwa kipindi cha mwaka (2009/2010).
- (iv) Kama hali ilivyokuwa mwaka uliopita, hakuna Halmashauri iliyopata hati mbaya kwa kipindi cha mwaka (2009/2010).

Halmashauri nyingi zilizopata hati zisizoridhisha na Hati Zisizoridhisha zilichangiwa na mambo yafuatayo:

- Hakuna uhakiki wa mara kwa mara unaofanywa na menejimenti za Halmashauri kwenye mishahara na matokeo yake mishahara imekuwa ikilipwa kwa watumishi ambao hawapo kazini (wamefariki dunia, wamestaifu, wamefukuzwa au wameacha kazi) kuitia akaunti za benki zao bila kugundulika.  
Hati za malipo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na nyingine hazikuwa na nyaraka za kutosha kuthibitisha uhalali wa malipo kama inavyotakiwa na agizo Na 5(c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kutokana na hali hiyo hatukupata uhakika kuwa malipo yaliyofanyika yanahusika na shughuli za Halmashauri.
- Vitabu vya kupokelea maduhuli havikuwasilishwa kwa ajili ya Ukaguzi kinyume na agizo Na.101 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 1997.
- Makosa katika taarifa za fedha yatokanazo na kunakili vibaya miamala na kutofua taratibu za kihasibu.

- Taarifa za mtiririko wa fedha katika sehemu ya uuzaji na ununuaji mali umenakiliwa isivyopaswa kutohana na kuwa na tarakimu zisizo sahihi za mapato kutoka katika ruzuku ya mapato ya miradi ya maendeleo.

Maelezo hayo hapo juu yamechambuliwa kwa muhtasari kwenye jedwali lifuatalo:


**Mchanganuo wa hati za maoni ya Ukaguzi zilizotolewa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010**

| Halmashauri             | Hati zinazoridhisha |         | Hati zenye mashaka |         | Hati Isiyoridhisha |         | Jumla   |         |
|-------------------------|---------------------|---------|--------------------|---------|--------------------|---------|---------|---------|
|                         | 2008/09             | 2009/10 | 2008/09            | 2009/10 | 2008/09            | 2009/10 | 2008/09 | 2009/10 |
| Halmashauri za Majiji   | -                   | -       | 4                  | 4       | -                  | -       | 4       | 4       |
| Halmashauri za Manispaa | 10                  | 8       | 7                  | 9       | -                  | -       | 17      | 17      |
| Halmashauri za mijji    | 4                   | 1       | 2                  | 6       | -                  | -       | 6       | 7       |
| Halmashauri za Wilaya   | 63                  | 56      | 42                 | 46      | 1                  | 4       | 106     | 106     |
| Jumla                   | 77                  | 65      | 55                 | 65      | 1                  | 4       | 133     | 134     |
| Asilimia                | 58%                 | 48.5%   | 41%                | 48.5%   | 1%                 | 3%      | 100%    | 100%    |


Mchanganuo wa hati za maoni ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 unaweza kuoneshwa katika chati mihimili kama ifuatavyo:



Chati Mihimili iliyopo juu inaonesha kupungua kwa Halmashauri zenye hati zinazoridhisha na wakati huo hakuna Halmashauri ya Jiji au Mji iliyopata hati inayoridhisha kwa kipindi cha mwaka 2009/2010.



Chati Mihimili iliyopo juu inaonesha kuongezeka kwa Halmashauri zilizopata hati zenye shaka kwa kila aina ya Halmashauri wakati huo, Halmashauri (4) za Jiji zimepata hati zenye shaka kwa miaka miwili mfululizo.



Chati Mihimili iliyopo juu inaonesha kuongezeka kwa Halmashauri zenye Hati Zisizoridhisha kwa upande wa Halmashauri za Miji na Halmashauri za Wilaya.

Ukaguzi wetu umegundua mambo muhimu ya kutokubaliana yaliyosababisha mapungufu katika kuandaa na kuonesha taarifa za fedha zisizosahihi. Halmashauri 4 za Wilaya zilizopata Hati Zisizoridhisha ni kama ifuatavyo:

| Na. | Halmashauri                     | Sababu   |
|-----|---------------------------------|--|
| 1   | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga | <ul style="list-style-type: none"> <li>Vitabu 8 vya wazi vya kukusanya mapato (HW5) na vitabu 28 vyenye thamani ya Sh.8,000,000 havikupatikana wakati wa ukaguzi. Mapato yaliyokusanywa kwa kutumia vitabu hayakuweza kuthibitishwa ndani ya vitabu hivyo.</li> <li>Mali za kudumu ambazo hazikuonekana na ambazo hazimilikiwi na Halmashauri zimeingizwa katika rejestra ya mali za kudumu na kufanya jumla ya mali hizo kuongezeka kwa kiasi cha Sh.336,104,842.</li> <li>Ukaguzi wa hati za malipo umebaini kuwepo kwa malipo yaliyofanyika bila</li> </ul> |

|   |                             |  |
|---|-----------------------------|--|
|   |                             | <p>kuwa na viambatanisho, kwa hiyo matumizi ya kiasi cha Sh.137,135,443 hayahakuweza kuthibitika.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Mapato yaliyokusanya katika vyanzo vya Maliasili na Stendi ya mabasi hayakuwasilishwa Makao Makuu ya Halmashauri. Mapato ambayo hayakukusanya, yamesababisha kupungua kwa Sh.15,620,000 katika mapato yote.</li> <li>• Vifaa vyenye thamani ya Sh.27,183,900 vilivyonunuliwa kwa kufuata taratibu za manunuzi havikuingizwa kwenye leja ya vifaa na kusababisha upungufu wa jumla ya vifaa katika taarifa za fedha kiasi cha Sh.27,183,900.</li> <li>• Magari yenye thamani ya kununulia Sh.151,870,574 yaliyotolewa uchakavu na yakabaki bila thamani kabisa yameoneshwa kwenye mizania ya hesabu bila thamani wakati magari hayo bado yana hali nzuri na yanatumika. Hakuna juhudhi iliyofanywa ya kuthaminisha magari hayo ili yawe na thamani halisi kwa sasa. Hali hii imesababisha kupungua kwa thamani ya mali, vifaa na mitambo kwa kiasi hicho hicho.</li> </ul> |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya Rombo | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Salio la mali za kudumu lililooneshwa kwenye mizania ya hesabu za kuishia tarehe 30 Juni, 2010 halikuwa na vielekezi vya taarifa za fedha hivyo kushindwa kujua usahihi wa hesabu hizo zilizowasilishwa.</li> <li>• Salio la fedha katika mizania ya hesabu za kuishia tarehe 30 Juni, 2010 lina upungufu wa kiasi cha Sh.24,493,212.</li> <li>• Mishahara yenye jumla ya Sh.28,043,644 ya watumishi 42 waliostaafu 5 waliofariki imeendelea kutokea kwenye orodha ya mishahara ya Halmashauri na kulipwa kupitia</li> </ul>  |

|   |                                |  |
|---|--------------------------------|--|
|   |                                | <p>akaunti zao za benki.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri imelipa jumla ya Sh.18,313,962 kwenye taasisi mbalimbali za fedha ikiwa ni kulipa madeni ya mikopo ya waliokuwa watumishi wa Halmashauri.</li> <li>• Mizania ya hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2009 imeonesha salio ishia la madeni ya muda mfupi la Sh.17,244,256 bila kuonesha kama salio anzia kwa mwaka 2010 na kusababisha upungufu wa kiasi hicho hicho katika taarifa za fedha.</li> <li>• Halmashauri imelipa jumla ya Sh.35,745,856 kwa ajili ya kusafirisha chakula cha njaa kutoka hifadhi ya chakula Arusha kwenda Vijijini. Hata hivyo, malipo hayo yalifanyika kutoka katika akaunti ya Kilimo badala ya Akaunti ya Amana ambamo fedha hizo zilipokelewa. Hakuna ushahidi kuwa fedha hizo zimerejeshwa kwenye Akaunti iliyolipa.</li> <li>• Halmashauri ilihamisha jumla ya Sh.304,051,834 kwenda ngazi ya chini ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hakuna stakabadhi za kukiri mapokezi iliyopatikana pamoja na taarifa za matumizi ya fedha hizo.</li> </ul> |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Vitabu 101 vya kukusanya mapato havikupatikana wakati wa ukaguzi, Kwa hali hiyo mapato yaliyokusanya kwa kutumia vitabu hivyo hayakuweza kuthibitishwa.</li> <li>• Ukaguzi wa stakabadhi za mapato na taarifa za benki za Akaunti ya Mfuko Mkuu imeonesha kiasi cha Sh.149,033,336 hakikupelekwa benki.</li> <li>• Hati za malipo zenye jumla ya Sh.144,994,981 hazikupatikana wakati wa ukaguzi kwa hiyo uhalali wa malipo</li> </ul>  |

|  |  |   |
|--|--|---|
|  |  | <p>yaliyofanyika hayawezi kuthibitishwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri haikuandaa taarifa ya matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. Kukosekana kwa taarifa hiyo fedha zilizopokelewa na kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazikuweza kuthibitishwa.</li> <li>• Kinyume cha Agizo Na. 5(c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, (1997) malipo ya jumla ya Sh.449,681,752 hayakuwa na viambatanisho.</li> <li>• Tarakimu zilizooneshwa katika taarifa za fedha zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka 2009/2010 hazikuwa na vielekezi na michanganuo kwa ajili ya usahihi wake.</li> <li>• Mali za kudumu zenyе thamani ya jumla ya Sh.251,724,000 zilizoingizwa kwenye orodha ya mali zilizohesabiwa lakini hazijaoneshwa kwenye taarifa ya mizania ya hesabu inayoishia tarehe 30 Juni, 2010.</li> <li>• Taarifa ya mizania ya hesabu inaonesha kuwa thamani ya Mali, Mitambo na Vifaa ni Sh.7,586,056,782 tofauti na Sh.7,709,278,581 zilizoonekana kuwa sahihi wakati wa ukaguzi. Tofauti ya Sh.123,221,799 haijarekebishwa.</li> <li>• Mizania ya hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni,2009 imeonesha bakaa la fedha la Sh.3,042,262,002 wakati takwimu sahihi ni Sh.3,031,858,932 na kusababisha</li> </ul> |
|--|--|---|

|   |                                  |   |
|---|----------------------------------|---|
|   |                                  | tofauti ya Sh.10,403,070 ambazo hazijarekebishwa.   |
| 4 | Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Hati za malipo yeye jumla ya Sh.1,393,123,804 sawa na asilimia 12.7 ya matumizi yote hazijawasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Kwa kukosekana hati hizo na viambatanisho vyake uhalali wa malipo hayo hauwezi ukathibitishwa.</li> <li>• Ukaguzi wa daftari la fedha na usuluhisho wa benki umebaini kuwa kulikuwa na malipo yasiyofahamika Sh.754,064,592 yaliyolipwa na Halmashauri kutoka katika akaunti za benki mbalimbali na kuoneshwa kwa makosa kama rasilimali fedha zilizomilikiwa hadi ukomavu. Hata hivyo aina ya malipo hayo hayakuweza kuthibitishwa.</li> <li>• Imebainika kwamba malipo yeye jumla ya Sh.578,921,883 yaliyofanywa na Halmashauri hayajaidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri kinyume cha Agizo Na. 8(a) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997.</li> <li>• Ukaguzi wa hesabu za mwisho wa mwaka 2009/2010 umebaini kuwa kiasi cha Sh.528,097,936 zilionekana kwenye daftari la fedha lakini hazikuonekana katika taarifa za benki, kutorekebishwa kwa dosari kunaashiria upotevu wa fedha na kuonesha bakaa zisizo sahihi katika taarifa za fedha.</li> <li>• Halmashauri imelipa jumla ya Sh.144,089,120 bila kuwa na viambatanisho vya kutosha kinyume cha Agizo Na. 8(a) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997. Kukosekana kwa viambatanisho hivyo, uhalali wa malipo hayo hauwezi ukathibitishwa.</li> </ul> |

|  |  |   |
|--|--|---|
|  |  | <ul style="list-style-type: none"> <li>Hasara iliyooneshwa katika taarifa ya mapato na matumizi ni pungufu kwa kiasi cha Sh.125,670,551.</li> <li>Ukaguzi wa hati za malipo pamoja na hati za mishahara ya kila mwezi umebaini kuwa makato ya mishahara Sh.70,545,984 hayajawasilishwa kwenye taasisi husika. Malimbikizo ya makato kwa muda mrefu yanaweza yakasababisha fedha hizo kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa.</li> </ul> |
|--|--|---|

**Orodha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na aina ya hati iliyotolewa kwa miaka miwili ya 2008/2009 na 2009/2010**

| Na                    | Jina La Halmashauri                 | 2008/2009          | 2009/2010          |
|-----------------------|-------------------------------------|--------------------|--------------------|
| <b>Mkoa wa Arusha</b> |                                     |                    |                    |
| 1                     | Halmashauri ya Manispaa Arusha      | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 2                     | Halmashauri ya Wilaya Karatu        | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 3                     | Halmashauri ya Wilaya ya Monduli    | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 4                     | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 5                     | Halmashauri ya Wilaya ya Meru       | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 6                     | Halmashauri ya Wilaya ya Longido    | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 7                     | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa wa Pwani</b>  |                                     |                    |                    |
| 8                     | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo   | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 9                     | Halmashauri ya Wilaya               | Hati yenye         | Hati               |

|                              |                                       |                    |                      |
|------------------------------|---------------------------------------|--------------------|----------------------|
|                              | <b>ya Kibaha</b>                      | <b>shaka</b>       | <b>inayoridhisha</b> |
| 10                           | Halmashauri ya Mji wa Kibaha          | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka     |
| 11                           | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha   |
| 12                           | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia        | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka     |
| 13                           | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka     |
| 14                           | Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji/Utete | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha   |
| <b>Mkoa wa Dar es Salaam</b> |                                       |                    |                      |
| 15                           | Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka     |
| 16                           | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala      | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 17                           | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni  | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 18                           | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka     |
| <b>Mkoa wa Dodoma</b>        |                                       |                    |                      |
| 19                           | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi         | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 20                           | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino     | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka     |
| 21                           | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka     |
| 22                           | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa       | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 23                           | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa       | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 24                           | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa      | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| <b>Mkoa wa Iringa</b>        |                                       |                    |                      |
| 25                           | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa       | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha   |
| 26                           | Halmashauri ya Manispaa ya Iringa     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka     |

|    |                                  |                    |                    |
|----|----------------------------------|--------------------|--------------------|
| 27 | Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa  | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 28 | Halmashauri ya Wilaya ya Makete  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 29 | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 30 | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 31 | Halmashauri ya Mji wa Njombe     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 32 | Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo  | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
|    | <b>Mkoa wa Kagera</b>            |                    |                    |

|                            |   |                    |                    |
|----------------------------|---|--------------------|--------------------|
| 33                         | Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 34                         | Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba         | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 35                         | Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba       | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 36                         | Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe        | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 37                         | Halmashauri ya Wilaya ya Muleba         | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 38                         | Halmashauri ya Wilaya ya Ngara          | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 39                         | Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi       | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 40                         | Halmashauri ya Wilaya Chato             | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Kigoma</b>      |   |                    |                    |
| 41                         | Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu         | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 42                         | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo        | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 43                         | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma         | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 44                         | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/UJiji | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa wa Kilimanjaro</b> |   |                    |                    |
| 45                         | Halmashauri ya Wilaya ya Hai            | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 46                         | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi          | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 47                         | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi        | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 48                         | Halmashauri ya Wilaya ya Siha           | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 49                         | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga         | Hati yenye shaka   | Hati Isiyoridhisha |

|                        |                                     |                    |                    |
|------------------------|-------------------------------------|--------------------|--------------------|
| 50                     | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo      | Hati yenye shaka   | Hati Isiyoridhisha |
| 51                     | Halmashauri ya Wilaya ya Same       | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa wa Lindi</b>   |                                     |                    |                    |
| 52                     | Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa      | Hati inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha |
| 53                     | Halmashauri ya Wilaya ya Lindi      | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 54                     | Halmashauri ya Mji wa Lindi         | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 55                     | Halmashauri ya Wilaya ya Liwale     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 56                     | Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 57                     | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa    | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Manyara</b> |                                     |                    |                    |
| 58                     | Halmashauri ya Wilaya ya Babati     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 59                     | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'    | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 60                     | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 61                     | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu      | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 62                     | Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro  | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 63                     | Halmashauri ya Mji wa Babati        | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Mara</b>    |                                     |                    |                    |
| 64                     | Halmashauri ya Wilaya ya Musoma     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 65                     | Halmashauri ya Wilaya ya Bunda      | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 66                     | Halmashauri ya Manispaa ya Musoma   | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 67                     | Halmashauri ya Wilaya               | Hati               | Hati               |

|                         |                                     |                    |                    |
|-------------------------|-------------------------------------|--------------------|--------------------|
|                         | <b>ya Serengeti</b>                 | inayoridhisha      | inayoridhisha      |
| 68                      | Halmashauri ya Wilaya ya Tarime     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 69                      | Halmashauri ya Wilaya ya Rarya      | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Mbeya</b>    |                                     |                    |                    |
| 70                      | Halmashauri ya Wilaya ya Chunya     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 71                      | Halmashauri ya Wilaya ya Illeje     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 72                      | Halmashauri ya Wilaya ya Kyela      | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 73                      | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali    | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 74                      | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya      | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 75                      | Halmashauri ya Jiji la Mbeya        | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 76                      | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi      | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 77                      | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe     | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa wa Morogoro</b> |                                     |                    |                    |
| 78                      | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero  | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 79                      | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa     | Hati Isiyoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 80                      | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro   | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 81                      | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 82                      | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga     | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 83                      | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero    | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Mtwara</b>   |                                     |                    |                    |
| 84                      | Halmashauri ya Mji wa Masasi        | -                  | Hati yenye shaka   |

|                       |                                     |                    |                    |
|-----------------------|-------------------------------------|--------------------|--------------------|
| 85                    | Halmashauri ya Wilaya ya Masasi     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 86                    | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 87                    | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara   | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 88                    | Halmashauri ya Wilaya ya Newala     | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 89                    | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 90                    | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu   | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa wa Mwanza</b> |                                     |                    |                    |
| 91                    | Halmashauri ya Wilaya ya Geita      | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 92                    | Halmashauri ya Wilaya ya Kwindwa    | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 93                    | Halmashauri ya Wilaya ya Magu       | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 94                    | Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi   | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 95                    | Halmashauri ya Jiji la Mwanza       | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 96                    | Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema  | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 97                    | Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe    | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Rukwa</b>  |                                     |                    |                    |
| 98                    | Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 99                    | Halmashauri ya Mji wa Mpanda        | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 100                   | Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi      | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 101                   | Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 102                   | Halmashauri ya Manispaa ya          | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |

|                          |                                    |                    |                    |
|--------------------------|------------------------------------|--------------------|--------------------|
|                          | Sumbawanga                         |                    |                    |
| <b>Mkoa wa Ruvuma</b>    |                                    |                    |                    |
| 103                      | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga    | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 104                      | Halmashauri ya Manispaa ya Songea  | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 105                      | Halmashauri ya Wilaya ya Songea    | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 106                      | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 107                      | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Shinyanga</b> |                                    |                    |                    |
| 108                      | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 109                      | Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 110                      | Halmashauri ya Wilaya ya Kahama    | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 111                      | Halmashauri ya Wilaya ya Meatu     | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 112                      | Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 113                      | Halmashauri ya Manispaa Shinyanga  | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 114                      | Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu   | Hati inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha |
| 115                      | Halmashauri ya Wilaya ya Maswa     | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| <b>Mkoa Wa Singida</b>   |                                    |                    |                    |
| 116                      | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba    | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 117                      | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 118                      | Halmashauri ya Wilaya ya Singida   | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 119                      | Halmashauri ya Manispaa ya Singida | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |

|                       | <b>Mkoa wa Tanga</b>              |                    |                    |
|-----------------------|-----------------------------------|--------------------|--------------------|
| 120                   | Halmashauri ya Wilaya ya Handeni  | Hati yenye shaka   | Hati inayoridhisha |
| 121                   | Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 122                   | Halmashauri ya Mji wa Korogwe     | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 123                   | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 124                   | Halmashauri ya Wilaya ya Muheza   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 125                   | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 126                   | Halmashauri ya Jiji la Tanga      | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 127                   | Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi  | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 128                   | Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga   | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| <b>Mkoa wa Tabora</b> |                                   |                    |                    |
| 129                   | Halmashauri ya Wilaya ya Igunga   | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 130                   | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega    | Hati inayoridhisha | Hati yenye shaka   |
| 131                   | Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge  | Hati yenye shaka   | Hati yenye shaka   |
| 132                   | Halmashauri ya Wilaya ya Tabora   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 133                   | Halmashauri ya Manispaa ya Tabora | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |
| 134                   | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo   | Hati inayoridhisha | Hati inayoridhisha |



## SURA YA TATU

### 3.0 UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA NA MASUALA YA UDHIBITI WA NDANI

#### 3.1 UTENDAJI WA KIFEDHA

Uhakiki wa Mapato na Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2009/2010 ulibaini masuala mbalimbali kama yalivyoainishwa hapa chini:

##### 3.1.1 Fedha kutoka vyanzo vya ndani (Mapato ya vyanzo vya ndani ukilinganisha na matumizi ya kawaida)

Wakati wa mwaka husika, Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikusanya jumla ya Sh.137,416,106,722 kutoka vyanzo vyao vya ndani na kutumia jumla ya Sh.1,823,788,009,947 katika matumizi ya kawaida. Hata hivyo, ulinganisho kati ya mapato na matumizi ya fedha za Serikali za Mitaa umebaini kuwa Serikali za Mitaa kwa kutumia mapato yake ya ndani zinaweza kugharimia matumizi kwa shughuli za kawaida kwa 7.5% bila kutegemea fedha kutoka serikali kuu na wafadhili. Maelezo ya asilimia kuonyesha uwezo wa Halmashauri umeoneshwa kwenye **Kiambatisho 1.**

Halmashauri yenye asilimia kubwa ya makusanyo ya mapato dhidi ya matumizi ya kawaida ni Halmashauri ya Mji ya Masasi (134%) ikifuatiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (93%).

Kwa wastani, Halmashauri haiwezi kujiendesha kutokana na vyanzo vya mapato yake na hivyo wigo wa mapato ni lazima kupitiwa upya kwa pamoja na vyanzo vya mapato ambavyo bado havijaainishwa.

### **3.1.2 Matumizi Pungufu ya Ruzuku ya kawaida Sh.148,360,934,211**

Mamlaka za Serikali za Mitaa 103 zilitumia kiasi cha Sh.1,373,576,272,098 ukilinganisha na mapato ya Sh.1,521,937,206,309 na hivyo kufanya matumizi pungufu ya Sh.148,360,934,211. Mchanganuo umeoneshwa katika **Kiambatisho 2.**

### **3.1.3 Matumizi ya ziada kuliko mapato Sh.25,354,809,887**

Halmashauri thelathini na moja (31) zilitumia kiasi cha Sh.451,774,320,398 ukilinganisha na mapato ya Sh.426,419,510,511 na hivyo kufanya matumizi ya ziada ya Sh.25,354,809,887. Mchanganuo umeoneshwa katika **Kiambatisho 3.**

### **3.1.4 Ruzuku ya miradi ya maendeleo isiyotumika**

**Sh.175,774,156,104**

Ruzuku ya miradi ya maendeleo hutolewa kwa Halmashauri kwa ajili ya kujenga miundombinu au kufanya ukarabati wa miundo mbinu iliyopo kulingana na maeneo yaliyopewa kipaumbele kwa lengo la kujenga uwezo katika jamii, kuboresha huduma na kupunguza umaskini.

Fedha nyingi hutumika katika maeneo yanayohusu kupunguza umaskini kama vile Afya, Elimu, Maji, Barabara na Kilimo.


Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, kiasi cha Sh.507,866,599,666 kilitolewa katika Halmashauri 133 (isipokuwa Halmashauri ya Mji wa Masasi) ikiwa ni ruzuku ya fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi mbalimbali. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010 kiasi cha Sh.332,092,443,562 kilitumika, na kubakia kiasi cha Sh.175,774,156,104 ya fedha zote zilizotolewa kikihusisha Halmashauri 127. Mchanganuo wa Halmashauri zilizokuwa na fedha za maendeleo zilizobakia imeoneshwa katika **Kiambatisho 4.**

Mapato na Matumizi ya fedha ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa hayakuweza kudhibitishwa kutokana na taarifa ya matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji kwa mwaka wa fedha ulioishia tahere 30 Juni, 2010 haikuwasilishwa ukaguzi.

Muhtasari wa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo za Serikali zisizotumika kwa mwaka 2008/2009 na 2009/2010 ni kama ilivyooneshwa hapa chini:

| Mwaka     | Ruzuku iliyotolewa | Kiasi kilichosalia (Sh.) | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|--------------------|--------------------------|----------------------|
| 2008/2009 | 328,203,178,845    | 88,720,629,195           | 27                   |
| 2009/2010 | 507,866,599,666    | 175,774,156,104          | 35                   |

**Ulinganisho wa maelezo hayo hapo juu yanaweza kuoneshwa kwa kutumia chati mihimili ifuatayo:**



Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ruzuku ya miradi ya maendeleo iliyotolewa kwa Halmashauri ilipungua lakini asilimia ya salio iliongezeka kutoka asilimia 27 hadi 35.

Kuwepo kwa fedha za ruzuku za miradi ya maendeleo isiyotumika ni ushahidi kwamba miradi ya maendeleo ambayo ilitengewa ruzuku hizi haikutekelezwa kama ilivyopangwa. Hii pia inaweza ikasababisha mabadiliko ya bajeti ili kuweza kufidia mapungufu yaliyojitezea kutokana na mfumuko wa bei.


### **3.2 Tathimini ya mifumo ya Udhibiti wa Ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Sehemu hii inaonesha matokeo ya ukagazi kuhusiana na mambo mbalimbali ya udhibiti wa ndani ikiwa ni pamoja na mifumo ya uhasibu, udhibiti wa mazingira ya tathmini ya mchakato hatarishi, menejimenti ya udhibiti wa udanganyifu na ukagazi wa Teknolojia ya Habari (IT) inayolenga udhibiti wa mazingira ya habari katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Tathmini ya udhibiti wa ndani wa Serikali za Mitaa ni sehemu ya ukagazi wa fedha, Udhibiti wa ndani wa Serikali za Mitaa inawezesha Halmashauri kujihakikishia yenyewe kwamba taarifa zake za fedha ni za kuaminika, shughuli zake ni madhubuti na ufanisi wake ni kutekeleza sheria na kanuni, ukagazi wa mfumo na ufanisi wa mazingira ya utawala katika Serikali za Mitaa ni pamoja na mapitio ya udhibiti juu ya mifumo ya fedha hizo na kutoa taarifa kwa ajili ya maandalizi ya taarifa ya hesabu za kila mwaka.

Mfumo wa Udhibiti wa ndani ni kama unaonyeshwa katika mchoro ufuatao:

## Mfumo wa Udhibiti wa ndani



Mfumo wa udhibiti wa ndani unahusisha mambo yafuatayo:

- Udhibiti wa mazingira - kutoa nidhamu ya msingi na udhibiti wa muundo wa utawala bora na majukumu ya uongozi, ufhamu na utendaji kwa wale waliopewa majukumu ya utawala bora.
- Udhibiti wa vihatarishi - Inahusisha kutambua, kuchambua na kuzuia vihatarishi.
- Ufuatiliaji wa udhibiti - Tathmini na ufanisi wa mfumo wa udhibiti wa ndani ulivyo kwa hali ya sasa.
- Udhibiti wa shughuli - ni sera, taratibu na mazoea ya kuwa usimamizi katika kusaidia na kufikia malengo ya Halmashauri.

- Habari na Mawasiliano-inahusisha mawasiliano ya majukumu katika Halmashauri na kudhibiti kutoa taarifa katika sura ya aina na muda ili kuruhusu ofisi kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Yafuatayo ni mapungufu yaliyojitekeza wakati wa kutathmini kazi ya udhibiti wa ndani katika baadhi ya Halmashauri zilizochaguliwa.

### **3.2.1 Mapitio ya Mfumo wa hesabu kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

#### **3.2.1.1 Mfumo fedha jumuishi wa kusimamia ukaguzi**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAO) ikishirikiana na KPMG Tanzania ilifanya ukaguzi kwenye ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kati ya Agosti, 2009 na Juni, 2010.

#### **3.2.1.2 Malengo ya Ukaguzi huo**

Malengo makuu ya zoezi yalikuwa na lengo la kuhakikisha kwamba:

- (i) Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) unasaidiwa ipaswavyo na udhibiti wa jumla na kwa ajili ya kuhakikisha uadilifu, usiri na upatikanaji wa rasilimali ya habari;
- (ii) Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) unaendeshwa kwa ufanisi na inatarajiwu kuwa na ufanisi kama kipimo dhidi ya viwango na vigezo vinavyo kubalika;
- (iii) Rasilimali ya fedha ilivyotumika katika utekelezaji wa mfumo kutokana na ubora na ufanisi zaidi na ili kuendana na Sheria na Kanuni husika.
- (iv) Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) unatosheleza kwa taarifa na mahitaji ya watumiaji mbalimbali wa mfumo ikijumuisha Wizara, Idara, Mawakala na Serikali za Mitaa.

### **3.2.1.3 Matokeo ya tathmini katika Serikali za Mitaa**

Halmashauri 14 kati ya 134 zilihusishwa katika mpango wa tathmini hii yaani:

Halmashauri za Manispaa za Temeke, Ilala, Arusha, Dodoma, Moshi, Iringa; Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Moshi, Magu, Iringa, Mbeya na Meru; na Majiji ya Mbeya na Mwanza.

Mapitio ya mfumo yalibainisha matokeo yafuatayo kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

#### **(a) Masuala ya Thamani ya Fedha**

##### **(i) Ukosefu wa mafunzo kwa watumiaji**

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mafunzo kwa watumiaji wa mfumo funganishi (IFMS) yalifanyika kwa watumishi ambao baadaye walijiunga na mafunzo mengine matokeo yake watumiaji waliobaki hawakuwa na uelewa na mfumo huo. Pia kwa kutokuwa na mafunzo ya mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha, watumishi katika Halmashauri za Iringa na Mbeya hawatumii kompyuta katika kuandaa taarifa kwa mfano, Daftari ya Fedha, Urari, Mizania ya Hesabu na taarifa ya mapato na matumizi. Kwa nyongeza Halmashauri ya Wilaya ya Iringa wana tengeneza Usuruuhisho wa benki kwa njia za kawaida.

##### **(ii) Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha haukutekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru**

Mwezi Julai 2007, Halmashauri ya Wilaya ya Meru ilianzishwa baada ya kugawanya kwa Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru. Hii imesababisha changamoto zifuatazo:

- Inachukua takriban siku 4-5 kutayarisha taarifa ya kila siku na kila mwezi kwa ajili ya Halmashauri.
- Huchukua takriban mwezi mmoja na kufanya marekebisho na kuimarisha wakati kuandaa taarifa za fedha mwishoni mwa mwaka, na
- Mahesabu ya fedha na utoajiwa wa taarifa unafanyika kwa kuandikwa kawaida kwa mkono katika Ofisi ya Waziri Mkuu-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa lakini hakuna maamuzi wa mwisho yaliyofikiwa kuhusu utekelezaji wa mfumo huko.

**(iii) Kutotumika ipaswavyo kwa Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha**

Kazi zifuatazo zilifanyika kwa njia za kawaida kwa kuandikwa kwa mkono ingawa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha unatekelezwa kulingana na mkakati wa Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa.

- Marejesho ya Masurufu kutumia hati ya madai.
- Udhibiti wa mihami na hati ya kuagiza mali.
- Kupokea mali na kuchapisha hundi.
- Usimamizi wa mali.

Kwa kuongezea Halmashauri ya Manispaa Moshi ilikuwa tayari imenunua hundi zilizo kuwa zimechapishwa, lakini zilikuwa kwenye kasha na zilikuwa hazijaanza kutumika. Hata hivyo wanao tegemewa kutumia mfumo huo bado hawajapatiwa mafunzo.

**(iv) Usimamizi usioratibiwa**

Kwa sasa hakuna utaratibu maalum unaotumika kwa ajili ya kuboresha shughuli au matoleo ya mifumo funganifu kwenye Halmashauri. Kwa sababu hiyo, uchambuzi wa vifungu vyta Serikali na Takwimu za Fedha (GFS), kwa ajili ya Chati ya Hesabu (CoA) katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu ambayo inatumia toleo la 7.3.5 vifungu hivyo havijaboreshwu kuendana na toleo jipya. Kwa njia hii watumiaji kwenye serikali za mitaa wanalazimika kutumia njia za kawaida kubadilisha (CoAs) kabla ya kuingiza makisio ya bajeti kwenye leja kuu ili kuhakiki makisio yaliopitishwa ya bajeti ya Halmashaui yao.

- (v) **Kutohuishwa kwa Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa**  
Wakati wa ukaguzi Illobainika kuwepo kwa mgongano wa taarifa zilizotolewa na OWM - TAMISEMI na hali halisi iliyonekana wakati wa ukaguzi. Mfano OWM - TAMISEMI katika taarifa zake ilionesha kwamba Halmashauri ya Ilala ilikuwa inatumia toleo la 7.2 lakini ukaguzi ulibaini kuwa toleo la 7.3.5 ilikuwa likitumika.
- (vi) **Utumiaji wa toleo la EPICOR 7.2 ambao haukidhi matakwa**  
Illobainika kwamba, toleo la Epicor 7.2 ambalo linakadiriwa kutumika katika Halmashauri takribani 42 Tanzania nzima halitumii kikamilifu dhamira ya udhibiti wa vifungu vyta malipo katika bajeti, kinyume na makubaliano ya awali kwa mujibu wa mahitaji ya Serikali ya Tanzania.  
  
Dhamira hii ya udhibiti wa vifungu vyta malipo katika bajeti hakipatikani katika Halmashauri licha ya kwamba hilo ndilo hitaji la Serikali ya Tanzania. Hata hivyo mfumo huu funganifu unatumika katika Serikali Kuu. kwa mapitio ya mkataba wa awali wa mradi, dhamira hii ya udhibiti wa vifungu vyta malipo katika bajeti bado kujumuishwa kwenye toleo husika. Sikuweza kuthibitisha uwepo wa mfumo huo kutokana na kutopatiwa taarifa na mkaguliwa.
- (vii) **EPICOR 7.2 iliyohuishwa na kuwa 7.3.5 haitumiki**  
EPICOR toleo 7.2 liboreshwa katika Halmashauri ya Manispaa Arusha na kuwa 7.3.5 mwezi Agosti 2009 na washauri walioingia mkataba na OWM-TAMISEMI. Hata hivyo, watumiaji bado wanatumia toleo 7.2 kutokana na uhaba wa wafanyakazi waliopatiwa mafunzo juu ya matumizi ya EPICOR 7.3.5.
- (viii) **Gharama za uvezeshaji wa utumiaji wa Epicor 7.3.5 ni kubwa kwa Halmashauri**  
Katika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha, Epicor 7.3.5 iliyoboreshwa na Soft-Tech, lakini Halmashauri waliona

gharama zao ziko juu sana baada ya kuona nukuu ya bei ya Sh.55,000,000 kufanya maboresho na pia nyongeza ya Sh.2,000,000 kwa kila mshiriki wa mafunzo, ukiondoa posho ya kujikimu. Pia kiwango cha chini cha washiriki mafunzo kilipashwa kiwe si chini ya washiriki 5 watumiaji katika Halmashauri hawakupata msaada wa Soft Tech kwa kuwa gharama zao ni kubwa mno. Na kwa sababu hizo Halmashauri imelazimika kutumia washauri wa kujitegemea kwa ajili ya utoaji wa msaada huu.

- (b) **Udhibiti wa matumizi ya Habari na Teknolojia**
- (i) **Mfumo wa Bajeti (PLAN-REP2) hauna mwingiliano na Epicor**  
Hivi sasa, mfumo wa bajeti ulioko kwenye kompyuta (an MS Access database) inatumika kwenye Serikali za Mitaa kwa ajili ya utayarishaji wa bajeti. Hata hivyo uingizaji wa maelezo yaliyoko kwenye mfumo wa bajeti kwenda kwenye Epicor huingizwa kwa mkono kutokana na ukosefu wa mfumo unaoingiliana moja kwa moja. Pia mfumo wa bajeti hauruhusu mtumiaji kuwa na kasma zake nje ya zile zilizopo kwenye mfumo.
- (ii) **Mfumo wa EPICOR kutokubaliana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs)**  
Chati ya hesabu ndani ya Epicor haukidhi matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs). Kwa hiyo, ili kukamilisha majumuisho ya hesabu kwenye Halmashauri, wanalazimika kuandika vitabu kwa mkono. Kwa mfano mfumo wa viwango vya kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma vinataka ushuru wa vyanzo vya ndani vinavyo jumuisha, kodi ya majengo, kodi ya ardhi, kodi ya pango la nyumba za Halmashauri na kodi nyingine za biashara, kwa kuwa mfumo wa Epicor hautambui kasma hizo za mapato ya ndani inalazimika kuandikwa na kufanya marekebisho nje ya mfumo ili kuendana na mfumo wa viwango vya kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma.

- (iii) **Mapungufu katika mgawanyo wa kazi**  
 Katika Halmashauri za Iringa na Mbeya mtu mmoja ana uwezo wa kuingiza na kupitisha hati za malipo, madokezo ya madeni, masurufu na hati za madai na kuidhinisha hati hizo. Katika Halmashauri za Mkoa wa Mwanza, ilionekana Mhasibu wa Wilaya na Karani wana uwezo wa kuingia kwenye mfumo na kuingiza miamala na kuidhinisha hati za malipo.
- (c) **Udhibiti wa ujumla kuhusiana na Mfumo wa Mawasiliano**
- (i) **Rasimu ya Sera ya Usalama wa Mfumo wa Mawasiliano**  
 Kuna sera moja ya mfumo funganifu wa fedha inayotumika katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sera hii ya mfumo funganifu wa fedha bado haijaidhinishwa na mamlaka husika ya Serikali.
- (ii) **Miamala inayotayarishwa na msimamizi wa mfumo**  
 Kuna uwezekano mtumiaji wa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) kuweza kuingiza, kuidhinisha na kurekodi miamala kwa kutumia akaunti ya msimamizi wa mfumo (sa).

| Jina la Mteja  | Jina la Mtumiaji | Tarehe ya kuingiza | Kiasi (Sh.) |
|----------------|------------------|--------------------|-------------|
| DED Mbeya      | sa               | 2/7/2008           | 14,530,650  |
| Upendo Nsalala | sa               | 14/5/2009          | 184,400     |
| Samaria Mshewe | sa               | 14/5/2009          | 420,000     |

Chanzo: Takwimu zilizopatikana kutoka Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

- (iii) **Udhibiti hafifu wa usimamizi wa hifadhidata**  
 Katika kila Halmashauri iliyokaguliwa ilibainika kuwa hifadhidata hazina usimbajifice kwa ajili ya usalama wa hifadhidata na chaguo la kuhifadhi rekodi za matukio na

baadaye kuyakagua yanayohusu usalama wa hifadhidata haukuwezeshwa kufanya kazi katika hifadhidata ya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Zaidi ya hapo ilibainika kuwa msimamizi wa hifadhidata anaweza kurekebisha na kufanya chochote moja kwa moja kwenye taarifa zilizopo kwenye hifadhidata bila kutumia programu ya Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS). Mwisho kabisa, hapakuwa na kumbukumbu zinazoonesha watumishi wa teknolojia ya habari kupewa idhini ya kuingia kwenye seva ya hifadhidata inayotumia kufanya malipo na watumishi wengine.

- (iv) **Hakuna usalama wa mafaili nyeti ya hifadhidata**  
Nilibaini kuwa seva ya hifadhidata inahifadhi data za mifano/sampuli ambazo ni pubs na north wind. Zaidi ya hapo, ilibainika kuwa kumbukumbu na mafaili nyeti ya kuhifadhi nywila katika hali ya maandishi wazi ambazo hujitengeneza wakati wa kufunga mfumo bado hazijaondolewa. Majina ya mafaili yenye kumbukumbu hizo ni sqisp.log na setup.iss.
- (v) **Kukosekana kwa mafunzo kwa watumiaji wa Teknolojia ya mawasiliano**  
Kulikuwa hakuna mafunzo ya mfumo wa mawasiliano kwa watumishi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.
- (vi) **Kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi**  
Watumiaji wakuu wa Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Serikali za Mitaa ni ambao huingiza miamala kwenye mfumo. Hata hivyo hakuna mgawanyo wa kazi ulio huru katika kuhakiki jinsi ya kuingia kwenye mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha.
- (vii) **Kutokuwepo kwa utaratibu mzuri na mafunzo ya kujikinga na majanga**  
Hakuna utaratibu maalum uliowekwa wa kujikinga na majanga endapo kutatokea moto au majanga mengine. Hakuna mafunzo ya utumiaji wa vifaa vya kuzimia moto,

endapo kutajitokeza dharura ya moto. Na kwa nyongeza kulikuwa hakuna alama na maelekezo ya jinsi ya kufanya endapo dharura ya moto itajitokeza.

**(viii) Kutokuwapo nyaraka kwa ajili ya kupima utunzaji kumbukumbu**

Kutokana na wasimamizi wa mifumo, progamu huwa zinabdalishwa na mtumiaji wa mwisho lakini hakukuwa na uthibitisho wa maadishi unaoonyesha kubadilishwa kwa programu hizo.

**(ix) Udfaifu wa kusimamia na kutunza kumbukumbu za akiba**

Hakuna sera au taratibu zilizowekwa katika kuhifadhi kumbukumbu za akiba katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa zilizokaguliwa. Aidha, watumiaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi walikuwa bado kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kuweka kumbukumbu za Epicor. Na hivyo, itakuwa vigumu kurejesha kumbukumbu za akiba kutoka kwenye mfumo endapo majanga yatatokea.

**(x) Mambo mengine yaliobainika kwenye taarifa za baadhi ya Halmashauri**

Masuala mengine ya ukaguzi yaliyobainika wakati ukaguzi wa Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha yalikuwa kama ifuatavyo:

- Idara ya fedha na wafanyakazi wa uhasibu bado hawajapatiwa mafunzo kamilifu ya Epicor.
- Mfumo hautumiki kabisa badala yake kumbukumbu huandaliwa nje ya mfumo kwa kutumia excel, hiyo inatokana na watumishi kutokuwa na ujuzi.
- Taarifa za fedha ziliikuwa mara nyingi zinatayarishwa nje ya mfumo na hundi zinaandikwa kwa mkono.
- Hakuna udhibiti wa vifungu vya matumizi katika mfumo hivyo kusababisha matumizi zaidi katika vifungu.

- Udhibiti wa mali haupo katika mfumo, hivyo usimamizi wa mali unafanyika bila nje ya mfumo na mwisho wa mwaka hati ya marekebisho huingizwa kwenye mfumo kwa ajili ya kuandaa taarifa za fedha.

### **3.2.2 Mfumo wa Uhasibu nje ya Mfumo Funganifu**

Waraka wa fedha Na.1 wa 1999/2000 unataka shughuli zote za Serikali kufanyika kwa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS). Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha una hatua kama kupanga makisio, upatikanaji wa fedha kutoka Serikalini, kibali cha fedha, usimamizi wa mali, manunuzi/miadi na kudhibiti matumizi, malipo ya wadai/Usuluhisho wa benki, matumizi ya fedha za maendeleo, kitabu cha majumu hisho, usimamizi na uandikaji wa taarifa za fedha. Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) unatumia Epicor. Hata hivyo, kinyume na matakwa ya waraka tajwa hapo juu, nilibaini kuwa Halmashauri 50 kama ilivyo kwenye **Kiambatisho 5** kwenye taarifa hii wanaandaa taarifa zao bila kutumia Mfumo Funganifu. Utaratibu huu wa kuandika taarifa siyo wa kuaminika kwa utoaji wa taarifa za uhakika na kwa wakati.

Kwa utaratibu huu, utoaji wa taarifa unakuwa mgumu na hauna udhibiti na pia watu ambao hawausiki wanaweza kufanya mabadiliko kwenye takwimu bila idhini.

- Kutokana na masuala yaliyobainika hapo juu ninashauri kwamba, kuna haja kwa kila Halmashauri kuhakikisha kuwa watumishi walioko katika Idara ya Fedha, wanapatiwa mafunzo ya kutosha kuhusiana na Mfumo wa Epicor.
- Mfumo wa hesabu za Serikali za Mitaa lazima uimarishwe kwa sababu ni muhimu kwa mafanikio na usimamizi wa Halmashauri. Mfumo huu unasaidia kuandaa taarifa za mihamala ya maduhuli, matumizi,

mali na dhima ambazo kwa pamoja zinaandaa taarifa za fedha.

- Mfumo wa hesabu pia unasaidia kutoa taarifa kwa uongozi katika kusaidia kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Udhibiti juu ya Mfumo wa hesabu ni muhimu kwa usimamizi mzuri na katika kuimarisha taarifa za uhakika za fedha.

### **3.2.3 Utendaji wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

Wakati wa ukaguzi wangu kuhusu utendaji wa kazi wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani katika sampuli 122 ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, imebaini kuwa bado kuna mapungufu mengi ya rasilimali watu, fedha, mawanda ya ukaguzi, mbinu za ukaguzi na ubora wa ripoti zao kama inavyoieleza hapa chini pamoja na **Kiambatisho 5**.

- Vitengo vimeendelea kuwa na upungufu wa rasilimali watu na uhaba wa fedha, ukizingatia ukubwa wa shughuli za Serikali za Mitaa, Vitengo vingi vina mtumishi mmoja au wawili ambaeo hawatoshi kwa ukaguzi wa kina wa Mamlaka za Serikali za mitaa.
- Mawanda ya ukaguzi wa ndani kwa mwaka husika umezuiwa kutokana na ukosefu wa fedha na vitendea kazi. Kutokana na mkaguzi wa ndani kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, imeniwia vigumu kutegemea taarifa ya mkaguzi wa ndani katika kujipunguzia mawanda ya ukaguzi.
- Nafasi ya ukaguzi wa ndani katika utawala bora pamoja na majukumu na wajibu wake hayakubainishwa katika wa Mkataba ukaguzi
- Ukosefu wa kumbukumbu zinazoonesha taarifa ya maeneo yaliyokaguliwa ambayo yange wezesha mchakato wa mapitio na kutengeneza msingi wa matokeo ya ukaguzi ambayo yamo katika taarifa ya ukaguzi wa ndani.

Usimamizi wa Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara ya Fedha kuna umuhimu kuimarisha kazi za ukaguzi wa ndani kwa kuongeza fedha na rasilimali watu. Aidha wakaguzi wa ndani lazima wapatiwe elimu na ujuzi ili waweze kuongeza wigo wa ukaguzi na kuboresha utendaji wao.

### **3.2.4 Utendaji wa Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu ni sehemu muhimu ya mchakato wa utawala wa Hamashauri, iliyoundwa na kuimarisha mfumo wa udhibiti wa Halmashauri. Ufanisi Kamati ya Ukaguzi ina uwezo wa kuimarisha mazingira ya udhibiti, na hivyo kusaidia Maafisa Masuhuli kutimiza wajibu wao, uongozi na majukumu ya udhibiti na pia kuwezesha ufanisi wa kazi za ukaguzi wa ndani na kuimarisha utoaji taarifa za fedha. Ingawa majukumu haya yanaeleweka kwa uwazi, nilibaini kuwa utendaji wa Kamati za Ukaguzi wa Halmashauri 116 za Serikali za Mitaa kama inavyoonekana katika **Kiambatisho 5** haukuwa wa ufanisi kutokana na mapungufu yafuatayo:

- Utendaji dhaifu wa Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani unaashiria kwamba Kamati ya Ukaguzi zilishindwa kusimamia majukumu ya wakaguzi wa ndani.
- Kamati za Ukaguzi hazikuwa zinapitia taarifa za fedha na ripoti za Halmashauri.
- Katika baadhi ya matukio hakuna ushahidi kuwa ripoti za Kamati za kila mwaka kuwa zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kuchukua hatua sahihi juu ya mapendekezo ya Kamati.
- Hadidu za Rejea iliyotolewa na OWM-TAMISEMI zilizoainishwa ndani ya Waraka Na. CHA/3/215 ya 27/11/2007 na barua yenye Kumb. Na. CD.10/9/3 ya 24/01/2008 zimeainisha kuwa hakuna ushahidi unaoonesha kuwa katika nyaraka zote mbili (2) kwa Kamati ya Ukaguzi ili kupata ushauri wa kitaalamu kutoka nje ya Halmashauri na kukaribisha wageni wenye

uzoefu kuhudhuria mikutano yake na kutoa ushauri pale inapobidi.

Utendaji usio wa ufanisi wa Kamati ya Ukaguzi unaweza kueneza udhaifu katika udhibiti wa mazingira na utawala bora katika Halmashauri kwa ujumla.

Ni muhimu OWM-TAMISEMI kuongeza majukumu zaidi katika Kamati za Ukaguzi kama vile mapitio ya taarifa za fedha na ripoti, usimamizi wa vihatarishi na usimamizi wa udanganyifu na udhibiti ili kuifanya Kamati kuwa ni chombo imara katika ufuutiliaji wa udhibiti wa ndani.

### 3.2.5 Kuzuia na Kudhibiti Udanganyifu

Viwango vyta Kimataifa vyta Ukaguzi (ISA) 240 inafafanua udanganyifu kama "kitendo cha makusudi kinachofanywa na mtu mmoja au zaidi ndani ya menejimenti, wale wanaohusika na utawala bora, wafanyakazi, au watu wa nje, wakishirikiana kufanya matumizi ya udanganyifu au haramu." Jukumu la msingi kwa ajili ya kuzuia na kutambua udanganyifu hutegemeana na wale wanaoshugulika na uongozi wa wafanyakazi wa Halmashauri na utawala.

Jinsi ya kuzuia Udanganyifu na kudhibiti ni muhimu kwa Serikali za Mitaa na, bila shaka, kwa ngazi nyingine za Serikali na sekta binafsi. Ni moja ya masuala mengi ambayo yanahitaji kusimamiwa kwa ufanisi na kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinafuata kanuni za utawala bora. Lengo la tathmini ya udanganyifu ni kulihakikishia Bunge kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa zina mfumo wa kufaa katika kusaidia kuzuia na kupambana na udanganyifu na kujua sehemu za kufanya maboresha.

Tathmini yangu ya masuala ya udanganyifu katika sampuli 83 za Serikali za Mitaa ilibainika kuwa uongozi wa Halmashauri haukuwa na kumbukumbu za kimaandishi zilizoidhinishwa kuhusu mipango ya kuzuia udanganyifu

kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Hapakuwa na michakato ambayo ilikuwa imewekwa na menejimenti ya Halmashauri kuhusu kubaini kukabiliana na vihatarishi ya udanganyifu katika Halmashauri. Aidha, Uongozi wa Serikali za Mitaa hawana uthibitisho unaoonyesha wazi udhibiti maalum wa kupunguza vihatarishi kutokana na udanganyifu. Aidha, viashiria hatari ambayo ni dalili ya udanganyifu ni kama vifuatavyo:

- Uzembe wa utendaji wa kamati ya Ukaguzi,
- Ufanisi usiuridhisha wa ukaguzi wa Ndani,  
Kukosekana kwa hati za malipo,
- Kuwepo kwa matukio ambayo mapato haya kuwasilishwa benki kwenye akaunti za Halmashauri.
- Hati za Malipo kuwa na nyaraka pungufu,
- Taarifa za hesabu kuwa na makosa.
- Malipo yasiyoidhinishwa.
- Kutokuwepo kwa kamati ya mapokezi na ukaguzi wa mali zilizonunuliwa.
- Ukosefu wa usimamizi wa mali, utunzaji wa kumbukumbu na kufanya tathimini ya mali za kudumu.
- Mishahara ambayo haikulipwa kwa watumishi kutopelekwa Hazina.
- Ukosefu wa udhibiti ili kuhakikisha kuwa mapato yote kutokana na Serikali za Mitaa yalikusanywa na kuwekwa kwenye mfumo wa fedha.
- Kukosekana kwa stakabadhi za kukusanya mapato.

Asili ya viashiria vya udanganyifu vilivyobainisha hapo juu, vinaathiri udhibiti wa ndani na hivyo kuficha udanganyifu unaofanywa na uongozi au wafanyakazi wa ngazi ya chini unaweza kusababisha udanganyifu kutozuiwa na kutogunduliwa na menejimenti ya Halmashauri.

Kwa kuwa wajibu wa kuzuia na kugundua udanganyifu umo ndani ya menejimenti ya Halmashauri, mianya ambayo inaweza kuwa ni chanzo cha udanganyifu na ni lazima kizuiwe pamoja na kuandaa sera za kuzuia ubadhilifu.

Aidha, uongozi unatakiwa kuweka kumbukumbu na kuidhinisha mipango ya kuzuia udanganyifu na kufanya tathimini ya vihatarishi mara kwa mara.

Udhibiti wa udanganyifu ni lazima uunganishwe na majukumu na mipango ya Halmashauri na ionekane kwamba ni jukumu la kila mtu katika Halmashauri. Ni wajibu wa kila mmoja kutambua na kufanya kila awezalo kuzuia na kugundua, kuepuka makosa yasitendeke na mafunzo ya ufahamu yatolewe kwa watumishi.

### **3.2.6 Utaratibu wa Usimamizi wa Vihatarishi**

Usimamizi wa vihatarishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni sehemu ya asili ya mfumo wa udhibiti wa kusimamia utendaji kwa kuwa inahusisha kutambua na kuchambua vihatarishi na kuendelea kupunguza vihatarishi kwa wakati. Kuna haja kwa Halmashauri kuwa utaratibu wa kufuatilia mara kwa mara na kuhuisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ili kuhakikisha kwamba nguzo madhubuti katika kusimamia kazi za Halmashauri na katika kutoa huduma kwa jamii.

Katika sampuli ya Halmashauri 91 zilizokaguliwa imebainika kwamba Halmashauri hizo hazina mifumo ya usimamizi wa vihatarishi na bado hawajafanya upembuzi ili kubaini hatari zilizopo na zile zinazoweza kujitokeza kutokana na mazingira ya kubadilisha mbinu za utoaji huduma na sera ya usimamizi vihatarishi.

Kutokana na ukosefu wa sera na mipango ya usimamizi wa vihatarishi, Halmashauri haziko katika nafasi ya kukabiliana na athari mbaya kwa wakati.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuanzisha mifumo ya usimamizi wa vihatarishi ambayo itasimamiwa mara kwa mara na kuhuishwa ili kuhakikisha kwamba ni nyenzo madhubuti ya michakato ya Halmashauri na taratibu za kutoa huduma kwa jamii. Kamati ya Ukaguzi makini

inaweza kuwa na jukumu muhimu katika kufuutilia na kutathmini menejimenti ya vihatarishi katika Halmashauri. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha ufanisi wa utendaji wa ukaguzi wa ndani.

### **3.3. Utayarishaji wa Taarifa za Fedha**

#### **3.3.1 Utangulizi**

Taarifa za fedha ni muhimu katika kuonesha jinsi gani sekta ya umma, taasisi binafsi na serikali kwa pamoja ukijumuisha ngazi zote za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kufikia malengo ya kutimiza majukumu na wajibu wao kuhusiana usimamizi wa fedha.

Hivi karibuni, mabadiliko yamerahisisha kupunguza muda wa maandalizi ya taarifa za fedha. Mabadiliko hayo ni utumiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha (IFRS), Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) na Takwimu za Serikali katika masuala ya fedha (GFS) kutumika katika maandalizi ya Mpango wa kati wa Matumizi ya Fedha za Umma (MTEF).

Marekebisho ni sehemu ya kutambua mipango ya kimataifa ya kuwepo kwa nia ya kuboresha usimamizi wa fedha na ubora wa taarifa za fedha katika mashirika ya umma na sekta binafsi.

#### **3.3.2 Utumiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma**

Kuna ongezeko la mahitaji ya uwajibikaji na uwazi kwa wadau wote katika Sekta ya Umma katika Tanzania. Maranyingi wakati wa vikao vya Kamati Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) hujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya masuala ya uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha za umma.

Utayarishaji wa taarifa za fedha za uwazi na zinazoleweka ni njia muhimu kwa Serikali za Mitaa katika kuonyesha

uwajibikaji wao kwa wananchi ambao ndiyo walipa kodi na pia kama washirika wa maendeleo ambao mara nyingi wanachangia shughuli za maendeleo ya Serikali za Mitaa. Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs) ni ya ubora wa hali ya juu katika kukidhi mahitaji ya taarifa za fedha Kwa Sekta ya Umma. IPSASs zinatolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Uhasibu kwa Sekta za Umma (IPSASB), ambayo ni tawi la Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC).

Kipindi cha mpito kwenda IPSASs ni mfumo wa uhasibu uliyoundwa na kuongeza ubora na mtiririko ya utoaji taarifa za fedha, kuongeza uwazi na uwajibikaji, kuwezesha maamuzi bora na usimamizi wa fedha na utawala bora katika sekta ya umma kwa ujumla wake.

### **3.3.3 Changamoto**

Kufanikiwa kwa utumiaji wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kunategemea jitihada za wadau mbalimbali ambao wanasaidia kwa hali na mali ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na utayarishaji taarifa za fedha katika sekta ya Umma.

Sambamba na hilo hapo juu, ni ukweli usiofichika kwamba Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa mwaka 2000) na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya (LAFM) ya mwaka 1997 ambazo kwa wakati huu zinatumika kama nyaraka muhimu katika maandalizi ya taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitaji wala kuelezea IPSASs kama ni viwango vya kufuatwa katika utayarishaji wa taarifa za fedha za Halmashauri. Kwahiyoo, utaratibu mpya wa Kisheria utahitaji kuandaliwa ambao utaelezea IPSASs kama msingi wa uandaaji wa taarifa za fedha za Halmashauri.

Baada ya kuridhia na kuanza kutumia IPSASs kama Mfumo wa Menejimenti ya Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mfumo huu unatakiwa kuhuishwa ili kuendana na mahitaji na matakwa ya viwango hivyo vya uhasibu. Mfumo Funganifu wa Udhhibit wa Fedha (IFMS) unaotumika hivi sasa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu katika masuala ya udhibiti wa fedha unatakiwa kufanyiwa tathmini baada ya kuridhia kutumika kwa IPSASs. Vile vile, kujenga uwezo kwa watumiaji wa viwango hivi kunahitajika ili kusiwe na kikwazo katika matumizi ya IPSASs.

Kutumia viwango vipyta vya utayarishaji wa taarifa za fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kunaashiria mabadiliko makubwa katika mfumo na jinsi ya utayarishaji wa hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mabadiliko haya yanakuja na mahitaji mapya ya miundo na vielezo katika utayarishaji wa taarifa za fedha. Hii itawalazimu wahasibu na watumishi wengine wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukubali mabadiliko na kuacha utaratibu uliozoeleka wa utayarishaji wa taarifa mbalimbali.

Ninatambua kuwepo kwa jitihada na maendeleo katika matumizi ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kwa mfano OWM-TAMISEMI imetoa Waraka wenyewe Kumb. Na.CA:26/307/01A/79 wa tarehe 28 Septemba, 2009 ukizitaka Mamlaka za Serikali za Mitaa kutayarisha taarifa zao za fedha kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs). Vile vile, TAMISEMI walitayarisha mwongozo na vielelezo vitakavyotumika na Mamlaka za Serikali za Mitaa 134 katika utayarishaji wa taarifa zao za fedha.

Wadau katika juhudhi hizi mpya za mabadiliko katika Sekta ya Umma wanatakiwa kuongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Uchumi, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Washirika wa Maendeleo na Serikali kwa

ujumla. Pia ni muhimu kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kutoa maoni ya Mkaguzi katika taratibu na mchakato wa utumiaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAsSs).

### **3.3.4 Uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

#### **3.3.4.1. Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha**

Agizo Na.82 na 88 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka wa 1997 pamoja na Kifungu Na.45(4) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa na ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000), inawataka Maafisa Masuuli kuandaa taarifa za fedha za mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi kabla au tarehe 30 Septemba ya kila mwaka wa fedha.

Kati ya Halmashauri 134, Halmashauri 8 zilichelewa kuwasilisha taarifa za fedha ndani ya tarehe ya kisheria (30 Septemba, 2010) kwa kipindi cha kati ya siku 7 hadi 60 kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

| Na | Jina la Halmashauri                 | Tarehe ya kuwasilisha taarifa za fedha | Muda aliochelewesha |
|----|-------------------------------------|--|---------------------|
| 1. | Halmashauri ya Wilaya ya Babati     | 29 Novemba, 2010                       | 60                  |
| 2. | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino   | 7 Oktoba, 2010                         | 7                   |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Temeke     | 7 Oktoba, 2010                         | 7                   |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa     | 17 Novemba, 2010                       | 48                  |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa     | 7 Oktoba, 2010                         | 7                   |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara     | 15 Oktoba, 2010                        | 15                  |
| 7. | Halmashauri ya Mji wa Babati        | 22 Novemba, 2010                       | 52                  |
| 8. | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | 18 Oktoba, 2010                        | 18                  |

Kati ya Halmashauri nane (8) zilizotajwa hapo juu, Halmashauri mbili walirekebisha taarifa za fedha na kuziwasilisha tena baada ya kufanya marekebisho kama inavyoonesha hapa chini:

| Na. | Jina la Halmashauri                 | Tarehe ya kuwasilisha Taarifa za fedha | Tarehe ya Kuwasilisha taarifa zilizorekebishwa |
|-----|-------------------------------------|--|--|
| 1.  | Halmashauri ya Mji wa Babati        | 22 Novemba, 2010                       | 30 Disemba,,2010                               |
| 2.  | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | 18 Oktoba, 2010                        | 2 Disemba, 2010                                |

Aidha, Halmashauri 43 ziliwasilisha taarifa za fedha ndani ya muda wa kisheria, lakini kutokana na taarifa hizo kutokuwa sahihi walirejeshewa ili kufanya marekebisho, na kuletwa kwa mara ya pili baada ya marekebisho kati ya tarehe 7 Oktoba, 2010 na 2 Februari, 2011 kama inavyoonesha katika jedwali hapa chini:

| Na. | Jina la Halmashauri                | Tarehe ya kuwasilisha Taarifa za fedha | Tarehe ya kuwasilisha taarifa za fedha zilizorekebishwa |
|-----|------------------------------------|--|---|
| 1.  | Halmashauri ya Manispaa ya Singida | 28 Septemba, 2010                      | 31 Disemba, 2010  |
| 2.  | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo    | 27 Septemba, 2010                      | 1 Disemba, 2010   |
| 3.  | Halmashauri ya Mji wa Njombe       | 27 septemba, 2010                      | 7 Oktoba, 2010  |
| 4.  | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru   | 29 Septemba, 2010                      | 15 Oktoba, 2010   |
| 5.  | Halmashauri ya Manispaa ya Arusha  | 30 Septemba, 2010                      | 22 Januari, 2011  |
| 6.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto    | 28 Septemba, 2010                      | 14 Disemba, 2010  |

|     |   |                   |                  |
|-----|---|-------------------|------------------|
| 7.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa        | 27 Septemba,2010  | 7 Oktoba, 2010   |
| 8.  | Halmashauri ya Wilaya ya Newala         | 29 Septemba,2010  | 7 Disemba, 2010  |
| 9.  | Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe        | 29 Septemba,2010  | 11 Januari, 2011 |
| 10. | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/UJiji | 30 Septemba,2010  | 30 Disemba, 2010 |
| 11. | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi        | 27 Septemba,2010  | 7 Oktoba,2010    |
| 12. | Halmashauri ya Wilaya ya Iramba         | 27 Septemba,2010  | 1 Disemba, 2010  |
| 13. | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma         | 29 Septemba,2010  | 28 Disemba, 2010 |
| 14. | Halmashauri ya Wilaya ya Meatu          | 30 Septemba,2010  | 11 Disemba, 2010 |
| 15. | Halmashauri ya Wilaya ya Muleba         | 14 Septemba,2010  | 11 Disemba, 2010 |
| 16. | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero        | 29 Septemba,2010  | 11 Disemba, 2010 |
| 17. | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo       | 30 Septemba, 2010 | 15 Oktoba,2010   |
| 18. | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo          | 30 Septemba, 2010 | 29 Januari, 2011 |
| 19. | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro       | 30 Septemba, 2010 | 10 Disemba, 2010 |
| 20. | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo        | 29 Septemba, 2010 | 31 Disemba, 2010 |
| 21. | Halmashauri ya Wilaya ya Songea         | 28 Septemba, 2010 | 10 Oktoba, 2010  |
| 22. | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi           | 30 Septemba, 2010 | 15 Oktoba, 2010  |

|     |                                    |                   |                  |
|-----|------------------------------------|-------------------|------------------|
| 23. | Halmashauri ya Wilaya ya Singida   | 30 Septemba, 2010 | 1 Disemba, 2010  |
| 24. | Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge   | 30 Septemba, 2010 | 31 Disemba, 2010 |
| 25. | Halmashauri ya Wilaya ya Igunga    | 30 Septemba, 2010 | 14 Disemba, 2010 |
| 26. | Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu    | 30 Septemba, 2010 | 30 Disemba, 2010 |
| 27. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero | 28 Septemba, 2010 | 2 Disemba, 2010  |
| 28. | Halmashauri ya Wilaya ya Tabora    | 30 Septemba, 2010 | 17 Januari, 2011 |
| 29. | Halmashauri ya Wilaya ya Longido   | 28 Septemba, 2010 | 20 Januari, 2011 |
| 30. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga    | 30 Septemba, 2010 | 15 Oktoba, 2010  |
| 31. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu     | 28 Septemba, 2010 | 8 Disemba, 2010  |
| 32. | Halmashauri ya Wilaya ya Meru      | 30 Septemba, 2010 | 7 Januari, 2011  |
| 33. | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi   | 29 Septemba, 2010 | 30 Januari, 2011 |
| 34. | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma  | 14 Septemba, 2010 | 1 Disemba, 2010  |
| 35. | Halmashauri ya Wilaya ya Hai       | 30 Septemba, 2010 | 9 Januari, 2011  |
| 36. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarari   | 30 Septemba, 2010 | 11 Januari, 2011 |
| 37. | Halmashauri ya Manispaa ya Tabora  | 30 Septemba, 2010 | 1 Disemba, 2010  |
| 38. | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha    | 30 Septemba, 2010 | 15 Januari, 2011 |
| 39. | Halmashauri ya                     | 28 Septemba, 2010 | 20 Disemba, 2010 |

|     |                                    |                   |                  |
|-----|------------------------------------|-------------------|------------------|
|     | Wilaya ya Nzega                    |                   |                  |
| 40. | Halmashauri ya Wilaya ya Siha      | 30 Septemba, 2010 | 9 Januari, 2011  |
| 41. | Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro | 18 Septemba, 2010 | 17 Disemba, 2010 |
| 42. | Halmashauri ya Manispaa ya Songea  | 30 Septemba, 2010 | 12 Oktoba, 2010  |
| 43. | Halmashauri ya Wilaya ya Lindi     | 27 Septemba, 2010 | 1 Disemba, 2010  |
| 44. | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi     | 30 Septemba, 2010 | 2 Februari, 2011 |

Wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha zilizowasilishwa, nilibaini kuwa kulikuwa na idadi ya Halmashauri ambazo ziliwasilisha taarifa za fedha zenye makosa mengi ambazo ziliikuwa zimeletwa ili kuonekana zimewasilishwa kukidhi tarehe ya kuwasilishwa kisheria kwa ukaguzi.

Ukaguzi wa taarifa hizo za fedha zilionyesha kuwepo kwa mapungufu na yalihitajika marekebisho kwenye taarifa za Hesabu na kulazimika kuwarudishia ili wazirekebishe, na baadae ziliwasilishwa tena baada ya marekebisho.

Idadi ya Halmashauri ambazo zilirokebisha taarifa zake za fedha na kuwasilisha tena kwa ukaguzi zimeongezeka kutoka 24 mwaka 2008/2009 hadi kufikia 44 kwia mwaka (2009/2010). Mtiririko kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:

#### **Mtiririko wa taarifa za hesabu zilizorekebushwa kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Halmashauri zilizokaguliwa | Idadi ya Halmashauri zilizo Rekebisha | Asilimia |
|----------------|-------------------------------------|---------------------------------------|----------|
| 2007/2008      | 133                                 | 15                                    | 11       |
| 2008/2009      | 133                                 | 24                                    | 18       |
| 2009/2010      | 134                                 | 44                                    | 33       |

Mchanganuo huo hapo juu unaweza kuonyeshwa kwenye chati mihimili kama ifuatavyo:



Mtiririko hapo juu unaonyesha kuwa kuna ongezeko la taratibu katika idadi ya Halmashauri zilizofanya marekebisho ya taarifa za fedha. Kwa kiasi kikubwa hii imesababishwa na ukosefu wa mafunzo ya kutosha juu ya maandalizi ya taarifa kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAs) pia na uhamisho wa wafanyakazi ambao walipatiwa mafunzo ya IPSAs.

Inashauriwa kwamba, katika miaka ya baadaye, Halmashauri zinapaswa kuanzisha uhakiki wa ubora na kuwe na utaratibu kwa ajili ya maandalizi ya taarifa za fedha ili kuhakikisha usahihi wa taarifa hizo. Aidha, OWM-TAMISEMI inatakiwa kuendesha mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea uwezo wafanyakazi katika maandalizi ya taarifa za fedha.

#### **3.3.4.2 Ukaguzi wa taarifa za fedha**

Kwa ujumla, ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2009/2010 umebaini mapungufu yafuatayo katika utayarishaji wa taarifa za fedha:

**(a) Kufuata Viwango vilivyokubalika katika utayarishaji wa taarifa za fedha**

Taarifa za fedha za mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 zilizowasilishwa kwa ukaguzi na Mamlaka zote 134 za Serikali za Mitaa zimetayarishwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAsSs) na sehemu ya IV ya Sheria Na. 9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Agizo Na.53 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 ambayo ndiyo miongozo inayotumika.

Hata hivyo miongozo hiyo, yaani Sheria Na. 9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 (iliyorekebishwa 2000) na Agizo Na.53 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 pamoja na Sheria nyinginezo za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepitwa na wakati hivyo haziendani na mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAsSs).

Ninapendekeza Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya 1982 pamoja na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997, Mwongozo wa Uhasibu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1993 na Sheria nyingine zifanyiwe mapitio na marekebisho ili ziweze kukidhi mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAsSs).

**(b) Uwasilishaji wa taarifa za fedha usio sahihi**

Taarifa za fedha za Halmashauri tatu (3) zilizowasilishwa zilikuwa na makosa ya kimsingi hivyo kupotosha usahihi wa taarifa hizi kama ifuatavyo:

| Halmashauri                     | Mapungufu  |
|---------------------------------|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo | Taarifa za mizania ya hesabu za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo za mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 zimeonyesha salio la wadai jumla ya Sh.660,599,974. Hata hivyo, ukaguzi umegundua kuwa hapakuwa na mchanganuo kuonyesha madai ya muda mfupi na yale ya muda mrefu.  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa  | Halmashauri haikuandaa taarifa ya matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kukosekana kwa taarifa hiyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha vyanzo vya fedha, miradi ya maendeleo iliyotekelizwa, bajeti iliyopangwa, salio anzia, kiasi cha fedha kilichopokelewa, kiasi kilichotumika na salio ishia. |
| Halmashauri ya Mji wa Lindi     | Taarifa ya mapato na matumizi za Halmashauri ya Mji wa Kilwa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 imeonesha fedha za maendeleo kutoka Serikali Kuu Sh.1,911,447,792 kama fedha za matumizi ya kawaida na kusababisha upungufu wa fedha za maendeleo kwa kiasi hicho hicho.  |

Inaweza kuhitimishwa kuwa, Halmashauri zinatakiwa kutayarisha taarifa zake za fedha kulingana na viwango vya kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma na kuimarisha kitengo cha uhakiki wa ubora katika kuitopia taarifa za hesabu kabla ya kusainiwa.

**(c) Makosa yaliyori potiwa katika taarifa za fedha**

Tarakimu zilizoripotiwa katika taarifa nyingi za fedha zilizowasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama taarifa za mizania, mapato na matumizi, taarifa ya mtiririko wa fedha, taarifa ya kuhusu mabadiliko ya mtaji, taarifa za matumizi ya miradi ya maendeleo na ugharimiaji hazikuwa sahihi kama inavyooneshwa katika Kiambatisho 6.

Katika hali hiyo, taarifa hizi za fedha zimeonekana haziwezi kutegemewa na watumiaji.

Kutokana na kuonekana na dosari nyingi katika taarifa za fedha ukilinganisha na mwaka uliopita, inaashiria kuwa menejimenti husika hazikuwa makini katika kuandaa taarifa hizo hivyo kusababisha kutolewa kwa hati za ukaguzi nyingine tofauti na hati inayoridhisha.

**(d) Kuonyesha mali bila thamani**

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri sita (6) umeonyesha kuwepo kwa majedwali ya mali za kudumu bila kuonyesha thamani zake. Dosari hii inasababisha kuwe na upungufu wa thamani za mali zilizoonyeshwa katika taarifa za fedha zilizowasilishwa kama ifuatavyo:

| Halmashauri                       | Dosari zilizoonekana  |
|-----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Jiji la D'salaam   | Jumla ya mali, mitambo na vifaa 53 vimeoneshwa katika taarifa za fedha bila kuonesha thamani kinyume cha mahitaji ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma IPSASs 17 inayohitaji kuonesha thamani yake na ujumla uchakavu. |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara   | Jumla ya sekondari 18 zilizokabidhiwa kwa Halmashauri toka Wizara ya Elimu zimeoneshwa katika taarifa za fedha bila thamani.  |
| Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | Mali za kudumu za Halmashauri kama magari, kompyuta na kamera vilivyooneshwa katika taarifa za fedha havikuthaminishwa.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Newala   | Mali za kudumu zilizothaminishwa kutokana na ripoti ya mwezi Mei, 2010 hazikuoneshwa kwenye taarifa ya fedha.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu | Mali, Vifaa na Mitambo zilizokuwa mali ya Wizara ya Elimu na Ufundu hapo mwanzo zimekabidhiwa kwa Halmashauri na kuoneshwa katika taarifa ya fedha bila thamani.  |

|                                   |   |
|-----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Manispaa ya Tabora | Taarifa ya mizania ya hesabu imeonyesha mali, vifaa na mitambo zenyenye thamani ya Sh.10,293,265,180 lakini haikujumuisha magari manne, na vifaa vya ofisini ambavyo havikuthaminishwa. |
|-----------------------------------|---|

Kuwasilisha na kutoa taarifa ya mali bila thamani zake inapunguza thamani za mali zilizoonyeshwa katika taarifa ya fedha na haionyeshi hali halisi ya mali za Halmashauri. Halmashauri zinashauriwa kuthaminisha mali zote ili kuandaa taarifa za fedha kwa usahihi.

**(e) Kutoonyeshwa kwa mali za kudumu katika taarifa za fedha**

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha wa mwaka 2009/2010 nimegundua kuwa Halmashauri 9 hazikuonyesha mali za kudumu na pia rejesta ya mali za kudumu haijaandikwa kikamilifu kama ilivyoonyeshwa hapa chini:

| Halmashauri                       | Dosari zilizoonekana   |
|-----------------------------------|--|
| Halmashauri ya Manispaa ya Temeke | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri inamili ki na kutumia programu ya utunzaji wa takwimu za hesabu LGMP, PLANREP, USP, MOLIS, Epicor, MRECOM na GIS lakini hazijaonyeshwa katika taarifa ya fedha ya Halmashauri kinyume cha Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma IPSASs 31.</li> <li>• Ardhi na sehemu za wazi zinazomilikiwa na Halmashauri hazikuonyeshwa kwenye taarifa za fedha kinyume cha viwango vya kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma IPSASs 17 kifungu 74.</li> </ul> |

|                                 |  |
|---------------------------------|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo | Taarifa ya mizania ya hesabu inaonyesha kiasi cha Sh.6,869,600 ikiwa ni gharama za bidhaa gharani vya Halmashauri vilivyopo makao makuu lakini havikuonyeshwa wakati wa kuhesabu vitu hivyo kinyume na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma IPSASs, 12 vinavyohitaji taasisi kuonyesha bidhaa zilizoko nje ya kituo.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu | Halmashauri inamiliki programu ya utunzaji wa takwimu za hesabu (EPICOR computer software) lakini thamani yake haikuonyeshwa kwenye taarifa ya mizania ya hesabu.  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa  | Mali zenyet thamani ya Sh.251,724,000 zimeonyeshwa kwenye orodha ya kuhesabia mali lakini mali hizo hazikuonyeshwa kwenye taarifa ya fedha ya mwaka inayoishia terehe 30 Juni, 2010.   |
| Halmashauri ya Mji wa Lindi     | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri imefunga na inatumia programu za kompyuta ambazo zimetakiwa zitambulike kama mali isiyoshikika, hazikuonyeshwa kwenye rejestra ya mali za kudumu na kwenye taarifa za fedha. Programu hizi ni pamoja na PLANREP na Epicor.</li> <li>• Pikipiki aina ya XL-Yamaha yenyenamba ya usajili SM 3246 haikuoneshwakwenye rejestra ya vifaa na hata kwenye taarifa ya hesabu na thamani yake haijulikani.</li> <li>• Mali za kudumu zenyet thamani ya Sh.17,678,756 hazikuoneshwakwenye taarifa za fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 japo Halmashauri inazimili na kuzitumia mali hizo.</li> </ul> |

|                                   |   |
|-----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga   | Miradi ambayo imetekelizwa kwa kiwango chini ya asilimia 50 yenye thamani ya Sh.67,537,675 hazikuoneshwa kama kazi zinazoendelea.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Kazi zinazoendelea zenyne thamani ya Sh.193,606,222 ambazo zimefikia kiwango cha asilimia 50 hazikuonyeshwa kama mali kwenye mizania ya hesabu.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge  | Kielekezi cha taarifa za fedha Na.28 kimeonyesha mali za kudumu kama majengo, shule na vifaa vyatofisini vinavyomilikiwa na Halmashauri lakini havikuthaminishwa na kuonyeshwa kwenye mizania ya hesabu.            |
| Halmashauri ya Wilaya ya Urambo   | Mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha unaotumia Epicor kuanzia mwaka 2005 kupitia programu ya maboresho, thamani yake hajatambuliwa na kuonyeshwa kwenye mizania ya fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. |

Menejimenti za Halmashauri zinashauriwa kutunza kumbukumbu za mali za kudumu ikiwa pamoja na mali isiyoshikika na kuhakikisha kuwa rejestra ya mali inatunzwa kama msingi wa kuandaa taarifa za fedha zisizo na dosari.

**(f) Kutokuwepo kwa Vielekezi vya Taarifa za fedha/ Jedwali lenye maelezo ya kina**

Katika ukaguzi wa taarifa za fedha kwa mwaka husika tulibaini kuwa tarakimu mbalimbali zilizoingizwa katika hesabu za Halmashauri mbalimbali zilikuwa zinakinzana na tarakimu zilizoonyeshwa katika Vielekezi vya Taarifa za fedha na mapungufu mbalimbali yalibainika kama inavyooneshwa hapo katika jedwali hapo chini:

| <b>Halmashauri</b>                 | <b>Mapungufu yaliyojitekeza</b>  |
|------------------------------------|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Rombo     | Taarifa ya Mtiririko wa fedha iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi haikuwa na vielekezi vytaarifa za fedha kuthibitisha tarakimu ziliyoainishwa katika taarifa hiyo. Kwa kutokuwa na vielekezi vytaarifa za fedha, ni kinyume na Agizo Na.85 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997). |
| Halmashauri ya Wilaya Kilwa        | Kiasi cha Sh.10,597,761,876 kilichoonyeshwa katika kielekezi cha Taarifa za fedha hakikuambatanishwa na jedwali lenye maelekezo ya kina.   |
| Halmashauri ya Manispaa Sumbawanga | Kielekezi cha Taarifa za fedha Na. 39 kinachoonyesha bakaa ya ruzuku ya miradi ya maendeleo ya Sh.6,880,172,568 katika mizania ya fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 hakikuambatanishwa na taarifa za fedha.  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe   | Kiasi cha Sh.363,656,341 kilichooneshwakatika taarifa za Mapato na Matumizi ikiwanifedha zilizohamishiwa kutoka katikataasisi mbalimbali za Serikali hazikuwa na Kielekezi cha Taarifa za fedha.   |
| Halmashauri ya Mji wa Korogwe      | Mizania ya fedha kwa mwaka ulioishiatarehe 30 Juni, 2010 hazikuwa na vielekezi vytaarifa za fedha kinyume na Viwango vyakimataifa vyauhasibu kwa sekta ya umma IPSASs 1.   |

Agizo Na.85 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) na viwango vyakimataifa vyauhasibu kwa sekta ya umma Na.1 kwa pamoja zinaagiza kuwa taarifa za

fedha zinatakiwa ziambatanishwe na vielekezi nya taarifa za fedha ambavyo vinasaidia kuongeza uelewa wa taarifa zilizowasilishwa kwa watumiaji wa taarifa hizo. Kwa hiyo Halmashauri zote zinasisitizwa kuandaa vielekezi nya taarifa za fedha ili kuthibitisha tarakimu katika vifungu mbalimbali zilizoainishwa katika taarifa za fedha.

**(g) Kutoainishwa kwa michango ya jamii katika taarifa za fedha**

Katika ukaguzi uliofanyika kuhusiana na michango ya kijamii kwenye Vijiji na Kata imebainika kwamba, Halmashauri kumi na tano (15) zilizoainishwa katika jedwali hapo chini hazikuweza kuthaminisha michango ya wananchi kupitia nguvu zao au hazikuweza kuainisha kwenye taarifa za fedha michango ya wananchi kupitia nguvu zao katika miradi mbalimbali ya Maendeleo, kinyume na kifungu Na.127 na Na. 22(107) nya Viwango nya kimataifa nya uhasibu kwa Sekta ya Umma IPSAs. Baadhi ya Halmashauri hazikuweza kuanisha michango inayotokana na nguvu za wananchi ingawaje taarifa hizo zimeoneshwa katika taarifa za Madiwani zilizopo katika taarifa za fedha za Halmashauri husika.

| Halmashauri                       | Mapungufu   |
|-----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Manispaa ya Iringa | Halmashauri imechangia kiasi cha Sh.254,688,293 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbali mbali ya maendeleo katika Kata na Vijiji lakini haikuweza kuthaminisha michango ya nguvu za wananchi iliyotumika katika miradi husika. |
| Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa   | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali iliyotekeliza haikuweza kuthaminishwa ili kujua ni kiasi gani cha fedha kimechangiwa na Wananchi katika miradi hiyo.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo   | Halmashauri imechangia kiasi cha Sh.49,384,944 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Kata na Vijiji lakini haikuweza kuthaminishwa na kuoneshwa katika taarifa za fedha.                            |

|                                   |   |
|-----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba   | Michango ya nguvu za wananchi haikuweza kuthaminishwa na kuoneshwa katika taarifa za fedha. Kwa kutofanya hivyo imekuwa vigumu kuthibitisha michango ya wananchi katika kukamilisha miradi mbalimbali.                                      |
| Halmashauri ya Wilaya ya Chato    | Uongozi wa Halmashauri haukuweza kuthaminisha michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali ya maendeleo iliyotekelizwa.   |
| Halmashauri ya Manispaa ya Moshi  | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali ya maendeleo kama ilivyooneshwa katika kielekezi Na.17(b) katika taarifa ya Madiwani lakini michango hiyo ya wananchi haikuweza kuthaminishwa na kuonyeshwa katika taarifa za fedha. |
| Halmashauri ya Wilaya ya Chunya   | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali iliyotekelizwa haikuweza kuthaminishwa na kuoneshwa katika taarifa za fedha.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga   | Kulingana na kielekezi Na. 17 katika taarifa ya Madiwani imebainika kuwa wananchi walishiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo lakini michango yao haikuweza kuthaminishwa na kuonyeshwa katika taarifa za fedha.       |
| Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru  | Taarifa ya madiwani imeainisha kuwa michango ya wananchi ambao walishiriki katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo lakini haikuweza kuthaminishwa na kuingizwa katika taarifa za fedha kwa mwaka husika.                       |
| Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali iliyotekelizwa haikuweza kuthaminishwa kinyume na Aya 22.107 (d) ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAsSs).   |

|                                  |   |
|----------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali iliyotekelizwa haikuweza kuthaminishwa na uongozi wa Halmashauri, kinyume na Aya 22.107(d) na 22.127 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAWs).          |
| Halmashauri ya Mji wa Korogwe    | Michango ya nguvu za wananchi katika miradi mbalimbali iliyotekelizwa haikuweza kuthaminishwa na uongozi wa Halmashauri kinyume na Aya 22.107(d) na 22.127 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSAWs).           |
| Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge | Kulingana na kielekezi Na. 17 katika taarifa ya Madiwani imebainika kuwa wananchi walishiriki katika utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo lakini mchango wao haukuweza kuthaminishwa na kuonyeshwa katika taarifa za fedha. |

Kwa kuwa nguvu za wananchi zinaonesha hali halisi ya thamani ya mali, zinapaswa kuthaminishwa na kuoneshwa katika taarifa za fedha.

**(h) Kutooneshwa kwa usahihi wa vipengele katika taarifa za fedha**

Taarifa muhimu kwa watumiaji katika Halmashauri thelathini na mbili (32) hazikuoneshwa kwenye taarifa za fedha kama inavyotakiwa. Tazama jedwali hapo chini:

| Halmashauri                          | Taarifa ambazo siyo sahihi   |
|--------------------------------------|--|
| Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Jiji la Dar es Salaam limeshindwa kutambua thamani ya sasa ya hisa 3,631,046 zinazomilikiwa katika Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam (UDA) ambazo zilinunuliwa mwezi Oktoba, 2000 kwa Sh.363,104,600.</li> <li>• Taarifa za fedha za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 zimeonesha uwekezaji wa hisa</li> </ul> |

|                                   |  |
|-----------------------------------|--|
|                                   | <p>zenye thamani ya Sh.821,369,000 bila kuwa na kiambatanisho kinachoonesha idadi ya hisa inazomiliki.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Halmashauri ya Jiji imenunua hisa 240 zenyet thamani ya Sh.24,000,000 sawa na asilimia 51 katika Shirika la Soko la Kariakoo lakini hapakuwa na hati ya umilikaji wa hisa hizo.</li> <li>• Jiji lilipata mkopo wa Sh.1,269,792,000 kutoka Mfuko wa Huduma za Jamii (NSSF) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili “Business Park Complex”. Hata hivyo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam haikuonesha mkopo huo katika kielekezi cha taarifa za fedha kama matakwa ya Agizo Na.81 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) inavyoelekeza. Pia mkataba kati ya Halmashauri la Jiji la Dar es Salaam na Mfuko wa Huduma za Jamii (NSSF) haukuweza kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.</li> </ul> |
| Halmashauri ya Manispaa ya Temeke | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Katika kupitia taarifa ya mtiririko wa fedha imebainika kuwa kiasi cha Sh.4,216,451,684 kimeoneshwa kuwa kimepokelewa kama ruzuku ya miradi ya maendeleo hata hivyo, hati za kupokelea hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi kuthibitisha kama fedha hizo zimepokelewa na Halmashauri.</li> <li>• Aina mbalimbali ya Mali, Mitambo na Vifaa hazikuweza kutenganishwa katika Mizania ya Hesabu kinyume na Aya 17.88 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs).</li> </ul>  |

|                                 |   |
|---------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Njombe | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kielekezi cha taarifa za fedha Na.27 kinachohusu Mali, Mitambo na Vifaa kimeelekeza kuwa Halmashauri ilifanya tathimini ya mali zake kama vile majengo, mitambo, mashine na vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh.41,518,389,000. Hata hivyo, Halmashauri haikuweza kuthibitisha kama tathimini ilifanywa na Mthamini aliyethibitishwa kwa kazi hiyo.</li> <li>• Vifaa ghalani viliyobaki mwishoni mwa mwaka katika vituo mbalimbali kama vile kwenye mashule, zahanati na kwenye ofisi mbalimbali havikuweza kuoneshwa kwenye Mizania ya Hesabu.</li> </ul> |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kulingana na taarifa ya Madiwani, Halmashauri imethibitisha kuwa haijafanya uwekezaji wowote, lakini jedwali la vifaa na mali za kudumu limeonesha kuwa Halmashauri imefanya uwekezaji wenye thamani ya Sh.79,468,000 kulingana na Aya 16.20 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs).</li> <li>• Thamani ya kituo cha basi cha Kasulu kilichojengwa na Halmashauri katika mwaka 2009/2010 haikujumuishwa katika orodha mali, vifaa na mitambo ya Sh.2,861,407,297 iliooneshwa katika taarifa za fedha.</li> </ul>                    |

|                                 |   |
|---------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Rombo  | <ul style="list-style-type: none"> <li>Mizania ya hesabu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 imeainisha kiasi cha Sh.92,299,856 ikiwa ni tahadari ya kesi zilizopo mahakamani (kama ilivyooneshwa katika kielekezi cha taarifa ya fedha Na. 29) lakini haikuoneshwa katika Mizania ya hesabu kwa mwaka 2009/2010 kinyume na Aya 19 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs).</li> <li>Mizania ya hesabu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2009 ilionesha kuwa kulikuwa na mikopo ya muda mfupi ya Sh.17,244,256 lakini haikuoneshwa katika taarifa ya Mtiririko wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2009/2010.</li> </ul> |
| Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa  | Rasilimali fedha zenye thamani ya Sh.16,102,800 kama zilivyoonekana kwenye kielekezi cha taarifa ya fedha Na. 25 zimeingizwa kwenye taarifa za fedha kwa kutumia bei ya kununulia na siyo bei ya soko kinyume na Aya 15 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.   |
| Halmashauri ya Mji wa Lindi     | Halmashauri imejumuisha kimakosa mali zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kukodishwa zenye thamani ya Sh.10,529,464 katika orodha ya mali, mitambo na vifaa. Mali hizo zilitakiwa zioneshwe kama kitega uchumi kwa thamani ya soko kwa mujibu wa wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma Na. 16.  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Babati | Matumizi yenye jumla ya Sh.233,152,000 ambayo yalitumika katika Vijiji na kata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, lakini kwa makosa matumizi hayo yalioneshwa kama uhamisho wa fedha badala ya matumizi ya kawaida katika Taarifa ya matumizi ya fedha za maendeleo na ugharimiaji.   |

|                                 |  |
|---------------------------------|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Hanang | Matumizi yenyе jumla ya Sh.439,176,000 ambayo yalitumika katika Vijiji na kata kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, lakini kwa makosa matumizi hayo yalioneshwa kama uhamisho wa fedha badala ya matumizi ya kawaida katika Taarifa ya matumizi ya fedha za maendeleo na ugharimiaji. Pia matumizi hayo hapo juu yalijumuisha Sh.68,505,000 ikiwa ni malipo ya posho za madiwani ambayo yalilipwa na Halmashauri lakini bado yakaoneshwa kama uhamisho wa fedha. |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu  | Takwimu ya wadaiwa imejumuisha kiasi cha Sh.73,763,000 ambazo ni uhamisho wa fedha kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo hayo ni madeni ya ndani na siyo wadaiwa wa Halmashauri.  |
| Halmashauri ya Mji wa Babati    | Katika kupitia faili la kesi zilizopo mahakamani imebainika kuwa Halmashauri ina kesi tatu za madai ambazo Halmashauri inadaiwa fidia. Kiasi ambacho kinadaiwa hakijajulikana na uongozi wa Halmashauri haujaonesha katika taarifa zake za fedha kinyume Aya 19.34 ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs).  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Illeje | Taarifa za fedha zimeonyesha bakaa ya vifaa ghalani yenyе thamani ya Sh.32,992,320 lakini haikuambatanishwa na orodha iliyotumika kuhesabia mali.  |
| Halmashauri ya Jiji la Mbeya    | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa za fedha zimeonesha bakaa ya vifaa ghalani vyenye thamani ya Sh.103,601,000 lakini haikuambatanishwa na orodha iliyotumika kuhesabia mali.</li> <li>• Mizania ya hesabu imeonesha Sh.168,715,000 ikiwa ni kitega uchumi kilichowekezwa katika Mfuko wa Mikopo wa Serikali za Mitaa lakini hakuna uthibitisho wa hati au mkataba uliongiwa baina ya Halmashauri na mfuko husika.</li> </ul>                                  |

|                                     |  |
|-------------------------------------|--|
| Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | Mizania ya hesabu kwa mwaka ulioishia Juni, 2010 imeonyesha Sh.1,799,763,375 ikiwa ni bakaa ya fedha taslim. Kati ya fedha hizo Sh.32,073,913 hazikuwa na mchanganuo.  |
| Halmashauri ya Wilaya ya Newala     | Ruzuku ya fidia kwa vyanzo vya mapato vilivyofutwa kwa mwaka wa fedha haikuonyeshwa katika taarifa ya mapato na matumizi. Pia kiasi hicho cha fedha hakikuoneshwa katika Kielekezi cha taarifa za fedha Na.11 ingawaje kimeoneshwa katika ripoti ya Madiwani iliyopo kwenye Kielekezi Na.10.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu   | Kati ya michango ya muda mrefu ya Sh.56,583,600 iliyoonyeshwa katika Mizania ya hesabu, ni kiasi cha Sh.12,500,000 tu ndicho kinahusiana na mwaka wa fedha husika na kupelekea kiasi cha Sh.44,083,600 kuoneshwa kimakosa.   |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda     | Taarifa ya Mtiririko wa fedha imeonesha kuwa kuna kiasi cha fedha kimetolewa kwa ajili ya kununua Mali, Mitambo na Vifaa zenyenye jumla ya Sh.9,131,887,000. Hata hivyo Jedwali la mali za kudumu limeonyesha kuwa mali za kudumu zilizonunuliwa katika mwaka husika ni za Sh.7,486,598,000 na hivyo kupelekea tofauti ya Mali, Mitambo na Vifaa zenyenye thamani ya Sh.1,645,299,000. Hali hii inaashiria kuwa tarakimu katika taarifa ya Mtiririko wa Fedha siyo sahihi. |

|                                 |   |
|---------------------------------|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga | Halmashauri imeonesha kiasi cha Sh.178,287,821 kama Mapato mengineyo ya ndani ya Halmashauri katika taarifa ya Mapato na Matumizi na katika Kielekezi cha taarifa za fedha Na.14. Lakini hapakuwa na jedwali lililoonyesha mchanganuo wa mapato hayo na hivyo nimeshindwa kuthibitisha usahihi wa mapato hayo. Pia mapato hayo hayakuoneshwa katika muhtasari wa taarifa ya mapato iliyoonyeshwa katika ripoti ya Madiwani. |
| Halmashauri ya Mji wa Korogwe   | Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka husika imeonyesha mapato ya Sh.7,189,973 yaliyotokana na makusanyo ya ushuru kutokana shughuli za biashara zinazoendeshwa na Halmashauri. Hata hivyo kiasi hicho kimejumuisha kimakosa kiasi cha Sh.3,967,068 ambazo zimetokana na kodi au faini, ada na tozo.  |
| Halmashauri ya Jiji la Tanga    | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kielekezi Na.20 katika taarifa za fedha kimeonesha kiasi cha Sh.121,406,000 kama ruzuku na malipo ya uhamisho wa fedha ambayo yamejumuisha na posho zilizolipwa na Halmashauri.</li> <li>• Vile vile wakati wa ukaguzi nimebaini malipo ya Sh.1,157,071,778 ikiwa ni ruzuku iliyotolewa kama malipo ya uhamisho wa fedha lakini hayakuoneshwa katika kasma husika.</li> </ul>      |

Kwa kuzingatia mapungufu mbalimbali yaliyoainishwa hapo juu inamaanisha kwamba uongozi wa Halmashauri hauko makini katika uandaaji wa taarifa za fedha kulingana na kasma husika pia waandaaji wa hesabu hawana ujuzi wa kutosha katika uandaaji wa taarifa za fedha. Hivyo, OWM - TAMISEMI inashauriwa kuandaa mafunzo ya mara kwa mara kwa wahasibu wa Halmashuri na viongozi ili kuwajengea uwezo kwa kuandaa taarifa za fedha kulingana Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma.

**(i) Kasma mbalimbali zilizotumia fedha zaidi katika akaunti ya amana**

Halmashauri imeonyesha fedha zilizopo katika akaunti ya Amana kama sehemu ya wadai katika mwaka husika. Hata hivyo, baadhi ya kasma katika akaunti hiyo ya amana zimetumia fedha zaidi ya kiasi kilichowekwa katika akaunti kwa maana hiyo, fedha za kasma nyingine ambazo zimebekwa katika Akaunti hiyo zimetumika na kuathiri mipango iliyopangwa. Hajathibitika kama fedha zilizolipwa kutoka kwenye kasma zisizohusika kama zimerejeshwa. Baadhi ya Halmashauri ambazo zimetumia fedha zaidi ya kiwango kilichowekwa ni kama zifuatazo:

| Halmashauri                      | Fedha zilizolipwa zaidi ya Amana (Sh.) |
|----------------------------------|--|
| Halmashauri ya Wilaya ya Monduli | 98,937,742                             |
| Halmashauri ya Wilaya ya Iringa  | 51,777,574                             |
| Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi | 80,055,753                             |

Akaunti ya Amana imewekwa kwa ajili ya matumizi maalumu, kwa hiyo basi matumizi yote katika Akaunti ya Amana inashauriwa yalipwe katika kasma husika ili kuepuka kutumia fedha zilizowekwa kwa matumizi mengine na kupelekea mipango iliyopangwa kutotekelawa kwa wakati. Pia kwa kutokuwa na udhibiti wa kutosha kunaweza kupelekea fedha kutumika vibaya au kwa matumizi ambayo siyo halali.

### **3.4 Udhibiti wa matumizi**

#### **3.4.1 Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo Sh.2,830,338,208**

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Halmashauri 35 kati ya 134 zilizokaguliwa zilifanya malipo yenye jumla ya Sh.2,830,338,208 ambayo hati za malipo pamoja na

viambatanisho vyake havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi, hali ambayo imepunguza mawanda ya ukaguzi. Kwa kutokuwepo kwa hati za malipo ni kinyume na Agizo Na.368 na 369 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) ambayo kwa pamoja yanaelekeza kuwa hati za malipo pamoja na viambatisho vyake vinatakiwa kuweka vizuri na kutunzwa kwa muda usiopungua miaka mitano (5).


Matumizi yasiyo na hati za malipo yana sababisha kukosekana kwa maelezo muhimu ya malipo hayo kama vile, aina na madhumuni ya malipo. Zaidi ya hapo, kuna uwezekano mkubwa kuwa fedha hizo zimetumika kwa matumizi yasiyohalali.

Kwa vile hili ni tatizo sugu kwa Halmashauri nyingi na kwa muda mrefu, ningependa kuwakumbusha Maafisa Masuuli na menejimenti za Halmashauri kuhusu wajibu wao katika kuhakikisha kuwa nyaraka muhimu za Halmashauri zikiwemo hati za malipo zinatunzwa vizuri na kuwasilishwa kwa ukaguzi zinapohitajika. Halmashauri zilizokuwa na matumizi bila hati za malipo zimeainishwa katika kiambatisho Na.7.

Kwa muhtasari idadi ya Halmashauri zilizokuwa na matumizi yasiyokuwa na hati za malipo kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 imeoneshwa katika jedwali hapa chini:

| Mwaka     | Kiasi (Sh.)   | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|---------------|----------------------|
| 2008/2009 | 2,526,117,587 | 33                   |
| 2009/2010 | 2,830,338,208 | 35                   |

Taarifa hii inaweza kuoneshwa katika chati mihimili ifuatayo:



Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kutunza nakala halisi za hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake kwa kila mwaka.

### 3.4.2 Malipo yeye nyaraka pungufu Sh.5,515,453,908


Agizo Na. (5) (c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linataka malipo yote yanayofanywa kutokana na fedha za Halmashauri yawe na viambatisho vinavyothibitisha malipo kufanyika.

Wakati wa ukaguzi imebainika kwamba Halmashauri 71 zilifanya malipo yeye nyaraka pungufu ya jumla ya Sh.5,515,453,908 kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu. Halmashauri zilizofanya matumizi yeye nyaraka pungufu zimeoneshwa katika **kiambatisho Na.8** katika ripoti hii.

Kwa muhtasari idadi ya Halmashauri zenye matumizi yeye nyaraka pungufu kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010 zimeoneshwa katika jedwali hapa chini:

| Mwaka     | Kiasi (Sh.)   | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|---------------|----------------------|
| 2008/2009 | 5,313,071,671 | 62                   |
| 2009/2010 | 5,515,453,908 | 71                   |

Taarifa hiyo inaonyeshwa pia katika Chati Mihimili hapa chini:



Ninashauri kwamba malipo yote ni lazima yaambatishwe na nyaraka zinazohusiana kama vile ankara, risiti, jedwali la malipo lilisainiwa, hati ya kupokelea vifaa na maombi ya karadha n.k. ili kuwezesha uhakiki wa malipo kufanyika kwa ufanisi na kwa jinsi yalivyotokea. Nyaraka zinazohusiana ni lazima zihifadhiwe na menejimenti ya Halmashauri na kutolewa wakati wote zinapohitajika.

#### **3.4.3 Madai ya miaka ya nyuma yaliyolipwa Sh.620,278,565**

Agizo Na. 46 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linalekeza kwamba, malipo yote yanatakiwa yalipwe katika mwaka husika wa fedha au malipo ambayo hayakulipwa yanatakiwa kuonyeshwa katika orodha ya wadai wa Halmashauri lakini malipo yasije yakaachwa kulipwa tu kwa sababu ya kukwepa kuonyesha matumizi ya ziada katika taarifa za fedha.

Katika mwaka husika wa ukaguzi imebainika kwamba kiasi cha Sh.620,278,565 ambacho kinahusisha matumizi yaliyolipwa katika Halmashauri 24 kilitakiwa kilipwe katika

mwaka wa fedha 2008/2009, lakini malipo hayo yamefanyika katika mwaka wa fedha 2009/2010 kinyume na Agizo lililotajwa hapo juu. Pia hakuna uthibitisho kuwa malipo hayo yalikuwa katika orodha ya Wadai wa Halmashauri katika mwaka wa fedha 2008/2009. Angalia **kiambatanisho 9.**

#### **3.4.4 Kutooneka kwa stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji Sh.8,074,271,947**

Malipo ya Sh.8,074,271,947 yalilipwa moja kwa moja na Hazina kwenda kwenye Taasisi mbalimbali ikiwa ni makato ya kisheria, lakini malipo hayo hayakuweza kuthibitika kama yamepokelewa na Taasisi husika kwa vile hazikuweza kukiri mapokezi hayo kwa kutoa stakabadhi/ risiti ya kukiri kupokea kiasi cha fedha kilicholipwa. Kutokuwepo kwa stakabadhi hizo ni kinyume na kinyume na Agizo Na. 5 (c) la Memoranda ya Fedha za Serikali za Mitaa la mwaka 1997. Halmashauri nane (8) ambazo zimebainika kuwa na malipo ambayo hayana stakabadhi/risiti za kukiri malipo yaliyolipwa zimeonyeshwa katika majedwali hapo chini:

- (i) Makato ya kisheria kutoka katika mishahara yaliyolipwa moja kwa moja na Hazina -Sh.7,570,902,570**

| <b>Na.</b>   | <b>Halmashauri</b>               | <b>Kiasi (Sh.)</b>   |
|--------------|----------------------------------|----------------------|
| 1            | Halmashauri ya Wilaya ya Hai     | 3,522,681,073        |
| 2            | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo   | 2,294,823,312        |
| 3            | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi | 1,753,398,185        |
| <b>Jumla</b> |                                  | <b>7,570,902,570</b> |

- (ii) Makato ya kisheria kutoka katika mishahara yaliyolipwa na Halmashauri husika Sh.503,369,377**

| Na.          | Halmashauri                         | Kiasi (Sh.)        |
|--------------|-------------------------------------|--------------------|
| 1            | Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba     | 222,575,000        |
| 2            | Halmashauri ya Wilaya ya Babati     | 117,023,587        |
| 3            | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | 104,375,500        |
| 4            | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo    | 30,280,834         |
| 5            | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia      | 29,114,456         |
| <b>Jumla</b> |                                     | <b>503,369,377</b> |

Menejimenti za Halmashauri inatakiwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kuwa malipo yote yanayofanywa kwenye taasisi mbalimbali ni lazima yawe na stakabadhi za kukiri mapokezi ya fedha zilizolipwa. Pia hizo stakabidhi za kukiri mapokezi zinatakiwa zitunzwe vizuri na zipatikane wakati wowote zinapohitajika.

### 3.5 Ukaguzi wa Mishahara

Katika kuitia taarifa za mishahara zilizoandaliwa katika Halmashauri mbalimbali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 nimebaini mapungufu yafuatavyo:

#### 3.5.1 Mishahara isiyolipwa ambayo haikurejeshwa Hazina Sh.1,185,252,606

Agizo Na. 307 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaagiza kwamba mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe benki ndani ya siku kumi (10) za kazi. Pia maelekezo kutoka Wizara ya Fedha ambayo yalitolewa kwa barua yenyе kumbukumbu Na. EB/AG/5/03/01/Vol.VI/136 ya tarehe 31 Agosti, 2007 ambayo inaelekeza kwamba mishahara yote isiyolipwa inatakiwa kurejeshwa Hazina kuitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa. Kinyume na maelekezo yaliyotolewa, katika ukaguzi wa mishahara imebainika kwamba kuna mishahara

isiyolipwa kiasi cha Sh.1,185,252,606 katika Halmashauri 55 haikuweza kurejeshwa Hazina. Angalia **kiambatisho 10.**

### **3.5.2 Mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliostaafu, kuachishwa kazi na watoro Sh.583,221,297**

Ukaguzi wa kumbukumbu za mishahara ikiwemo taarifa za mishahara ilioandaliwa kwa komputa na rejista za mishahara isiyolipwa katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2010, imebainika kwamba kiasi cha Sh.583,221,297 cha mishahara kililipwa na Halmashauri 38 kwa watumishi ambao aidha wamestaafu, wameachishwa kazi au wametoroka na majina yao yameendelea kuonekana katika taarifa za mishahara ilioandaliwa kwa komputa. Angalia **kiambatanisho 11.**

### **3.5.3 Tofauti kati ya fedha za mishahara zilizopokelewa toka Hazina na fedha zilizolipwa Sh.790,203,584**

Katika kulinganisha taarifa za mishahara kutoka Hazina na kiasi cha fedha kilicholipwa kwa watumishi kwa ajili ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2009/2010 imebainika tofauti ya Sh.790,203,584. Tofauti hiyo imeonekana katika Halmashauri sita (6) kama ilivyo katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri                       | Kiasi<br>kilichopokelewa<br>(Sh.) | Kiasi<br>kilicholipwa<br>(Sh.) | Tofauti<br>(Sh.)     |
|-----|-----------------------------------|-----------------------------------|--------------------------------|----------------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Sihia    | 3,201,721,056                     | 2,819,238,923                  | 382,482,133          |
| 2.  | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo    | 11,075,806,996                    | 11,183,922,726                 | (108,115,730 )       |
| 3.  | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi  | 8,204,205,453                     | 9,399,577,761                  | (1,195,372,308)      |
| 4.  | Halmashauri ya Wilaya ya Songea   | 6,035,775,448                     | 5,950,532,590                  | 85,242,858           |
| 5.  | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke | 19,177,406,550                    | 19,137,802,440                 | 39,604,110           |
| 6.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mafia    | 1,845,124,098                     | 1,839,168,745                  | 5,955,353            |
|     | <b>Jumla</b>                      | <b>49,540,039,601</b>             | <b>50,330,243,185</b>          | <b>(790,203,584)</b> |

### **3.5.4 Marejesho ya mikopo kwa watumishi ambao si wafanyakazi tena wa Halmashauri Sh.290,174,973**

Ukaguzi wa mishahara na nyaraka zake umebaini kwamba kiasi cha Sh.290,174,973 kililipwa na Halmashauri sita (6) kwa taasisi mbalimbali za fedha ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyochukuliwa na waliokuwa watumishi wa Halmashauri. Hata hivyo upembuzi yakinifu wa taarifa za mishahara ulibaininisha kuwa, watumishi hao walishaacha utumishi hivyo hawakustahili kuendelea kulipwa mishahara.

Malipo yaliyofanyika katika Halmashauri hizo yameainishwa katika jedwali lifuatalo:

| <b>Na.</b> | <b>Halmashauri</b>                | <b>Kiasi (Sh).</b> |
|------------|-----------------------------------|--------------------|
| 1          | Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba   | 227,569,484        |
| 2          | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo  | 22,271,871         |
| 3          | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo    | 18,313,962         |
| 4          | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi  | 15,255,618         |
| 5          | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | 3,626,840          |
| 6          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbanga   | 3,137,198          |
|            | <b>Jumla</b>                      | <b>290,174,973</b> |

Mfumo wa udhibiti wa ndani wa mishahara umekuwa ni changamoto katika Halmashauri nyingi kwa hiyo menejimenti katika Halmashauri husika zinatakiwa kuimarisha mifumo ya ndani ili kuweza kuthibiti matumizi yasiyo na tija kwa Serikali kuitia malipo ya mishahara.

### **3.5.5 Mikopo ya watumishi isiyodhibitiwa**

Waraka wa watumishi Na. CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2009 unaelekeza kwamba makato katika mishahara ya watumishi inatakiwa isizidi theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao. Hata hivyo imebainika kwamba kuna wafanyakazi wengi wa Halmashauri wanakatwa mishahara yao zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya mishahara yao. Pia kuna baadhi ya watumishi wamekuwa wakikatwa mshahara wote. Mfano ni Manispaa ya Dodoma, katika mishahara ya watumishi 198 iliyohakikiwa imebainika kwamba watumishi 45 ambao ni sawa na 23% hawapati mishahara kabisa. Katika Halmashauri chache zilizokaguliwa imebainika kwamba Halmashauri 36 zimekiuka maelekezo ya Waraka wa Utumishi ultajwa hapo juu. Angalia **kiambatisho 12.**

Kwa watumishi kuendelea kukatwa zaidi ya mishahara bila kudhibitiwa inaweza kuleta madhara makubwa kwa watumishi husika kama vile kutokuwa na utendaji mzuri wa kazi unaosababishwa na kutokuwa na mishahara. Matatizo hayo ya mishahara yanachangiwa na menejimenti za Halmashauri kwa kutokuwa makini kwa kuhakikisha masilahi ya wafanyakazi yanalindwa.

Usimamizi wa mishahara usizingatie tu kuwa mfanyakazi analipwa stahili yake ya mshahara ila mwajiri anatakiwa kuhakikisha kuwa mfanyakazi anapata mshahara mwisho wa mwezi ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi.

### **3.6 Matumizi ya fedha zilizotolewa kwa watu waliopata maafa**

Majanga yanaleta usumbufu mkubwa katika utendaji wa shughuli za jamii iliyopata maafa kwa kupotelewa na vifaa mbali mbali na uharibifu wa mazingira ambako kunapelekea ugumu kwa jamii husika kuweza kukabiliana na majanga kwa kutumia rasilimali walizonazo peke yake.

Katika aya hii tumedhamiria kutathmini matumizi ya fedha na vifaa mbalimbali ambavyo vilitolewa kama msaada kwa

waathirika wa majanga ya mafuriko na ya milipuko wa mabomu yaliyotokea haswa katika Halmashauri za Wilaya za Kilosa, Iringa, Same, Mpwapwa na mkoa wa Dar es Salaam.

**3.6.1 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa - Fedha taslimu na vifaa mbali mbali havikuthibitika kupokelewa na kuingizwa katika taarifa za fedha za Halmashauri Sh.193,901,000**  
 Kutokana na Mvua kubwa iliyonyesha mkoani Dodoma tarehe 26 Disemba 2009, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilikumbwa na mafuriko yaliyoanzia Mjini Dodoma, Mpwapwa na Halmashauri ya Kongwa na kupelekea michango ya dharura ikiwemo chakula na vifaa mbali mbali kupelekwa sehemu ya tukio ili kusaidia wananchi waliopatwa na majanga ya mafuriko.

Hata hivyo wakati wa kukagua taarifa mbalimbali za mapokezi ya misaada na taarifa za fedha imebainika kwamba misaada ya fedha taslimu na vifaa vingine vilivyotolewa havikuweza kupokelewa kwa kutumia stakabadhi/risiti ya kukiri mapokezi na kuonyeshwa kwenye taarifa za fedha za Halmashauri. Misaada ilivoletwa katika Halmashauri ni kama inavyoonekana katika jedwali:

#### **Fedha taslimu zilizochangwa Sh.69,441,000**

| Taasisi husika                  | Fedha taslim<br>(Sh.) | Kumb. Na.         |
|---------------------------------|-----------------------|-------------------|
| Rotary Club of Morogoro Central | 400,000               | AB.74/175/01 F.7  |
| MMCF                            | 3,900,000             | AB.74/175/01 F.25 |
| Chuo Kikuu cha Mzumbe           | 1,000,000             | AB.74/175/01 F.27 |
| Rotary Club of Morogoro Central | 500,000               | AB.74/175/01 F.31 |
| Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mara   | 5,000,000             | AB.74/175/01 F.61 |
| KKKT Morogoro Diocese           | 1,300,000             | AB.74/175/01 F.80 |
| Ofisi ya Katibu Tawala -        | 9,200,000             | AB.74/175/01 F.64 |

| Pwani                                       |                   |                          |
|---|-------------------|--------------------------|
| Chuo cha Ualimu Morogoro.                   | 1,000,000         | AB.74/175/01 F.120       |
| Ofisi ya Waziri Mkuu                        | 4,940,000         | AB.74/175/01 F.65<br>"B" |
| ELGBO SACCOS Morogoro                       | 200,000           | AB.74/175/01 F.11<br>"B" |
| Chuo kikuu cha Mzumbe University            | 1,200,000         | AB.74/175/01 F.1 "B"     |
| Tanzania Association of Foresters           | 301,000           | AB.74/175/01 F.117       |
| Morogoro Municipal Community Foundation     | 500,000           | AB.74/175/01 F.112       |
| Clouds Entertainment and Vodacom Foundation | 40,000,000        | AB.74/175/01 F.93        |
| <b>Jumla</b>                                | <b>69,441,000</b> |                          |

**Michango ya vifaa mbalimbali Sh.82,460,000**

| Taasisi husika                                  | Vifaa                            | Kiasi (Sh.) | Kumb.Na.                 |
|---|----------------------------------|-------------|--------------------------|
| Karimjee Jivanjee Foundation and Toyota Tz. ltd | Magodoro 2000 na mablanjeti 2000 | 75,000,000  | AB.74/175/01 F.87 and 88 |
| Staff of Tanzania High Commission Nairobi Kenya | Vyandaura 232                    | 1,360,000   | AB.74/175/01 F.110       |
| Free Pentecostal Church of Tanzania             | Mabati 50 geji 30, nguo          | 1,300,000   | 39 of 27/5/2010          |
| Anglikana Coast Diocese                         | Vyakula na nguo                  | 2,300,000   | 160 of 22/1/2010         |
| DAWASA  | Mahindi                          | 1,500,000   | 98                       |
| DAWASA/ DAWASCO                                 | Mahindi                          | 1,000,000   | 98                       |

**Mchango wa Euro 20,000**

| Jina la Taasisi    | Vifaa              | Kumb. Na.    |
|--------------------|--------------------|--------------|
| Care International | Vifaa vya shule na | AB.74/175/01 |

|             |         |       |
|-------------|---------|-------|
| In Tanzania | masweta | F.106 |
|-------------|---------|-------|

### Michango ambayo thamani yake haijulikani

| Taasisi           | Msaada               | Kumb.             |
|-------------------|----------------------|-------------------|
| Serikali ya Libya | Ujenzi wa nyumba 200 | AB.74/175/01 F.93 |

#### 3.6.2 Halmashauri ya Wilaya ya Iringa - Fedha pungufu zilizotumwa kutokana na mauzo ya mahindi ya njaa Sh.74,674,500

Katika mwaka fedha wa ukaguzi, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilipokea tani 2908.8 za mahindi kutoka Kamati ya Maafa kwa ajili ya wananchi walioathiriwa na mafuriko katika kijiji cha Idodi katika kata ya Ismani. Usambazaji wa mahindi hayo ulikuwa kama ifuatavyo:

- Tani 126.1 zilisambazwa bure kwa familia ambazo hazikuwa na uwezo.
- Tani 2782.7 ziliuzwa kwa bei ndogo ya Sh.50 kwa kilo.

Katika kukagua mapato yaliyotokana na mauzo ya Tani 2,782.7 za mahindi ilibainika kwamba jumla ya mauzo ya Sh.139,135,000 zilipatikana na kiasi cha Sh.64,460,500 ndicho tu kilichowasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha Maafa na kubakia Sh.74,674,500. Pia kiasi cha fedha kilichopelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu hakijathibitika kupokelewa kwa vile hapakuwa na stakabadhi ya kukiri kupokea kiasi hicho cha fedha.

#### 3.6.3 Halmashauri ya Wilaya ya Same

##### (i) Malipo ya ziada yaliyotokana na malipo ya maafa katika kijiji cha MambaMiamba Sh.4,684,256

Katika kupitia taarifa katika akaunti ya Amana imeonesha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Same ilipata kiasi cha Sh.36,694,500 ikiwa ni michango kwa ajili ya waathirika wa maporomoko ya ardhi katika kijiji cha Mamba Miamba lakini Halmashauri iliweza kutumia kiasi cha Sh.41,378,756 na kusababisha matumizi ya ziada ya Sh.4,684,256 sawa na

12.8% ya fedha zote zilizopokelewa katika Kasma ya maafa katika Akaunti ya Amana.

(ii) **Matumizi ambayo hayakuwa na viambatisho vinavyothibitisha malipo kufanyika**

Udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani umesababisha Halmashauri kufanya malipo ya Sh.2,000,000 bila kuwa na viambatisho ili kuthibitisha kwamba fedha zilizolipwa zimepokelewa. Kutokuwepo kwa viambatisho vya kutosha ni kinyume na Agizo Na. 5 (c) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na kunapelekea uhalali wa malipo hayo kutothibitika.

**3.6.4 Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa - Bakaa ya fedha za dharura Sh.100,201,000**

Menejimenti ya Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ilipeleka ombi maalum la fedha kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha kwa ajili ya ukarabati wa dharura katika barabara ya Chiseyu-Msagali ambayo iliharibiwa na mvua kubwa zilizonyesha mwezi Disemba, 2009.

Ombi hilo la fedha liliombwa kwa barua yenyewe kumbukumbu Na. HW/MPW/R.10/ 10/3 ya tarehe 05 Februari, 2010. Mnamo tarehe 1 Machi, 2010 OWM-TAMISEMI ilimwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mpwapwa barua yenyewe kumbukumbu Na. FA.307/488/OIJ/21 kumjulisha kuwa Wizara imetuma kiasi cha Sh.230,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo. Halmashauri ilikiri mapokezi ya fedha hizo terehe 28 Februari, 2010 kwa stakabadhi Na. HW5 No. 00130240 na kuingizwa katika mfuko wa barabara.

Wakati fedha hizo zinapokelewa tayari Halmashauri ilikwishaingia mkataba na M/S Singida General Supplies Co. Ltd kwa ukarabati mdogo wa barabara hiyo hiyo kwa Mkataba Na. MDC/RFB/RD/C04/09/10 wa Sh.129,799,000. Hata hivyo, mkataba wa kazi hiyo ultolewa mwezi Disemba, 2009 kabla ya mafuriko kutokeea na mkataba wa

nyongeza kwa kazi za ziada haukuweza kupatikana wakati wa ukaguzi.

Mikataba mingine ya kazi ya barabara ilioingiwa tarehe 8 Julai, 2010 katika barabara hiyo hiyo ni kama ifuatavyo:

| Mkataba Na.             | Kiasi cha Mkataba (Sh.) | Mkandarasi                                    | Kiasi kilicholipwa (Sh.) |
|-------------------------|-------------------------|---|--------------------------|
| MDC/RFB/RD/01/2010/2011 | 42,800,000              | Ms Peace Construction                         | 42,800,000               |
| MDC/RFB/RD/02/2010/2011 | 76,536,000              | Ms Joroji Contractors Co. Ltd                 | 35,000,000               |
| MDC/RFB/RD/03/2010/2011 | 49,580,000              | Ms Hakika Contractors and Civil Engineers Co. | 168,916,000              |
| Jumla                   | 168,916,000             |   | 246,716,000              |

Hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2009/2010, bakaa ya Sh.100,201,000 ilibaki kutokana na fedha hizo za dharura na zikajumuishwa na fedha zingine za mfuko wa barabara katika mwaka wa fedha 2010/2011. Kutokana na bakaa hii inaashiria kulikuwa na makisio makubwa ya fedha zilizoombwa na Halmashauri.

### 3.6.5 Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam - Fidia kwa waathirika wa milipuko ya Mabomu Mbagala Sh.8,669,779,560

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Ofisi ya Katibu Tawala ya Mkoa wa Dar es Salaam ilipokea jumla ya Sh.8,669,779,560 kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu ikiwa ni malipo ya fidia kwa waathirika wa milipuko ya mabomu Mbagala. Mapokezi ya fedha yalikuwa kama yanavyoonekana katika jedwali hapo chini:

| Stakabadhi ya Serikali Na./Tarehe | Kiasi (Sh.)   | Akaunti |
|-----------------------------------|---------------|---------|
| 24344829 ya tarehe 14/08/2009     | 8,050,000,000 | Amana   |

|                                  |                      |       |
|----------------------------------|----------------------|-------|
| 24344833 ya tarehe<br>16/10/2009 | 84,266,000           | Amana |
| 24344832 ya tarehe<br>09/10/2009 | 380,080,300          | Amana |
| 24344516 ya tarehe<br>17/06/2010 | 136,313,060          | Amana |
| 24344545 ya tarehe<br>02/08/2010 | 4,120,200            | Amana |
| 24344438 tarehe<br>21/12/2009    | 15,000,000           | Amana |
| <b>Jumla</b>                     | <b>8,669,779,560</b> |       |

Hata hivyo hati za malipo zilizohusika na malipo ya fidia ziliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi bila kuwa na viambatisho au nyaraka zinazohusiana na malipo hayo ikiwa ni kinyume na Kanuni Na.86 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001(zilivyorekebishwa 2004) ambayo inaelekeza kuwa hati za malipo zinatakiwa ziwe na viambatisho vinavyoonyesha taarifa muhimu za malipo hayo.

Kwa kuzingatia mapungufu yaliyojitokeza katika kuainisha matumizi ya fedha na vifaa mbali mbali vilivyotolewa kama misaada kwa waathirika wa majanga mbalimbali yaliyotokea nchini, ni muhimu kwa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kuweka utaratibu mzuri kwa kuwasaidia waathirika wa majanga mbalimbali kwa kuweka vizuri taarifa za fedha na vifaa vilivyotolewa kwa ajili hiyo na kuwa na makadirio ambayo ni sahihi ya fedha zitakazombwa Serikalini kwa ajili ya majanga. Kwa kuongezea, Taasisi mbalimbali zinazohusika na majanga hapa nchini zinatakiwa kuimarisha utaratibu wa usimamizi na kuzidisha ushirikiano ili kujenga umaja na kuondoa tishio la maafa nchini.

### 3.7 Ukaguzi wa Maduhuli ya Halmashauri

#### 3.7.1 Vitabu vya Makusanyo visivyowasilishwa

Agizo Na. 101 na 102 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka, 1997 linawataka maafisa wote waliopewa vitabu nya makusanyo kuwasilisha taarifa ya vitabu vilivyotumika na vile ambavyo havijatumika kwa kila mwisho wa mwezi na endapo kuna upotevu wowote wa vitabu, uripotiwe kwa afisa anayehusika mapema iwezekanavyo. Nakala ya ripoti hiyo iwasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kinyume na maagizo haya, vitabu 948 nya makusanyo toka Halmashauri 48 havikupatikana kwa ajili ya ukaguzi kama inavyoonyesha kwenye mchanganuo ufuatao na kiambatisho Na. 13.

**Muhtasari wa vitabu nya makusanyo visiviyowasilishwa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010**

| Mwaka     | Idadi ya vitabu vilivyokosekana | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|---------------------------------|----------------------|
| 2008/2009 | 1341                            | 50                   |
| 2009/2010 | 948                             | 48                   |

- Kwa kuwa vitabu hivi vilikusudiwa kukusanya mapato ya Halmashauri, sikuweza kujua mara moja ni kiasi gani kilikusanywa kwa kutumia vitabu hivyo.
- Kuna uwezekano mkubwa wa wizi wa mapato ya Halmashauri na kupotosha makisio ya mapato ya Halmashauri.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuweka mifumo imara ya udhibiti wa vitabu nya makusanyo ili kuondoa uwezekano wa upotevu wa fedha za Halmashauri. Vilevile Halmashauri husika zinatakiwa kuwasilisha vitabu vilivyokosekana kwa ajili ya ukaguzi na kuchukua hatua za haraka ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria wale wote walioshindwa kuwasilisha makusanyo ya Halmashauri.

### **3.7.2 Maduhuli yasiyorejeshwa na Mawakala wa Makusanyo Sh.2,608,924,620**

Agizo Na. 110 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 makusanyo yote ya Halmashauri yawasilishwe kwa watunza fedha wa Halmashauri husika kwa usalama. Kinyume na Agizo hilo, ukaguzi uliofanywa kwenye Halmashauri 43 kwa kipindi cha mwaka huu wa fedha ulibaini kiasi cha Sh.2,608,924,620 kilichokusanya na Mawakala mbalimbali lakini hakikuwasilishwa kwa mtunza fedha kama inavyoonyesha kwenye mchanganuo ufuatao na kiambatisho Na. 14.

**Mchanganuo wa maduhuli yasiyowasilishwa kwenye Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010**

| Mwaka     | Maduhuli yasiyowasilishwa | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|---------------------------|----------------------|
| 2008/2009 | 1,095,113,399             | 43                   |
| 2009/2010 | 2,608,924,620             | 43                   |

Kutokana na jedwali hapo juu, kiasi cha makusanyo yasiyowasilishwa kimeongezeka kutoka Sh.1,095,113,399 hadi Sh.2,608,924,620. Hii inaonyesha udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani na mapungufu katika usimamizi wa mikataba ya makusanyo.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuimarisha udhibiti wa ndani katika makusanyo ya maduhuli yatokanayo na vyanzo vyatofauti na kuboresha taratibu za kuingia mikataba na kufuatilia marejesho kutoka kwa mawakala wa makusanyo.

### **3.7.3 Ushuru usiolipwa kutoka minara ya simu, mabango ya matangazo na mazao Sh.745,038,193**

Agizo Na. 120 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka, 1997 linalezea kuwa ni jukumu Mweka Hazina wa Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kiuhasibu ili kuhakikisha usahihi katika ukusanyaji na utunzaji wa fedha zote za Halmashauri. Kinyume na Agizo hili, ukaguzi umebaini kuwa, maduhuli ya Sh.745,038,193 yatokanayo na ushuru wa minara ya simu, mabango ya matangazo na mazao hayakukusanywa na Halmashauri sita (6) kutoka kwa walipa kodi husika kama ifuatavyo:

| <b>Na</b>    | <b>Halmashauri</b>                  | <b>Chanzo cha mapato</b> | <b>Kiasi kisichokusanywa (Sh.)</b> |
|--------------|-------------------------------------|--------------------------|------------------------------------|
| 1.           | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala    | Minara ya mawasiliano    | 193,598,000                        |
| 2.           | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma   | Mabango ya matangazo     | 26,963,920                         |
| 3.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero    | Ushuru wa Mazao          | 248,103,791                        |
| 4.           | Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro | Vyanzo mbalimbali        | 197,354,831                        |
| 5.           | Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba | Ushuru wa mazao          | 69,030,155                         |
| 6.           | Halmashauri ya Manispaa ya Singida  | Ada ya kamisheni         | 9,987,496                          |
| <b>Jumla</b> |                                     |                          | <b>745,038,193</b>                 |

Hali hii sio tu inaashiria udhaifu katika kutumia fursa mbalimbali za ukasanyaji wa maduhuli bali pia inaonesha jinsi Halmashauri zinavyoshindwa kuboresha vyanzo vyataga mapato vilivyopo. Kwa hiyo, ni jukumu la menejimenti za Halmashauri kuweka mipango thabiti ya kiuhasibu ili kuhakikisha ukusanyaji na utunzaji mzuri wa maduhuli.

## **3.8 Usimamizi wa Mali na Madeni ya Muda Mfupi**

### **3.8.1 Usimamizi wa fedha**

Usimamizi wa fedha kwa ujumla unahusisha makusanyo na mapokezi ya fedha za Umma na pia usimamizi wa akaunti za benki za Halmashauri. Ukaguzi wa usimamizi wa fedha katika Halmashauri mbalimbali ulibaini mambo yafuatayo:

#### **3.8.1.1 Masuala yasiyoshughulikiwa ya usuluuhisho wa kibenki**

Agizo Na. 68 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) linasema kwamba waweka Hazina katika Halmashauri wahakikishe kuwa usuluuhisho wa kibenki ukiwemo udhibiti kati ya kitabu cha mapato na hati za benki zinafanywa walau mara moja kwa kila mwezi na kufanya marekebisho katika vitabu vya hesabu.

Kinyume na Agizo hili, Halmashauri mia moja na tatu (103) zilikuwa na masuala yasiyoshughulikiwa kama vile; mapokezi kwenye vitabu lakini hayakuingia benki, hundi zisizowasilishwa benki, malipo yaliyoko benki lakini hayapo kwenye vitabu na mapato yaliyoko kwenye benki lakini hayako kwenye vitabu. Pia hakuna ushahidi unaoonyesha kuwa taarifa za suluuhisho za kibenki zinahakikiwa na maafisa wafawidhi. Mchanganuo wa masuala yasiyoshughulikiwa kwenye suluuhisho za kibenki kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010 ni kama ifuatavyo:

- Kiasi cha Sh.9,612,413,862 kilikuwa mapato katika daftari la fedha ambayo hayapo katika taarifa za benki.
- Kiasi za Sh.28,792,732,991 zilizolipwa kwa watu mbalimbali hazikuwasilishwa benki hadi mwaka wa fedha ulivyofungwa tarehe 30 Juni 2010.
- Kiasi cha Sh. 805,665,694 kutoka Halmashauri mbalimbali zilikuwa ni fedha ambazo hazijafika benki.

Hakuna jitihada zilizochukuliwa kuhakikisha zinaingia benki.


- Kiasi cha Sh. 2,586,187,823 kilichukuliwa kwenye taarifa za benki za Halmashauri lakini hazikuingizwa kwenye daftari za fedha.
- Kiasi cha Sh. 1,257,775,757 kilipokelewa kwenye taarifa za benki mbalimbali za Halmashauri lakini hazikuingizwa kwenye vitabu vya fedha.

Mchanganuo masuala yasiyosuluhihwa na Halmashauri husika umeonyeshwa kwenye kiambatisho Na. 15.

Jedwali lifuatelo linaonyesha mchanganuo wa masuala yasiyosuluhihwa kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010.

| Mwaka   | Mapokezi katika daftari la fedha hayapo katika taarifa za benki (Sh.) | Hundi ambazo Hazikupelekwa Benki (Sh.) | Fedha ambazo hazijafika benki (Sh.) | Malipo benki hayajaingiz wa katika daftari la fedha (Sh.) | Mapato benki hayakuoneka katika daftari la fedha (Sh.) |
|---------|---|--|-------------------------------------|---|--|
| 2008/09 | 3,160,893,295   | 10,895,917,505                         | 350,907,782                         | 838,210,104   | 1, 634,905,409   |
| 2009/10 | 9,612,413,862   | 28,792,732,991                         | 805,665,694                         | 2,586,187,823   | 1,257,775,757  |

Jedwali hapo juu linaweza kuonyeshwa kwenye chati mihimili ufuatao:



- Mwenendo unaonyesha kwamba mapokezi katika daftari la fedha lakini hayapo katika taarifa za benki kwa mwaka 2008/09 yalikuwa Sh.3,160,893,295 wakati mwaka 2009/10 zilikuwa Sh.9,612,413,862.
- Hundu ambazo ziliandaliwa kwa malipo ya wateja mbalimbali lakini hazikupelekwa benki kwa Mwaka 2008/2009 zilikuwa Sh.10,895,917,505 wakati mwaka 2009/2010 zilikuwa Sh.28,792,732,991.
- Fedha ambazo hazijaingizwa katika akaunti ya Halmashauri kwa Mwaka 2008/2009 zilikuwa ni Sh.350,907,782 wakati kwa Mwaka 2009/2010 zilikuwa Sh.805,665,694.
- Kiasi cha Sh.838,210,104 zilitolewa katika akaunti za benki lakini hazikuingizwa katika daftari za fedha za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2008/2009 wakati Sh.2,586,187,823 zililipwa benki katika mwaka wa fedha 2009/2010 bila kuingizwa kwenye daftari la fedha.
- Jumla ya mapato ya 1,634,905,409 yaliyoingia benki lakini hayakuonekana katika daftari za fedha za Halmashauri kwa mwaka 2008/2009 wakati kwa mwaka 2009/2010 jumla ya Sh.1,257,775,757 ziliingia benki lakini hazikuoneka katika daftari za fedha za Halmashauri.

Makosa na ubadirifu wa fedha za Serikali unaweza usibainike kwa muda mrefu kama mambo yanayohusu usuluhishi wa benki hayatarekebishwa mapema. Kwa hali

hiyo, menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa usuluhisho wa benki unafanywa kila mwezi na kuidhinishwa na maafisa waandamizi, pia marekebisho yafanyike katika vitabu nya hesabu.

### 3.8.2 Uhakiki wa fedha na Ukaguzi wa kushtukiza

#### (i) **Ukaguzi wa Kushtukiza**

Agizo Na.170 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri au Mwakilishi wake kuratibu uhakiki wa fedha taslimu wa kushtukiza mara kwa mara. Kinyume na agizo hili, ukaguzi umebaini kuwa, Halmashauri 34 kama inavyoonekana katika **kiambatisho 16**, hazikuwa na utaratibu wala hazikufanya uhakiki wa fedha.

#### (ii) **Kiwango cha juu cha kutunza fedha**

Agizo Na.352 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaitaka Halmashauri kwa kutumia kamati ya Fedha na Mipango kuweka kiwango cha juu cha kuhifadhi fedha katika ofisi ya Halmashauri na kiwango hicho hakitakiwi kuzidi bila kibali cha kamati. Ukaguzi wa kushtukiza uliofanywa katika Halmashauri sita (6) ulibaini kuwa, Halmashauri hizo hazina viwango maalumu vilivyoidhinishwa na kamati za fedha kinyume na Agizo kama ilivyooneshwa katika **kiambatisho 16**.

### 3.8.3 Wadaiwa wasiolipa Sh.44,059,104,038

Ukaguzi wa taarifa za fedha za Halmashauri mia moja na tisa (109) umeonyesha jumla ya Sh.44,059,104,038 ikiwa ni madai mbalimbali ambayo hayajarejeshwa kama ilivyoainishwa kwenye **kiambatisho 17**.

Aina za wadaiwa katika Halmashauri zilikuwa kama ifuatavyo:


- Fedha iliyolipwa kabla ya huduma,
- Maduhuli kutoka kwa mawakala wa kukusanya mapato

- Masurufu na karadha za watumishi
- Mikopo ya Wanawake na Vijana

Fedha za Halmashauri zinazoshikiliwa na wadaiwa sio tu kwamba ni kinyume na Agizo Na. 120 na 121 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 bali pia inaathiri mitaji ya kujiendeshea na kuchelewesha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

Jedwali hapa chini linaonyesha ulinganisho wa wadaiwa kwa miaka miwili ya 2008/2009 na 2009/2010.

| Mwaka     | Kiasi (Sh.)    | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|----------------|----------------------|
| 2007/2008 | 35,644,785,554 | 113                  |
| 2008/2009 | 44,059,104,038 | 109                  |



Jedwali hapo juu linaonyesha ongezeko la wadaiwa kwa Sh.8,414,318,484 kutoka Sh.35,644,785,554 zilizotolewa kwenye taarifa ya mwaka uliopita hadi Sh.44,059,104,038 kwa mwaka huu wa fedha.

Hii ni kinyume na Agizo Na 120 na 121 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 ambalo linaeleza wazi kuwa “litakuwa jukumu la mweka hazina kuweka mipango mizuri ya kiuhasibu ili kuhakikisha ukusanyaji, utunzaji na upelekaji wa fedha benki” pia Agizo linamtaka mweka hazina “pale inapowezakana kuhakikisha kuwa fedha zote zikusanywe kabla au wakati wa kupata huduma”.

Kushindwa kukusanya fedha za wadaiwa kwa wakati ni ishara ya udhaifu katika kusimamia madeni na ukosefu wa sera madhubuti juu madeni.

Halmashauri zinashauriwa kuongeza juhudu katika usimamizi wa rasilimali ikiwemo kuanzisha kanuni na taratibu na kuweka kipaumbele katika usimamizi wa ukusanyaji wa madeni bila kuathiri utoaji wa huduma.

#### **3.8.4 Wadai wasiolipwa Sh.52,041,114,397**


Ulipaji wa madeni kwa wakati ni jambo muhimu na linaleta imani kati ya Halmashauri na wasambazaji wa vifaa na huduma na kuongeza hali ya kuaminiwa na jamii inayohudumia Halmashauri.

Hata hivyo, ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2010 ulibaini kuwa Halmashauri 113 zilikuwa na wadai wasiolipwa wenye jumla ya Sh.52,041,114,397 ikiwa ni ongezeko la Sh.729,527,635 ikilinganishwa na Sh.51,311,586,762 kwa mwaka uliopita.

Halmashauri zilizoripoti kiasi kikubwa cha wadai ni Manispaa ya Ilala Sh.5,687,236,970, Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Sh.2,278,790,650 na Halmashauri ya Jiji la Mwanza Sh.2,084,870,291.

Jedwali lifuatalo linaonyesha ulinganisho wa wadai kwa mwaka wa fedha 2008/2009 na 2009/2010:

| Mwaka     | Kiasi (Sh.)    | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|----------------|----------------------|
| 2008/2009 | 51,311,586,762 | 113                  |
| 2009/2010 | 52,041,114,397 | 113                  |



Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kulipa madeni yake haraka yanapofikia wakati wa kulipa na zianzishe udhibiti thabiti, kanuni na taratibu katika kuhakikisha kuwa uongozi wa Halmashauri unawajibika na ahadi unazozitoa. Orodha ya Halmashauri zinazodaiwa imeonyeshwa kwenye **kiambatisho Na. 18.**

### 3.8.5 Mali ambayo haikuhesabiwa na orodha ya kuhesabia mali hazikutolewa

Agizo Na 241 na 242 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaitaka Halmashauri kuhesabu vifaa na mali zake kila mwisho wa mwaka wa fedha. Hata hivyo nilibaini kuwa zoezi hili halikufanyika katika Halmashauri nne (4) kinyume na maagizo hayo. Vile vile Halmashauri tisa (9) ambazo zilidai kufanya zoezi hili, hazikuwasilisha orodha ya kuhesabia mali ili kuthibitisha kuwa zoezi la kuhesabu mali lilifanyika ipasavyo.

Hii inamaanisha kuwa usahihi wa mali zilizoripotiwa kwenye taarifa za fedha hauwezi kuthibitishwa. Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa kuhakikisha kuwa mali za Halmashauri zao zinahesabiwa kila mwisho wa mwaka wa fedha na maafisa wasiopungua watatu wanahudhuria zoezi hilo na kuwa orodha ya kuhesabia mali zinasainiwa na maafisa wote waliohudhuria.

Mchanganuo wa Halmashauri husika na mapungufu yaliyojitekeza ni kama ifuatavyo:

| <b>Na.</b> | <b>Halmashauri</b>                | <b>Halmashauri ambazo hazikuhesabu mali</b> | <b>Halmashauri ambazo hazikuleta orodha ya kuhesabia mali</b> |
|------------|-----------------------------------|---|---|
| 1          | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha   | /   |   |
| 2          | Halmashauri ya Mji wa Kibaha      | /   |   |
| 3          | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe | /   |   |
| 4          | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga | /   |   |
| 5          | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga   |   | /   |
| 6          | Halmashauri ya Wilaya ya Same     |   | /   |
| 7          | Halmashauri ya Wilaya ya Illeje   |   | /   |
| 8          | Halmashauri ya Wilaya ya          |   | /   |

|    | Mbarali                                  |  |   |
|----|--|--|---|
| 9  | Halmashauri<br>Jiji la Mbeya             |  | ✓ |
| 10 | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Sengerema |  | ✓ |
| 11 | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Shinyanga |  | ✓ |
| 12 | Halmashauri<br>ya Mji wa<br>Korogwe      |  | ✓ |
| 13 | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Lushoto   |  | ✓ |

### 3.9 Usimamizi wa mali za kudumu

#### 3.9.1 Mapungufu katika usimamizi wa mali za kudumu

Sehemu hii inatoa kwa muhtasari mapungufu ya Halmashauri mbalimbali katika usimamizi wa mali za kudumu wakati wa uagizaji, usajili, umilikaji, matunzo na mauzo ya mali chakavu.

Halmashauri zinasimamia miundombinu na mali za jamii mbalimbali kama vile barabara, majengo, mali na vifaa ambavyo vinatoa huduma katika jamii. Ni muhimu Halmashauri zikaonyesha kwa vitendo matokeo ya matumizi ya vifaa vya kudumu ili jamii iweze kuona na kunufaika na huduma inayotokana na mali hizo. Katika Halmashauri zilizo nyingi mali za kudumu ndizo zinazochukua sehemu kubwa katika matumizi ya fedha za mwaka na inahitaji mwendelezo wa miradi ya maendeleo kushughulikia ukuaji na mabadiliko ya viwango. Zaidi ya hayo, matumizi mengi ya fedha za maendeleo zinaenda kwenye mali za kudumu.

Mapungufu yaliyojitokeza wakati wa kutathmini usimamizi wa mali za kudumu uliohusisha Halmashauri hamsini (50) ni kama ilivyoainishwa kwenye **kiambatisho Na.19.**

### 3.9.2 Kutweka daftari sahihi la mali za kudumu

Agizo Na 366 na 367 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 linaagiza Halmashauri kutunza daftari la mali za kudumu litakaloonyesha tarehe ya manunuzi, bei ya kununulia, maelezo kuhusu mali zilizouzwa au kununuliwa katika mwaka husika.

Kinyume na maagizo hayo, katika sampuli ya Halmashauri kumi na nane (18), Halmashauri tano (5) hazikuwa na rejista ya mali za kudumu, Halmashauri kumi na tatu (13) zilizosalia ziliwu na rejista ambazo hazikuandaliwa ipasavyo ili kuimarisha udhibiti wa mali za kudumu. Rejista ya mali za kudumu inasaidia kutambua mali za Halmashauri kwa kulinganisha leja kuu, mali halisi pamoja na rejista ili kujua ukamilifu wa taarifa za mali. Zaidi ya hayo baadhi ya rejista za mali za kudumu hazikuboreshwa ili kuonyesha mali zilizonunuliwa na kuuzwa na zilizohamishwa kwa kipindi cha mwaka husika.

Kulingana na hali hiyo hapo juu, inakuwa vigumu kuthibitisha usahihi wa mali za kudumu zinazomilikiwa na Halmashauri. Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kutunza rejista ya mali za kudumu zinazoonesha taarifa zote muhimu za mali za Halmashauri.

Jedwali lifuatalo linaonyesha Halmashauri ambazo aidha hazitunzi rejista za mali au rejista zilizopo hazijaboreshwa ipasavyo:

| Na. | Halmashauri | Hakuna rejista | Rejista ya mali za |
|-----|-------------|----------------|--------------------|
|-----|-------------|----------------|--------------------|

|    |   | <b>ya mali</b> | <b>kudumu haitunzwi<br/>ipasavyo</b> |
|----|---|----------------|--------------------------------------|
| 1  | Halmashauri ya<br>Mji wa Kibaha         |                | ✓                                    |
| 2  | Halmashauri ya<br>Manispaa ya<br>Ilala  | ✓              |                                      |
| 3  | Halmashauri ya<br>Manispaa ya<br>Temeke |                | ✓                                    |
| 4  | Halmashauri ya<br>Wilaya ya Bahi        |                | ✓                                    |
| 5  | Halmashauri ya<br>Wilaya ya<br>Kondoa   |                | ✓                                    |
| 6  | Halmashauri ya<br>Wilaya ya<br>Mpwapwa  |                | ✓                                    |
| 7  | Halmashauri ya<br>Wilaya ya Same        |                | ✓                                    |
| 8  | Halmashauri ya<br>Wilaya<br>Nachingwea  | ✓              |                                      |
| 9  | Halmashauri ya<br>Wilaya ya<br>Ruangwa  | ✓              |                                      |
| 10 | Halmashauri ya<br>Wilaya ya<br>Hanang'  |                | ✓                                    |
| 11 | Halmashauri ya<br>Wilaya ya Kiteto      |                | ✓                                    |
| 12 | Halmashauri ya<br>Wilaya ya<br>Chunya   |                | ✓                                    |
| 13 | Halmashauri ya<br>Wilaya ya Kyela       |                | ✓                                    |
| 14 | Halmashauri ya<br>Wilaya ya             |                | ✓                                    |

|    | Morogoro                         |   |   |
|----|----------------------------------|---|---|
| 15 | Halmashauri ya Wilaya ya Geita   | ✓ |   |
| 16 | Halmashauri ya Wilaya ya Songea  |   | ✓ |
| 17 | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru |   | ✓ |
| 18 | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni | ✓ |   |

### 3.9.3 Mali za kudumu zisizotumika Sh.1,647,221,445

Kwa kipindi cha mwaka wa ukaguzi, Halmashauri sita (6) zilinunua vifaa kwa ajili ya Hospitali na kujenga majengo katika Vijiji na Kata. Hata hivyo wakati wa kutembelea maeneo husika nilibaini kuwa vifaa vilivyonunuliwa pamoja na majengo yaliyojengwa havitumiki. Hii inamaanisha kuwa huduma iliyokusudiwa haikuwafikia wananchi kwa muda uliopangwa na hakuna thamani ya fedha iliyopatikana kupitia miradi hiyo.

Mchanganuo ni kama ifuatavyo:

| Na | Halmashauri                     | Kiasi (Sh.)   | Hoja ya ukaguzi   |
|----|---------------------------------|---------------|---|
| 1  | Halmashauri ya Wilaya ya Karatu | 1,008,931,062 | Ujenzi wa ofisi na ukumbi wa Halmashauri umekamilika lakini jengo halitumiki.                                   |
| 2  | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi   | 312,786,983   | Majengo yaliyokamilika katika Vijiji na kata za Ibugule, Bahi Mkulu hadi wakati wa ukaguzi yalikuwa hayatumiki. |
| 3  | Halmashauri ya Wilaya ya        | 70,000,000    | Halmashauri ilinunua mashine moja ya nusu   |

|  |        |  |
|--|--------|--|
|  | Kasulu | kaputi na chombo cha kuchunguzia wagonjwa mwezi Juni, 2010 kwa ajili ya hospitali ya Wilaya lakini havitumiki. |
|--|--------|--|

|              |                                   |                      |  |
|--------------|-----------------------------------|----------------------|--|
|              | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma   | 30,258,000           | Nyumba moja ya wafanyakazi iliyojengwa katika shule ya sekondari ya Mkigo imeisha lakini haitumiki.  |
| 4            | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali  | 23,865,000           | Halmashauri ilinunua mashine ya kufulia na kukaushia nguo kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya lakini hadi ukaguzi unafanyika mwezi Novemba 2010 mashine hizo zilikuwa hazijafungwa.   |
| 5            | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara | 3,000,000            | Mashine za viyoyozi zilizonunuliwa na Halmashauri hazijafungwa.  |
| 6            | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke | 198,380,400          | (i) Kituo cha mabasi cha Temeke kilichojengwa tangu mwaka 2008 hakitumiki.<br>(ii) Mashine za kufulia na kifisha vijidudu zilizotolewa na Serikali ya Korea tangu mwaka 2007 hazitumiki na hazikuonyeshwa kwenye vitabu vya Halmashauri. |
| <b>Jumla</b> |                                   | <b>1,647,221,445</b> |  |

### **3.10 Uendeshaji wa Mifuko Maalumu**

#### **3.10.1 Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo**

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 kinaleza kuwa, kila mwaka wa fedha, Serikali itatoa mgawo wa fedha kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa kila jimbo na fedha hizo zitaonyeshwa kwenye makisio ya kila mwaka wa fedha. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kwenye Halmashauri 29 ulibaini kuwa Halmashauri 25 zilikuwa na bakaa la fedha hadi tarehe 30 Juni 2010 kutokana na Hazina kuchelewa kutoa fedha hizo kama ifuatavyo:

| Na  | Halmashauri                       | Tarehe ya Kutolewa fedha | Kiasi kilicho-pokelewa | Kiasi kilichotumika | Kiasi kilichobaki/kilichotumika zaidi |
|-----|-----------------------------------|--------------------------|------------------------|---------------------|---------------------------------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo   |                          | 26,269,000             | 24,852,000          | 1,417,000                             |
| 2.  | Halmashauri ya Mji wa Njombe      | Juni 2010                | 19,000,000             |                     | 19,000,000                            |
| 3.  | Halmashauri ya Wilaya ya Misseri  | Juni 2010                | 45,382,000             | 24,454,000          | 20,928,000                            |
| 4.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha   | 11/5/2010 na 21/6/2010   | 27,762,000             |                     | 27,762,000                            |
| 5.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero  | Juni 2010                | 28,406,000             |                     | 28,406,000                            |
| 6.  | Halmashauri ya Wilaya ya Siba     | Juni 2010                | 30,334,000             |                     | 30,334,000                            |
| 7.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga   | Mei na Juni 2010         | 33,576,000             |                     | 33,576,000                            |
| 8.  | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi  | Mei na Juni 2010         | 34,958,000             |                     | 34,958,000                            |
| 9.  | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | Mei na Juni 2010         | 36,130,000             |                     | 36,130,000                            |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi  | Mei na Juni 2010         | 40,155,000             | 1,319,400           | 38,835,600                            |
| 11. | Halmashauri ya Jiji la Mwanza     | Mei na Juni 2010         | 45,470,335             |                     | 45,470,335                            |
| 12. | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | Mei na Juni 2010         | 46,222,000             |                     | 46,222,000                            |
| 13. | Halmashauri ya                    | Mei na Juni              | 47,090,000             |                     | 47,090,000                            |

|              | Wilaya ya Meru                        | 2010                   |                      |                   |                      |
|--------------|---------------------------------------|------------------------|----------------------|-------------------|----------------------|
| 14.          | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa       | 6/5/2010 na 16/6/2010  | 47,446,225           |                   | 47,446,225           |
| 15.          | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega        | Mei na Juni 2010       | 51,000,000           |                   | 51,000,000           |
| 16.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi        | Mei na Juni 2010       | 55,962,999           | 3,426,800         | 52,536,199           |
| 17.          | Halmashauri ya Wilaya ya Dodoma       | Juni 2010              | 67,838,000           |                   | 67,838,000           |
| 18.          | Halmashauri ya Manispaa ya Musoma     | 11/5 na 24/6/2010      | 69,918,000           |                   | 69,918,000           |
| 19.          | Halmashauri ya Wilaya ya Hai          | Mei na Juni 2010       | 71,174,000           |                   | 71,174,000           |
| 20.          | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru      | Mei na Juni 2010       | 73,686,000           |                   | 73,686,000           |
| 21.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa      | Mei na Juni 2010       | 75,576,000           |                   | 75,576,000           |
| 22.          | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe       | 19/5/2010 na 22/6/2010 | 80,533,000           |                   | 80,533,000           |
| 23.          | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga       | Mei na Juni 2010       | 85,148,000           |                   | 85,148,000           |
| 24.          | Halmashauri ya Wilaya ya Maswa        | Mei na Juni 2010       | 90,101,000           |                   | 90,101,000           |
| 25.          | Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga | Mei na Juni 2010       | 99,396,000           | 2,067,500         | 97,328,500           |
| <b>Jumla</b> |                                       |                        | <b>1,328,533,559</b> | <b>56,119,700</b> | <b>1,272,413,859</b> |

Zaidi ya hayo, kifungu cha 7(3) cha Sheria ya mfuko wa maendeleo ya Jimbo ya mwaka 2009 kinataka Halmashauri kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana za Serikali za Mitaa kumbukumbu za fedha zilizopokelewa na Kamati za Maendeleo ya Jimbo na matumizi ya fedha hizo ili kupata picha halisi ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya maendeleo ya majimbo.

Kinyume na kifungu hicho, hakuna Halmashauri hata moja kati ya hizo hapo juu ilioandaa taarifa ya utekelezaji wa miradi iliyofadhiliwa na mfuko huo na hivyo hazikuwasilishwa OWM-TAMISEMI.

### 3.10.2 Michango ya 20% kwenye Vijiji na Kata

Kifungu cha 9 (e) cha Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Na.9 ya 1982 inaeleza kuwa mapato ya Vijiji na Kata yatajumuisha mapato kutoka Serikali Kuu, Wilaya au kutoka

kwa mtu mmoja mmoja au Taasisi kwa njia ya michango. Pia, Agizo Na. 91 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 inaeleza kuwa Mkurugenzi atahakikisha kuwa kila Kijiji ndani ya eneo husika kinapokea fedha moja kwa moja au kwa kupitia Mamlaka husika.

Mwaka 2004 Serikali ilifuta baadhi ya Vyano vyatapato yatokanayo na kodi na kuamua kutoa fidia kwenye Halmashauri kwa kodi hizo zilizofutwa. Halmashauri ziliamuliwa kupeleka 20% ya vyano vilivyofutwa kwenye kata na Vijiji kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Kata na Vijiji na kusaidia shughuli za maendeleo.

Ukaguzi ulibaini kuwa Halmashauri 22 hazikurejesha kwenye Vijiji na Kata Jumla ya Sh.1,244,275,051 ikiwa ni a fidia ya 20% kutokana na vyano vyatapato vilivyofutwa kama inavyooneshwa hapa chini:

| Na | Halmashauri                       | Mchango wa 20% (Sh.) | Kiasi kilichopelek wa (Sh.) | Kiasi kilichobaki (Sh.) |
|----|-----------------------------------|----------------------|-----------------------------|-------------------------|
| 1. | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | 43,436,580           | 12,350,000                  | 31,086,580              |
| 2. | Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba   | 57,469,692           | -                           | 57,469,692              |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa   | 112,367,080          | -                           | 112,367,080             |
| 4. | Halmashauri ya Wilaya ya Longido  | 46,525,600           | 34,690,705                  | 11,834,895              |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga   | 86,192,000           | 84,181,843                  | 2,010,157               |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Meru     | 68,319,464           | 14,558,800                  | 53,760,664              |
| 7. | Halmashauri                       | 85,812,400           | -                           | 85,812,400              |

|              |                                     |                      |                    |                      |
|--------------|-------------------------------------|----------------------|--------------------|----------------------|
|              | ya Wilaya ya Morogoro               |                      |                    |                      |
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga     | 60,340,581           | -                  | 60,340,581           |
| 9.           | Halmashauri ya Manispaa ya Songea   | 62,887,380           | 6,825,000          | 56,062,380           |
| 10.          | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga     | 68,752,180           | 24,400,000         | 44,352,180           |
| 11.          | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru    | 68,752,180           | 24,400,000         | 44,352,180           |
| 12.          | Halmashauri ya Manispaa ya Arusha   | 87,822,300           | 25,726,223         | 62,096,077           |
| 13.          | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto     | 86,010,000           | 23,087,000         | 62,923,000           |
| 14.          | Halmashauri ya Wilaya ya Monduli    | 115,033,679          | -                  | 115,033,679          |
| 15.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa    | 60,792,541           | 17,500,000         | 43,292,541           |
| 16.          | Halmashauri ya Manispaa Kigoma      | 58,956,499           | 41,290,828         | 17,665,671           |
| 17.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi      | 56,498,600           | 14,180,108         | 42,318,492           |
| 18.          | Halmashauri ya Manispaa y ya Dodoma | 95,769,386           | 89,397,190         | 6,372,196            |
| 19.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali    | 81,040,440           | -                  | 81,040,440           |
| 20.          | Halmashauri ya Wilaya ya Same       | 83,760,340           | -                  | 83,760,340           |
| 21.          | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang     | 170,323,826          | -                  | 170,323,826          |
| <b>Jumla</b> |                                     | <b>1,656,862,748</b> | <b>412,587,697</b> | <b>1,244,275,051</b> |

Kutokana na jedwali hapo juu, naweza kuhitimisha kwa kusema kuwa, jamii za Vijijini hazikupata mgawo wao wa fedha za maendeleo na kwa hiyo basi, miradi mingi ya maendeleo haikutekelezwa kama ilivyokusudiwa.

Menejimenti za Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa fedha za maendeleo kwa ajili ya Vijiji na Kata zinapelekwa kwa wakati kama ilivyoagizwa na Serikali.

### **3.10.3 Mfuko wa Afya ya Jamii**

Mfuko wa Afya ya Jamii ulianzishwa mwaka 1997 ikiwa ni mmoja wa mifuko iliyoainishwa na Serikali kwa ajili ya kuhamasisha jamii katika uchangiaji wa huduma za afya Tanzania.

Ukusanyaji na utumiaji wa Fedha katika Mifuko umeelezwa zaidi katika Waraka Na. 2 wa mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao ulielekeza kuwa fedha zitatumika kwa matumizi yaliyopitishwa yakiwemo ununuzi wa madawa, matengenezo madogo madogo ya majengo, mafuta na posho za watumishi kwa ajili ya safari za kwenda kununua madawa.

Katika kipindi hiki cha ukaguzi, nimepitia usimamizi wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika Halmashauri kumi (10) na kubaini kuwa Halmashauri hizo zilikuwa na bakaa ya jumla ya Sh. 383,337,857 ambazo kwa kiasi kikubwa ilisababishwa na aidha Halmashauri nyingi kutofungua akaunti za benki zinazojitegemea kwa ajili ya Mfuko wa Afya pekee au kuchelewa kwa fedha toka Hazina. Pia Halmashauri hizo hazikutengeneza taarifa ya fedha kwa ajili ya Mfuko wa Afya ya Jamii kwa mwaka husika.

Orodha ifuatayo inaonyesha Halmashauri ambazo zilibaki na bakaa wakati wa kufunga mwaka tarehe 30 Juni, 2010:

| <b>Na.</b>   | <b>Halmashauri</b>                    | <b>Bakaa (Sh.)</b> |
|--------------|---------------------------------------|--------------------|
| 1.           | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe       | 18,388,594         |
| 2.           | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo     | 34,206,954         |
| 3.           | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe       | 88,374,000         |
| 4.           | Halmashauri ya Wilaya ya Maswa        | 20,712,500         |
| 5.           | Halmashauri ya Manispaa ya Songea     | 13,709,211         |
| 6.           | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga       | 55,398,903         |
| 7.           | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru      | 25,595,500         |
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa      | 98,048,186         |
| 9.           | Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga | 10,174,246         |
| 10.          | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma     | 18,729,763         |
| <b>Jumla</b> |                                       | <b>383,337,857</b> |

Zaidi ya hayo, kiasi cha Sh.4,748,850 Kilichokusanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kupitia mfuko wa Afya ya Jamii hakikuwasilishwa makao makuu ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa ajili ya nyongeza kutokana na kuchelewa kusainiwa kwa mkataba kati ya Wizara ya Afya na Halmashauri husika. Pia kiasi cha Sh.1,810,700 kilichokusanywa na vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba hakikuwasilishwa kwenye akaunti kuu ya maduhuli ya Halmashauri kwa utunzaji zaidi.

Ninasisitiza kwamba, ni lazima Halmashauri zitengeneze taarifa za hesabu za mfuko na pia zihakikishe kuwa fedha za mfuko zinatumika tu kwa shughuli zilizokusudiwa na ambazo zimeidhinishwa kama ilivyoainishwa katika Waraka na. 2 wa mwaka 1997 uliotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

### 3.10.4 Mfuko wa Wanawake na Vijana

Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu ilianzisha mfuko huu maalumu kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wanawake na vijana kwa kuwapa mikopo midogo midogo katika maeneo wanayoishi.

Ukaguzi uliofanyika katika uendeshaji wa mfuko kwa kuchagua Halmashauri 27 umebaini kuwa, Halmashauri 11 hazikutengeneza hesabu za mwaka kuonyesha hali halisi ya mfuko. Hii ni kinyume na matakwa ya Agizo Na. 84 (iii) la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.

Vile vile Halmashauri hazikuchangia Sh.279,415,551 kwenye mfuko ikiwa ni mchango wa asilimia 10 kutoka kwenye vyanzo vyake na vya ndani na kulikuwa na mikopo isiyorejeshwa na vikundi ya jumla ya Sh.522,297,988. Kutorejeshwa kwa mikopo kwa wakati kunanyima vikundi vingine fursa ya kuchukua mikopo.

Jedwali hapa chini linaonesha mambo yaliyojitokeza katika Mfuko wa Wanawake na Vijana:

| Na. | Halmashauri                       | Mchango wa 10% | Taarifa ya mwaka ya Fedha | Kiasi cha mikopo isiyorejeshwa (Sh.) |
|-----|-----------------------------------|----------------|---------------------------|--------------------------------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa   | 48,004,456     | Haikuandaliwa             | 12,650,000                           |
| 2.  | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | 8,894,000      | Haikuandaliwa             | 10,500,000                           |
| 3.  | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo    | -              | Imeandaliwa               | 17,720,900                           |
| 4.  | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe   | -              | Imeandaliwa               | 26,353,900                           |
| 5.  | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe   | -              | Imeandaliwa               | 9,042,260                            |
| 6.  | Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba   | -              | Imeandaliwa               | 7,863,000                            |
| 7.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi  | -              | Imeandaliwa               | 5,248,300                            |

|              |                                   |                    |               |                    |
|--------------|-----------------------------------|--------------------|---------------|--------------------|
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo   | -                  | Imeandaliwa   | 5,845,600          |
| 9.           | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa   | -                  | Haikuandaliwa | 9,970,000          |
| 10.          | Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba   | -                  | Imeandaliwa   | 23,897,500         |
| 11.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya    | -                  | Haikuandaliwa | 36,268,556         |
| 12.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga   | -                  | Imeandaliwa   | 4,091,500          |
| 13.          | Halmashauri ya Wilaya ya Meru     | -                  | Imeandaliwa   | 6,980,500          |
| 14.          | Halmashauri ya Manispaa ya Moshi  | -                  | Imeandaliwa   | 72,115,868         |
| 15.          | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | 222,517,095        | Haikuandaliwa | 12,448,119         |
| 16.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga   | -                  | Haikuandaliwa | 11,560,000         |
| 17.          | Halmashauri ya Wilaya ya Siha     | -                  | Haikuandaliwa | 8,788,000          |
| 18.          | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga   | -                  | Haikuandaliwa | 5,990,300          |
| 19.          | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo   | -                  | Imeandaliwa   | 92,871,181         |
| 20.          | Halmashauri ya Wilaya ya Monduli  |                    | Imeandaliwa   | 4,306,910          |
| 21.          | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma | -                  | Imeandaliwa   | 12,481,000         |
| 22.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi    | -                  | Imeandaliwa   | 68,878,789         |
| 23.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi  | -                  | Imeandaliwa   | 4,464,684          |
| 24.          | Halmashauri ya Wilaya ya Handeni  | -                  | Haikuandaliwa | 5,079,000          |
| 25.          | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma | -                  | Haikuandaliwa | 9,985,500          |
| 26.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali  | -                  | Haikuandaliwa | 28,876,621         |
| 27.          | Halmashauri ya Wilaya ya Same     | -                  | Imeandaliwa   | 8,020,000          |
| <b>Jumla</b> |                                   | <b>279,415,551</b> |               | <b>522,297,988</b> |

Halmashauri zinatakiwa kutengeneza michanganuo ya fedha ya mfuko ikionyesha matumizi na mapato tangu mifuko ianzishwe kwa fedha zilizochangwa na Serikali Kuu, Halmashauri na wafadhili wengine wakiwemo taasisi zisizokuwa za Kiserikali.

Vilevile, michanganuo ni lazima ionyeshe kiasi kilichopo, kiasi kinachodaiwa; jumla ya riba iliyopokelewa na michango inayodaiwa kwenye mfuko.

Zaidi ya hapo, menejimenti iandae mikakati ya kurejeshwa kwa mikopo yote inayodaiwa ili kuwawezesha watu wengine kukopa na kuboresha hali zao za maisha.

#### **3.10.4 Hesabu za mwaka za Vijiji na kata hazikuandaliwa na fedha zilizo pelekwa kwenye Vijiji/ Kata hazikuingizwa kwenye vitabu**

Katika ukaguzi imebainika kuwa Vijiji/ kata katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi hazikutengeneza hesabu za mwaka 2009/2010 kinyume na Agizo Na.91 na 92 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997.

Vilevile, jumla ya Sh.52,920,298 zilibainika kuhamishwa kutoka Akaunti ya Mfuko Mkuu kwenda kwenye Vijiji na Kata ikiwa ni ruzuku ya maendeleo kwa mwaka 2009/2010 lakini hazikukaguliwa.

Kutokuwa na kumbukumbu za mapokezi na matumizi ya fedha zilizopelekwa kwenye Vijiji/Kata haiwezi kuthibitika kama fedha hizo zimetumika kama zilivyopangwa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuandaa mikakati ya kuhakikisha kuwa Vijiji/kata zinaandaa hesabu za mwaka na kukaguliwa.

**3.11 Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita kwa ripoti ya jumla na ripoti ya kila Halmashauri husika**

**3.11.1Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Halmashauri kwa ripoti ya jumla**

Kifungu cha 40 (4) cha Sheria ya Ukaguzi, Na. 11 ya mwaka 2008 kinanitaka kuunganisha katika ripoti ya mwaka utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita. Sehemu hii inahusu kiwango cha utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

Kulingana na Kifungu cha 40(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Na. 11 ya 2008 Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) ndiye anatakiwa kupokea majibu kutoka kwa Maafisa Masuuli na baada ya hapo PMG anatakiwa kuwasilisha kwa Waziri ambaye atawasilisha ripoti kwenye Bunge. Vile vile Mlipaji Mkuu anawajibika kupeleka nakala ya taarifa jumuifu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyomo katika ripoti hiyo kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Majibu ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa hesabu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2009, niliyapokea kutoka kwa Mlipaji Mkuu tarehe 27 Julai 2010 na pia nilipokea nakala ya mpango kazi kutoka TAMISEMI kwenda kwa makatibu Tawala wa Mikoa.

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa juhudzi zilizofanywa na Mlipaji Mkuu, Katibu Mkuu TAMISEMI, na Maafisa Masuuli wote kwa kutoa majibu ya ripoti na hatua zitakazochukuliwa katika utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti yangu, japokuwa kulikuwa na mapendekezo ya ukaguzi ambayo hayakuweza kushughulikiwa miongoni mwa majibu yote yaliyotolewa kama yafuatayo:

**(i) Makusanyo ya Maduhuli yaliyofanywa na Mawakala kwa niaba ya Halmashauri kwa mwaka 2007/2008 na 2009/2010**

Ukaguzi umebaini mapungufu ya ukusanyaji wa maduhuli kutoka kwa mawakala. Eneo hili la makusanyo limegubikwa na mikataba isiyokuwa na manufaa kwa Halmashauri ambayo huwanufaisha zaidi mawakala.

Eneo hili limeonyesha mapungufu ya kimikataba ambalo limeziathili Halmashauri nyingi. Uwezo wa Halmashauri wa kifedha kuhudumia shughuli za kila siku kutoka kwenye vyanzo vyake nya mapato yake ya ndani unakwamishwa na mapungufu ya udhibiti wa ndani juu ya ukusanyaji wa maduhuli.

Halmashauri zinashauriwa kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuingia mikataba na mawakala wa kukusanya maduhuli. Mikataba yote ni lazima ihakikiwe na Wanasheria wenyewe sifa kabla Halmashauri haijasaini makubaliano hayo. Kwa mipango kazi iliopelekwa kwa Makatibu Tawala wa mikoa, OWM-TAMISEMI ilichukua jukumu la kutoa miongozo kuhusiana na ubinafishaji wa ukusanyaji wa maduhuli katika ngazi ya Halmashauri. Utekelezaji wa suala hili bado unasubiliwa.

**(ii) 2008/09 - Uhuishaji wa Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa**

Nimekwisha kutoa taarifa kuhusiana na kuhuisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya) Na.7 ya mwaka 1982, Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Miji) Na.8 ya mwaka 1982. Sheria hizi zinafafanuliwa zaidi pia na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 na mwongozo wa uandaaji wa hesabu za Serikali za Mitaa wa mwaka 1993.

Napendekeza kuwa, ili kuwa na maboresho endelevu, hasa katika mifumo iliyoridhiwa kwa kuzingatia mifumo iliyio bora kwingineko duniani kama kuridhia kutumika Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs) na uanzishwaji wa kamati za ukaguzi za hesabu, sheria na kanuni zilizopo zinapaswa kuhuishwa ili kuendana na mifumo mipyä iliyoridhiwa. Utekelezaji wa maboresho hayo bado unashubiriwa.

**(iii) 2008/09 - Utumiaji na Utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSASs)**

Ili kuwa na uhakika wa matumizi ya Viwango vya Kimataifa ambavyo vinatumwiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuimarisha udhibiti wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, napendekeza kwa Serikali kuwa na Ofisi ambayo itafanyakazi ya Mlipaji Mkuu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi hii itakuwa sawa na Mlipaji Mkuu wa Serikali Kuu. Badala yake ingekuwa ni vyema kuongeza wigo wa kazi za Mlipaji Mkuu wa Serikali wa sasa hadi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Majibu au taarifa za utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi yanashubiriwa.

**(iv) 2008/09 - Viongozi wa juu wa Halmashauri kuajiriwa kwa mkataba**

Kutokana na ukweli kwamba, udhibiti wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa hauimariki kama inavyotarajiwa. Nashauri kuwa na umuhimu wa kuimarisha utaratibu wa ajira katika kufanikisha mpango wa ugatuaji wa madaraka kwa wananchi (D by D). Pendelekezo hili limetokana na ukweli kwamba, ajira katika uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa unafuata mfumo wa masharti ya kudumu na malipo ya izeeni ambao umeshindwa kuboresha udhibiti wa fedha.

Hivyo, napendekeza ili kuweza kuimarisha uongozi katika ngazi za Halmashauri mamlaka za uteuzi zinashauriwa kuwa na mikakati ya kubadilisha masharti ya ajira katika ngazi za juu za Halmashauri kutoka masharti ya kudumu na malipo ya izeeni kwenda kuwa ya masharti ya mikataba.

### **3.11.2 Ufutiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka iliyopita katika Ripoti ya kila Halmashauri**

Sehemu hii inaeleza kwa ufupi mapendekezo ya ukaguzi uliopita ambayo hayajatekelezwa au yametekelezwa sehemu na pia nimeona vyema kujumuisha mambo ambayo yameweza kuthamanishwa katika ukaguzi wa kawaida na ufutiliaji wa mambo kutoka katika kaguzi maalumu zilizofanywa mwaka 2008/2009 katika baadhi ya Halmashauri.

Kwa mwaka wa ukaguzi, mapendekezo mbalimbali yaliyotokana na hoja zilizotolewa na wakaguzi kwa mambo ya msingi kwa miaka ya nyuma. Nilibaini kuwa Halmashauri 5 ambazo ni Halmashauri ya Manispaa Iringa, Halmashauri ya Mji wa Njombe, Halmashauri ya Wilaya Kilolo, Halmashauri ya Wilaya Chato na Halmashauri ya Manispaa Songea zilitokeleza mapendekezo ya ukaguzi. Ila, Halmashauri 129 zilikuwa hazijatekeleza mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma yenye jumla ya Sh.122,128,377,615 katika kiasi hicho, Halmashauri za Kilwa ilikuwa na mapendekezo yasiyotekeliza ya kiasi cha Sh.8,992,407,355, ikifuatiwa na Same Sh.8,176,961,278, Kongwa Sh.7,242,561,049 na Manyoni Sh.6,097,936,644.

Hulka au tabia ya kutotekeliza mapendekezo ya ukaguzi inapelekea kujirudia kwa hoja ambazo zimetolewa na wakaguzi kwa miaka ya nyuma. Hii inaashiria kuwepo kwa mapungufu katika uwajibikaji kwa uongozi wa Halmashauri husika.

Nimekuwa nikitoa hoja na mapendekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa malengo ya kurekebisha mambo yaliyojitekeza wakati wa ukaguzi kwa ajili ya kuzishughulikia mapema ili kuimarisha udhibiti wa rasilimali za Halmashauri.

**Ulinganifu wa mambo yaliyojitekeza kwa miaka mitatu iliyopita mfululizo (2007/2008; 2008/2009 na 2009/2010) umeoneshwa katika jedwali hapa chini:**

| Mwaka     | Kiasi cha masuala yasiyotekelawa (Sh.) | Idadi ya Halmashauri |
|-----------|--|----------------------|
| 2007/2008 | 32, 903,395,306                        | 112                  |
| 2008/2009 | 53,463,558,647                         | 126                  |
| 2009/2010 | 122,128,377,615                        | 129                  |

Mwelekeo wa masuala yasiyotekelawa ni kama inavyooneshwa katika chati mihimili ifuatayo:



Chati Mihimili hapo juu inaonyesha ongezeko la mapendekezo yasiyotekelawa la Sh.53,463,558,647 kutoka ukaguzi uliopita wa mwaka 2008/2009 ukihusisha Halmashauri 126. Katika ukaguzi wa mwaka 2009/2010 idadi ya Halmashauri zilizokuwa na mapendekezo yasiyotekelawa iliongezeka kutoka Halmashauri 126 hadi

129 yakiwa na jumla ya Sh.122,128,377,615 na kufanya ongezeko la Sh.68,664,818,968 kama ilivyoonyeshwa hapo juu. Vilevile hii inajumuisha mambo ya miaka ya nyuma kutoka katika kaguzi maalumu zilizofanyika mwaka 2008/2009. Mwelekeo huo unaashiria kuwa uongozi wa Halmashauri haukuchukua hatua madhubuti kushughulikia mapendelekezo hayo. **Kiambatanisho 20** kinaonyesha mambo yasiyoteklezwa katika kaguzi za miaka ya nyuma.

## SURA YA NNE

### 4.0 KUPITIA MIKATABA NA UZINGATIAJI WA TARATIBU ZA MANUNUZI KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 inaelezea manunuzi kama mchakato unaohusisha kununua, kupanga, kukodi au kupata mali au kazi za ujenzi au huduma kwa taasisi inayonunua kwa kutumia fedha za umma na unahusisha majukumu yote yanayohusiana na kupata vifaa, shughuli za ujenzi au huduma ikijumuisha maelezo ya mahitaji, kuchagua na kuitisha wazabuni, kuandaa na hatimaye kutoa mikataba. Ikizingatiwa kwamba sehemu kubwa ya matumizi ya Serikali hutumika katika manunuzi ya vifaa na huduma, kuna haja ya kuimarisha nidhamu ya matumizi na kuwa na uwazi katika mchakato wa manunuzi ili kupata kiwango cha juu cha thamani ya fedha katika manunuzi yote yanayofanywa na Serikali.

#### 4.1 Ufuataji wa Kanuni za manunuzi

Kifungu 44(2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni Na. 31 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma (Vifaa, ujenzi na huduma zisizo za ushauri, kuuza mali za umma kwa Zabuni) za mwaka 2005, zinanitaka kueleza katika ripoti yangu kama taasisi inayokaguliwa imefuata matakwa ya Sheria hii na kanuni zake. Kuhusu wajibu wa taasisi zinazofanya manunuzi ikijumuisha Halmashauri, ninachoweza kusema kwa ujumla ni kwamba, kiwango cha ufuataji wa Sheria za manunuzi ya Umma na Kanuni zake kutohana na Halmashauri zilizokaguliwa bado si cha kuridhisha kulingana na matakwa halisi ya Sheria hii.

#### 4.2 Ufanisi wa Utendaji kazi wa Kitengo cha Usimamizi Manunuzi (PMU)

Kifungu 34 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, na Kanuni 22 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa za mwaka 2007 zinatamka kwamba, kila taasisi inayofanya manunuzi, inatakiwa kuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi chenye wataalamu wa kutosha.

Kitengo cha Usimamizi Manunuzi kitaundwa na wataalamu wa manunuzi pamoja na wataalamu wa fani mbalimbali na wakisaidiwa na watumishi wa kutosha.

Tathmini ya utendaji wa kitengo hiki katika Halmashauri mbalimbali imeonesha kuongezeka kwa ufanisi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika ripoti yangu ya mwaka uliopita. Kwa mwaka huu, Halmashauri 29 zimeonekana kuwa na Vitengo vya Usimamizi wa Manunuzi visivyo fanya kazi ipasavyo, ikilinganishwa na Halmashauri 11 zilizotolewa taarifa mwaka uliopita.

Mapungufu yaliyobainika yanajumuisha Wazabuni kutoa huduma kabla ya kusaini mikataba na kushindwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kila mwezi za manunuzi kwenye Bodi ya Zabuni ya Manunuzi kulingana na kifungu cha 35 (o) na (q) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004, na Kanuni 23 ya Kanuni za Bodi ya Zabuni ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2007.

Muhtasari wa mapungufu yaliyojitokeza ni kama inavyonekana katika jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri                         | Matokeo ya Ukaguzi  | Kiasi (Sh.) |
|-----|-------------------------------------|---|-------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Arusha     | Malipo ya Manunuzi kwa bidhaa na huduma yalifanyika kwa fedha tasilimu badala ya hundi kutokana na udhaifu uliopo katika kitengo cha manunuzi   | 12,678,650  |
| 2.  | Halmashauri ya Jiji la Dares Salaam | Malipo kwa wasambazaji wa bidhaa na huduma yalifanyika kwa kutumia masurufu kwa wafanyakzi kinyume na Kanuni 68(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2005 ambayo inasisitiza ushindani ili kupunguza gharama | 59,850,000  |

|    |                                   |   |            |
|----|-----------------------------------|---|------------|
| 3. | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | Halmashauri ilinunua bidhaa zenyе thamani ya Sh.21,492,500 ambazo hazikuwemo kwenye mpango wa manunuzi kinyume na Kifungu 45 cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004.  | 21,492,500 |
| 4. | Halmashauri ya Jiji la Mbeya      | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia huduma na bidhaa kinyume Agizo Na.128 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) na Kifungu Na.44 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004. | 3,000,000  |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Babati   | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia vifaa kinyume Agizo Na.250 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997)   | 12,119,000 |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega    | Ripoti za manunuzi za kila mwezi hazikuandaliwa na nakala kupelekwa kwenye ofisi za ukaguzi ndani ya siku thelathini kinyume na Kanuni 116 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005.                                     | -          |
| 7. | Halmashauri ya Wilaya ya Longido  | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia matairi kinyume Agizo Na.128 Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997) na Kifungu Na.44 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004.             | 3,800,000  |

|     |  |  |           |
|-----|--|--|-----------|
| 8.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga          | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia huduma na bidhaa kinyume Kanuni 68 ya Kanuni za Manunuvi ya Umma, 2005   | 3,800,000 |
| 9.  | Halmashauri ya Wilaya ya Liwale          | Mkuu wa Kitengo cha Manunuvi anaripoti kwa Mweka Hazina badala ya Afisa Masuuli, pia Kitengo hakitayarishi taarifa za kila mwezi za manunuvi.  | -         |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi           | Kinyume na Kanuni Na. 116 ya Manunuvi ya Umma, 2005 nakala za mikataba hazikupelekwa katika ofisi ya ukaguzi ndani ya siku thelathini baada ya mikataba kusainiwa.   | -         |
| 11. | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto          | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia shajala kinyume Kanuni Na. 68 ya Kanuni ya Manunuvi ya Umma, 2005  | 7,300,000 |
| 12. | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/ Ujiji | Halmashauri haikutumia nukuu ya bei na utaratibu wa ushindani katika manunuvi ya bidhaa na huduma, kinyume na Kifungu 63 (1) ya Sheria ya Manunuvi, 2004 na Kanuni 83 (3) ya Kanuni ya Manunuvi ya Umma, 2005. | -         |
| 13. | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi           | Masurufu yaliyolipwa kwa wafanyakazi yalitumika kununulia huduma na bidhaa kinyume Agizo 128 Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa  | 1,206,550 |

|     |                                   |   |           |
|-----|-----------------------------------|---|-----------|
|     |                                   | (1997) na kifungu Na. 44 cha sheria ya Manunuzi ya Umma, 2004.  |           |
| 14. | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | Masurufu yalilipwa kwa watumishi kwa ajili ya ukarabati wa jengo la katika kituo cha Afya Dutumi kinyume na kifungu Na. 59 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21, 2004. | 3,370,000 |
| 15. | Halmashauri ya Wilaya Mwanga      | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na kunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kinyume na Kanuni Na.116 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005.                | -         |
| 16. | Halmashauri ya Wilaya Chunya      | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na kunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kinyume na Kanuni Na.116 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005.                | -         |
| 17. | Halmashauri ya Wilaya ya Moshi    | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na nakala za mikataba za mikataba iliyosainiwa haikunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.        | -         |
| 18. | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa  | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na Mikataba iliyosainiwa haikunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.                              | -         |
| 19. | Halmashauri ya Wilaya ya Tabora   | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na Mikataba iliyosainiwa  | -         |

|     |                                     |  |           |
|-----|-------------------------------------|--|-----------|
|     |                                     | haikunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.  |           |
| 20. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero  | Taarifa ya utekelezaji wa miradi ya mwaka haikuandaliwa, hali ambayo imesababisha kutofanyika kwa tathmini ya udhibiti wa manunuzi   | -         |
| 21. | Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga | Ukaguzi umebaini kuwa Kitengo cha Manunuzi (PMU) kimeundwa na watumishi kutoka katika vitengo vingine ambao hawawezi kufanya kazi wakati wote.                                   | -         |
| 22. | Halmashauri ya Wilaya ya Karatu     | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na Mikataba iliyosainiwa haikunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  | -         |
| 23. | Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe     | Ripoti za kila mwezi za manunuzi hazikuandaliwa na Mikataba iliyosainiwa haikunakiliwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali  | -         |
| 24. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa     | Malipo ya Manunuzi kwa bidhaa na huduma yalifanyika kwa fedha taslimu badala ya hundi katika Halmashauri ya Wilaya Kilosa kutokana na udhaifu uliopo katika kitengo cha manunuzi | 6,676,850 |
| 25. | Halmashauri ya Wilaya ya Siha       | Dondoo za maamuzi ya Vikao vya zabuni hazikunakiliwa kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za   | -         |

|              |                                  |   |                    |
|--------------|----------------------------------|---|--------------------|
|              |                                  | serikali kinyume na kanuni Na. 96(2) ya Kanuni za Manunuzi, 2005. |                    |
| 26.          | Halmashauri ya Wilaya ya Singida | Mzabuni alitoa huduma kabla ya mkataba kusainiwa                  | 43,671,001         |
| <b>Jumla</b> |                                  |   | <b>182,953,551</b> |

Ukaguzi umebaini kuwa, sababu ya kutofuata Sheria na Kanuni za Manunuzi ni mapungufu ya uanzishwaji wa vitengo vya manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Katika baadhi ya maeneo, Vitengo vya Manunuzi havina watumishi wa kutosha na waliopo hawana elimu na mafunzo ya kutosha.

#### **4.3 Mapitio ya Mikataba na Uzingatiaji wa Taratibu za Ununuzi katika Halmashauri**

Sura hii inahusika na tathimini ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya mwaka 2004 pamoja na Kanuni husika, taratibu za ununuzi ya bidhaa, kazi za ujenzi na utoaji wa huduma katika Halmashauri pamoja na mapungufu yanayohusiana na ununuzi yaliyoonekana wakati wa ukaguzi wa hesabu za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. Tathmini yangu kuhusiana na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni umegundua yafuatayo:

##### **4.3.1 Vifaa ambavyo Havikuingizwa Katika Leja Sh.577,578,107**

Agizo Na.207 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997 inaagiza kwamba, kumbukumbu za mapokezi, vifaa vilivytoka stoo na bakaa ya vifaa katika stoo viandikwe katika kurasa tofauti za leja ya stoo ikionesha taarifa zote za manunuzi kama; tarehe ya manunuzi, kiasi na bei ya kila bidhaa iliyonunuliwa, risiti ya kutolea mali, hati ya kupokelea vifaa, kiasi kilichotolewa, tarehe ya kutoa ghalani na kiasi kilichobaki ghalani.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuhusu udhibiti wa bidhaa ghalani umeonyesha kuwa Halmashauri 24 hazikufuata matakwa ya Sheria na Kanuni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.21.**

**4.3.2 Vifaa Viliviyolipiwa Lakini Havikupokelewa Sh.240,494,600**  
 Kanuni 122(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2005, ambazo zinaitaka kila taasisi inayofanya manunuzi kupata taarifa ya mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa kulingana na mkataba ili kuwezesha taasisi husika kufanya malipo kwa mzabuni. Kinyume na kanuni hiyo, vifaa vyenye thamani ya Sh.240,494,600 viliagizwa na kulipiwa lakini vilionekana kupokelewa pungufu au kutopokelewa kabisa na Halmashauri husika kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo.

| Na.          | Halmashauri                       | Kiasi (Sh.)        |
|--------------|-----------------------------------|--------------------|
| 1            | Halmashauri ya Manispaa ya Iringa | 11,066,000         |
| 2            | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto  | 31,796,600         |
| 3            | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo   | 92,300,000         |
| 5            | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo  | 58,077,000         |
| 6            | Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga | 16,849,000         |
| 7            | Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni  | 7,200,000          |
| 8            | Halmashauri ya Wilaya ya Tarime   | 23,206,000         |
| <b>Jumla</b> |                                   | <b>240,494,600</b> |

**4.3.3 Manunuzi Yaliyofanywa bila Ushindani wa bei  
Sh.570,589,420**

Uhakiki wa kumbukumbu za manunuzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 ulibaini kuwa kiasi cha Sh. 570,589,420 kililipwa na Halmashauri 26 kwa ajili ya kununua vifaa, kazi za ujenzi na huduma mbalimbali bila kufuata utaratibu wa ushindani wa bei kinyume na Kanuni 63 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2005.

Kiasi hiki ni ongezeko la Sh.402,062,833 ikilinganishwa na Sh.168,526,587 zilizoripotiwa mwaka uliopita ambapo ni Halmashauri kumi na sita (16) tu ndizo zilifanya malipo ya aina hii. Kutokufuata Kanuni za Manunuzi zilizowekwa kunaleta wasiwasi kama kweli thamani ya fedha ilipatikana katika manunuzi haya.

Jedwali hapa chini linaonesha kiasi kilicholipwa bila ushindani kwa kila Halmashauri.

| <b>Na.</b>   | <b>Halmashauri</b>                | <b>Kiasi (Sh.)</b> |
|--------------|-----------------------------------|--------------------|
| 1.           | Halmashauri ya Manispaa ya Songea | 12,848,600         |
| 2.           | Halmashauri ya Wilaya ya Babati   | 6,572,000          |
| 3.           | Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino | 60,929,650         |
| 4.           | Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe  | 11,171,450         |
| 5.           | Halmashauri ya Wilaya ya Chato    | 27,952,860         |
| 6.           | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto  | 44,499,600         |
| 7.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya    | 11,490,000         |
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu    | 15,829,700         |
| 9.           | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo   | 2,382,000          |
| 10.          | Halmashuri ya Manispaa ya Arusha  | 12,484,800         |
| 11.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi  | 6,400,000          |
| 12.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi    | 1,206,550          |
| 13.          | Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba | 14,109,446         |
| 14.          | Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa  | 27,059,400         |
| 15.          | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi     | 8,884,000          |
| 16.          | Halmashauri ya Wilaya ya Iringa   | 6,122,430          |
| 17.          | Halmashauri ya Wilaya ya Tabora   | 10,610,000         |
| 18.          | Halmashauri ya Wilaya ya Karatu   | 7,372,200          |
| 19.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero  | 19,850,910         |
| 20.          | Halmashauri ya Wilaya ya Lindi    | 52, 029,840        |
| 21.          | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma | 22, 667,270        |
| 22.          | Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi | 1,419,329          |
| 23.          | Halmashauri ya Wilaya ya Hanang   | 13,250,000         |
| 24.          | Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo | 7,973,403          |
| 25.          | Halmashauri ya Jiji la Mwanza     | 161,630,582        |
| 26.          | Halmashauri ya Wilaya ya Makete   | 3,843,400          |
| <b>Jumla</b> |                                   | <b>570,589,420</b> |

Uongozi wa Halmashauri husika unatakiwa kuhakikisha kwamba, angalau ankara kifani tatu zipatikane kutoka kwa watoa huduma tofauti kabla ya manunuzi kufanyika ili kuhakikisha kuwa Sheria na Kanuni za Manunuzi zinafuatwa. Inapobidi kununua kutoka kwa mwuzaji mmoja, uthibitisho na uhalali wa kufanya hivyo ni lazima upatikane na utaratibu huo upate kibali kutoka katika Bodi ya Zabuni.

#### **4.3.4 Mapungufu katika kutunza kumbukumbu za mikataba na miradi Sh.1,755,429,901**

Utunzaji bora wa nyaraka za mikataba na miradi ni muhimu kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa nyaraka zinapohitajika na ili kuhakikisha mikataba inafanyika na kufuatiliwa ipasavyo. Utaratibu mzuri wa kuhifadhi nyaraka pia utawezesha Halmashauri husika na wadau wengine kama vile wafadhili na wakaguzi kupata nyaraka na taarifa muhimu kwa urahisi zaidi.

Hata hivyo katika kuitia mikataba mbalimbali katika kipindi cha ukaguzi nilibaini mikataba mingi ambayo haikuwa na nyaraka muhimu katika majalada husika kama vile; makadirio ya gharama za ujenzi, Makadirio ya Mkandarasi, vyeti vya kuruhusu malipo kwa mkandarasi na manunuzi ambayo yalifanywa kinyume na mpango wa manunuzi wa mwaka.

Kiwango cha kufuata sheria na kanuni za manunuzi bado hakiridhishi ingawa kwa upande wa matumizi ya aina hii kwa mwaka wa ukaguzi, kiasi cha Sh.1,755,429,901 kama inavyoonyeshwa katika **kiambatanisho Na. 22** kilitumika ikilinganishwa na kiwango cha Sh.1,930,772,578 kilichoripotiwa katika ukaguzi wa mwaka uliopita.

Uongozi wa Halmashauri husika kwa mara nyingine unakumbushwa kuimarisha taratibu za manunuzi ili kuhakikisha kwamba zinapata thamani ya fedha kwa mali na huduma zinazonunuliwa. Kulingana na Agizo Na.281 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (1997), Halmashauri husika zinatakiwa kuteua watumishi watakaohusika na usimamizi na utekelezaji wa mikataba.

## SURA YA TANO

### 5.0 UKAGUZI WA MIRADI ILIYOPATA FEDHA TOKA KWA WAHISANI

Mamlaka za Serikali za Mitaa, pamoja na kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake pia hupata ruzuku kutoka Serikali Kuu na wafadhiri mbambali kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Wakati wa ukaguzi nilifanya tathmini ya utekelezaji wa miradi ya Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG); Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM). Pia Mamlaka za Serikali za Mitaa hupokea, ruzuku kutoka kwa wafadili wengine katika kuboresha hali ya kijamii kwa kupitia miradi ya Mfuko wa Jamii Tanzania (TASAF), Mfuko wa Afya ya Jamii (HBF), Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo (ASDP) na Mpango wa Sekta ya Maendeleo ya Maji (WSDP). Hata hivyo matokeo ya ukaguzi wa miradi inayofadhiriwa kupitia mifuko hii imetolewa kwenye ripoti za pekee na kupelekwa kwenye uongozi wa Halmashauri husika.

#### 5.1 Mwelekeo wa Fedha

##### 5.1.1 Miradi ya Maendeleo Ya Serikali za Mitaa (LGDG)

###### (a) Fedha ambazo hazikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 Sh.5,739,576,430

Ukaguzi uliofanyika ili kujua ni kiasi cha fedha zilizotumika kwenye Halmashauri ulibaini kuwa kiasi cha Sh.5,739,576,430 kilichopokelewa na Halmashauri 18 zilibaki bila ya kutumika mwishoni mwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 kama inavyoonekana hapa chini:

| Na. | Halmashauri                     | Kiasi (Sh.) |
|-----|---------------------------------|-------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe | 698,315,317 |
| 2.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha | 17,290,615  |

|              |                                    |                      |
|--------------|------------------------------------|----------------------|
| 3.           | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa    | 600,504,026          |
| 4.           | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto   | 971,787,949          |
| 5.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu     | 107,248,632          |
| 6.           | Halmashauri ya Wilaya ya Bunda     | 56,209,962           |
| 7.           | Halmashauri ya Jiji la Mbeya       | 10,000,000           |
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega     | 1,039,971,348        |
| 9.           | Halmashauri ya Wilaya ya Siha      | 148,661,815          |
| 10.          | Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro | 104,843,339          |
| 11.          | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga    | 118,752,291          |
| 12.          | Halmashauri ya Wilaya ya Urambo    | 659,671,000          |
| 14.          | Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe  | 51,426,574           |
| 15.          | Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto    | 590,349,022          |
| 16.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa   | 207,280,787          |
| 17.          | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma  | 134,870,560          |
| 18.          | Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi  | 222,393,193          |
| <b>Jumla</b> |                                    | <b>5,739,576,430</b> |

**(b) Tofauti ya Fedha zilizopokelewa na Mamlaka ya Serikali za mitaa na fedha zilizopelekwa na LGRP kuitia Hazina Sh.3,547,208,794**

Katika ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Halmashauri na taarifa za uwasilishaji wa fedha kwenye Halmashauri zilizopatikana kutoka katika Taarifa za Fedha za LGRP kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 imebainika kuwa Wizara ya Fedha ilipeleka kwenye Halmashauri jumla ya Sh.4,745,078,000 ukilinganisha na kiasi cha Sh.8,292,286,794 zilizopokelewa na Halmashauri na kufanya tofauti ya ya Sh.3,547,208,794 kama inavyoonekana hapa chini:

| Na.          | Halmashauri                      | Kiasi kilichopokelewa na Halmashauri (Sh.) | Kiasi kwenye hesabu za LGRP (Sh.) | Tofauti (Sh.)        |
|--------------|----------------------------------|--|-----------------------------------|----------------------|
| 1.           | Halmashauri ya Wilaya ya Njombe  | 1,942,411,302                              | 508,569,000                       | 1,433,842,302        |
| 2.           | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha  | 238,760,641                                | 163,399,000                       | 75,361,641           |
| 3.           | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa  | 1,820,541,242                              | 975,678,000                       | 844,863,242          |
| 4.           | Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto | 1,289,470,874                              | 654,006,000                       | 635,464,874          |
| 5.           | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu   | 577,191,021                                | 536,428,000                       | 40,763,021           |
| 6.           | Halmashauri ya Wilaya ya Bunda   | 820,853,581                                | 671,767,000                       | 149,086,581          |
| 7.           | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega   | 1,274,863,332                              | 993,754,000                       | 281,109,332          |
| 8.           | Halmashauri ya Wilaya ya Siha    | 328,194,801                                | 241,477,000                       | 86,717,801           |
| <b>Jumla</b> |                                  | <b>8,292,286,794</b>                       | <b>4,745,078,000</b>              | <b>3,547,208,794</b> |

**(c) Fedha za Miradi ya Maendeleo hazikupokelewa na Halmashauri Sh.33,830,000**

Ukaguzi wa nyaraka za kupokelea fedha umebaini kuwa fedha Sh.33,830,000 zilizotumwa kutoka Hazina kwenda

katika Halmashauri ya Liwale kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa CDG hazikupokelewa na Halmashauri.

**(d) Fedha za Ruzuku zilizoazimwa bila Kurudishwa Sh.42,753,019**

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang iliazima kiasi cha Sh.42,753,019 kutoka kwenye mfuko wa LGDG kwa ajili ya matumizi katika akaunti mbalimbali. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa fedha hizo zilikuwa hazijarudishwa kwenye akaunti husika.

Hii inamaanisha kuwa jamii iliyokusudiwa kupata huduma kwa kutumia fedha hizo haijafaidika kutoptana miradi iliyopangwa haikutekelezwa.

Pia, naweza nikatoa hitimisho kwamba, kuna udhaifu wa utunzaji wa kumbukumbu na mawasiliano kati ya Mamlaka za Serikali, Hazina na TAMISEMI.

Wafadhili wanashauriwa kufanya mawasiliano na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa taarifa ya fedha zilizopelekwa pamoja na aina ya shughuli zilizopitishwa kwa utekelezaji.

**5.1.1 Fedha za NMSF ambazo hazikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 Sh.175,049,929**

Katika mwaka wa ukaguzi, Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS) kwa kuitia Wizara ya Fedha ilipeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Mkakati wa Kitaifa wa Kudhibiti Ukimwi (NMSF) 2008-2012 ambao wafadhili wake wakuu ni Serikali ya Marekani kuitia USAID, PEPFAR, wafadhili wengine na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia MTEF.

Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika kuangalia mapato na matumizi ya fedha hizo katika Halmashauri 15

zilizochaguliwa ilibainika kuwa kiasi cha Sh.175,049,929 kilikuwa hakijatumika kufikia tarehe 30 Juni, 2010 kama inavyooneshwa hapa chini.

| Na. | Halmashauri                                 | Kiasi<br>kilichokuwepo<br>Sh. | Kiasi<br>kilichotumika<br>(Sh.) | Kiasi kilichobaki<br>(Sh.) |
|-----|---|-------------------------------|---------------------------------|----------------------------|
| 1.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa             | 100,958,400                   | 66,997,400                      | 33,961,000                 |
| 3.  | Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa             | 102,301,900                   | 101,512,890                     | 789,010                    |
| 4.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya              | 92,387,288                    | 87,923,498                      | 4,463,700                  |
| 5.  | Halmashauri ya Wilaya ya Bunda              | 74,183,000                    | 74,183,000                      | -                          |
| 6.  | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro           | 44,646,000                    | 44,597,742                      | 48,258                     |
| 7.  | Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara             | 45,179,000                    | 26,966,100                      | 18,212,900                 |
| 8   | Halmashauri ya Manispaa ya Singida          | 23,775,000                    | 23,775,000                      | -                          |
| 9   | Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga             | 45,340,000                    | 25,407,000                      | 19,933,000                 |
| 10  | Halmashauri ya Wilaya ya Newala             | 56,134,162                    | 40,595,000                      | 15,539,162                 |
| 11  | Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe            | 87,036,703                    | 51,994,897                      | 35,041,806                 |
| 12  | Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani | 22,695,500                    | 21,594,300                      | 1,101,200                  |
| 13  | Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma           | 27,735,000                    | 14,890,000                      | 12,844,200                 |

|    |                                     |             |             |             |
|----|-------------------------------------|-------------|-------------|-------------|
| 14 | Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga | 201,368,409 | 194,368,730 | 6,998,679   |
| 15 | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma   | 60,117,014  | 34,000,000  | 26,117,014  |
|    | Jumla                               | 983,857,376 | 808,805,557 | 175,049,929 |

Kiwango kikubwa cha salio la fedha inaonesha kuwa kazi za mradi zilizolengwa hazikutekelezwa kama ilivyopangwa na hivyo kuchelewesha utoaji wa huduma kwa jamii.

#### 5.1.2 Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM)

(a) Fedha ambazo hazikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 Sh.787,229,499

Ukaguzi uliofanyika katika baadhi ya Halmashauri kuhusu mwelekeo na utumiaji wa Fedha za MMAM ilibainika kuwa Halmashauri tano (5) zilipokea fedha kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya ambapo hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 zilikuwa zimebakia jumla ya Sh.787,229,499 kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Halmashauri                       | Kiasi kilichopokelewa (Sh.) | Matumizi (Sh.) | Salio (Sh.) |
|-----|-----------------------------------|-----------------------------|----------------|-------------|
| 1   | Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi  | 688,913,172                 | 250,515,615    | 438,397,557 |
| 2   | Halmashauri ya Jiji la Mbeya      | 188,940,286                 | 25,877,880     | 163,062,406 |
| 3   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi    | 402,952,843                 | 261,638,434    | 141,314,409 |
| 4   | Halmashauri ya Manispaa ya Iringa | 117,269,198                 | 73,855,750     | 43,413,448  |
| 5   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya    | 370,540,615                 | 369,498,935.60 | 1,041,679   |
|     | Jumla                             | 1,768,616,114               | 981,386,614.6  | 787,229,499 |

**(b) Fedha kutolewa pungufu ya Makisio  
Sh.555,077,569**

Jumla ya fedha Sh.1,067,574,915 zilikisiwa kwa ajili ya kutekeleza mradi wa MMAM katika Halmashauri tatu(3), kati ya hizo Sh.512,497,346 ambayo ni sawa na 48% zilipokelewa na Halmashauri na kubakia jumla ya Sh.555,077,569 ambazo hazikupokelewa na Halmashauri kutoka Hazina kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini:

| Na. | Halmashauri                      | Makisio<br>(Sh.)     | Mapokezi<br>(Sh.)  | Pungufu<br>(Sh.)   | %    |
|-----|----------------------------------|----------------------|--------------------|--------------------|------|
| 1   | Halmashauri ya Jiji la Mbeya     | 228,000,000          | 188,940,000        | 39,060,000         | 17   |
| 2   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu   | 404,574,915          | 203,425,346        | 201,149,569        | 50.3 |
| 3   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali | 435,000,000          | 120,132,000        | 314,868,000        | 72   |
|     | <b>Jumla</b>                     | <b>1,067,574,915</b> | <b>512,497,346</b> | <b>555,077,569</b> |      |

Hii inaonesha kuwa, sehemu ya kazi zilizopangwa hazikutekelezwa na hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

**5.1.4 Fedha za MMEM ambazo hazikutumika hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 Sh.68,707,324**

Wizara ya fedha ilipeleka fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) wenyewe lengo la kuboresha ubora, kupanua wigo wa elimu kwenye shule na kuongeza mahudhurio ya wanafunzi katika Shule za Msingi.

Ukaguzi uliofanyika kuhusiana na matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa imebainika kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ilikuwa na jumla ya Sh.188,707,324,

kati ya hizo Sh.120,000,000 zilitumika kwa shughuli za maendeleo na kubakia jumla ya Sh.68,707,324 mwishoni mwa mwaka.

Pia kiasi cha Sh.153,380,000 kilitolewa na Wizara ya Fedha kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Musoma kwa ajili ya utekelezaji wa miradi wa MMEM, hata hivyo kiasi hicho cha fedha haijulikani kama kilitumika kama ilivyopangwa kwa kuwa taarifa ya utekelezaji pamoja na mchanganuo wa matumizi havikuletwa kwa ajili ya ukaguzi.

## **5.2 Uhakiki wa utekelezaji wa Miradi**

Uhakiki wa utekelezaji wa miradi katika ngazi ya Halmashauri, umebaini mapungufu katika udhibiti na usimamizi wa miradi hali ambayo inatakiwa kushughulikiwa kwa makini na kwa haraka na Halmashauri husika ili kuongeza utumiaji wa rasilimali zilizokusudiwa.

Nimebaini ya kuwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hawakufuata matakwa ya miradi husika ambayo yanataka kufanyika ukaguzi wa mara kwa mara wa miradi inayotekelawa kwenye Vijiji mbalimbali. Matokeo yake, miradi mingi ilitekelezwa kwa kuchelewa, ilitekelezwa lakini haitumiki na kutekelezwa chini ya kiwango kutokana na usimamizi kutoka kwa uongozi wa Halmashauri usioridhisha. Kwa muhtasari, mapungufu ya miradi iliyochaguliwa yameelezwa katika aya zifuatazo.

### **i) Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi**

Nimebaini kuwa, idadi kubwa ya miradi iliyotembelewa haikukamilika kwa kipindi kilichokubaliwa kwenye mikataba, wakati miradi ya ujenzi katika Halmashauri 18 yenye jumla ya makisio ya Sh.1,532,483,668 haijakamilika kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 23.

Hii imesababishwa na usimamizi mdogo wa miradi na ucheleweshaji wa upelekaji wa fedha katika ngazi ya chini.

**ii) Miradi ya Kijamii ambayo imekamilika na kuwa na huduma zote lakini haitumiki**

Kama ilivyoolezwa hapo awali, ruzuku ya maendeleo imelenga kuboresha hali ya jamii sana sana masikini, kutoka huduma za Vijijini hadi kuimarisha huduma na ukarabati miundombinu iliyochakaa. Matokeo ya ruzuku yanaonekana kwa jamii na miradi iliyotekelizwa katika maeneo hayo. Hata hivyo, ukaguzi wa kutembelea miradi iliyokamilika ulibaini kuwa, miradi katika Halmashauri tisa (9) yenye thamani ya Sh.700,971,208 imekamilika lakini haitumiki kama inavyooneshwa katika jedwali lifuatalo:

| Na. | Jina la Halmashauri             | Jina la mradi                               | Tarehe ya kukamilika | Kiasi (Sh.) |
|-----|---------------------------------|---|----------------------|-------------|
| 1   | Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje Kibaigwa | 30 Septemba 2009     | 105,000,000 |
| 2   | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi   | Ujenzi wa jengo la zahanati kata ya Ibugule | -                    | 66,244,400  |
|     |                                 | Ujenzi wa jengo la zahanati Bahi Mkulu      | -                    | 64,669,749  |
|     |                                 | Ujenzi wa jengo la utawala Bahi Mjini       | -                    | 181,872,834 |
| 3   | Halmashauri ya Wilaya ya Chunya | Ujenzi wa machinjio Makongolosi             | Disemba, 2009        | 6,964,500   |
|     |                                 | Ujenzi wa josho Namkukwe, Mkola na Mapogoro | Julai, 2010          | 16,533,000  |
| 4   | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma | Ujenzi wa Ofisi ya Mtendaji wa Kata Ilagala | -                    | 24,213,950  |
|     |                                 | Ujenzi wodi ya                              | -                    | 60,236,000  |

|              |                                |  |            |                    |
|--------------|--------------------------------|--|------------|--------------------|
|              |                                | Wazazi na Chumba cha kuhifadhi maiti - Uvinza.   |            |                    |
| 5            | Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya | Ujenzi wa madarasa mawili sekondari ya Ihango    | -          | 2,500,000          |
|              |                                | Ujenzi wa Ofisi ya Mtendaji wa Kata Bonde Songwe | -          | 13,270,000         |
|              |                                | Ujenzi wa Ofisi ya Mtendaji wa Kata Iwindi       | -          | 6,594,350          |
|              |                                | Ujenzi wa zahanati Nsambya                       | 15/06/2010 | 18,398,050         |
|              |                                | Ujenzi wa Zahanati Izumbwe                       | 15/06/2010 | 20,588,300         |
|              |                                | Ujenzi wa zahanati Luanda                        | 15/6/2010  | 24,110,600         |
|              |                                | Ujenzi wa zahanati Iwovo                         | 15/6/2010  | 28,396,850         |
| 6            | Kondoa                         | Upanuzi wa Mfumo wa maji Bukulu                  | -          | 4,378,625          |
|              |                                | Ujenzi madarasa mawili                           | -          | 10,000,000         |
| 7            | Kilombero                      | Ujenzi wa Soko Matema                            | Mei 2010   | 35,000,000         |
| 8            | Rungwe                         | Ujenzi wa madarasa mawili Lupoto Sekondari       | -          | 12,000,000         |
| <b>Jumla</b> |                                |  |            | <b>700,971,208</b> |

Kutotumika kwa miradi ya jamii inachelewesha upatikanaji wa huduma kwa jamii na manufaa yatokanayo na miradi hiyo.

### **iii) Ujenzi wa miradi ya Jamii usiokidhi viwango**

Ukaguzi wa baadhi ya miradi kwa mwaka husika, umebainika kuwa, Sh.630,876,670 zilitumiwa na Halmashauri tatu (3) kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya jamii ambayo ilikamilika kwa kasoro mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali hapa chini. Nilibaini kuwa, miradi iliyotekelizwa inatakiwa kufanyiwa ukarabati mkubwa kwa sababu ya kasoro zake na kusababisha kutotimia kwa malengo yaliyokusudiwa.

| <b>Na</b> | <b>Halmashauri</b>              | <b>Mradi</b>   | <b>Kiasi (Sh.)</b> | <b>Mapungufu</b>   |
|-----------|---------------------------------|--|--------------------|--|
| 1         | Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma | Ufungaji wa Sola katika Shule ya Sekondari ya wasichana Rugufu | 39,200,000         | Paneli za sola zilizofungwa zinatofautiana na makubaliano. Badala ya Paneli 20 za 100W, ziliwekwa paneli 40 za 45W kwa tofauti ya jumla ya 200W. |
|           |                                 | Ukarabati wa zahanati ya Msimba                                | 5,698,000          | Baadhi ya sehemu kwenye dari zimeharibika  |
|           |                                 | Ukarabati wa nyumba ya mganga na zahanati ya Mwandiga          | 43,225,200         | Milango haikufungwa vizuri. Na kuna nyufa kwenye sakafu  |
|           |                                 | Ujenzi wa  | 14,293,070         | Kuna nyufa   |

|   |                                   |  |            |   |
|---|-----------------------------------|--|------------|---|
|   |                                   | darasa katika Shule ya Sekondari ya Kagongo                                      |            | kwenye sakafu   |
|   |                                   | Nyumba ya mganga katika zahanati ya Nyarubanda                                   | 24,000,000 | Ukuta una nyufa na milango haikufungwa vizuri               |
|   |                                   | Ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya sekondari ya Sunuka                    | 24,000,000 | “Wire mesh” hazikukamilika na dari haijafungwa vizuri       |
|   |                                   | Ujenzi wa wodi ya wazazi na chumba cha kuhifadhi maiti katika zahanati ya Uvinza | 60,236,000 | Milango haijafungwa vizuri                                  |
| 2 | Halmashauri ya Wilaya ya Chunya   | Ukarabati wa zahanati ya Udinde  | 8,280,000  | Shata za wavu wa mbu hazikutengenez wa                      |
| 3 | Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo | Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Changalikwa                                      | 41,194,440 | Kuna nyufa kwenye ukuta ambazo zinahitaji ukarabati.        |
|   |                                   | Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Kibindu  | 41,194,440 | Fisha bodi haikufungwa na hata ujenzi wa shule hauna ubora. |
|   |                                   | Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Matipwili  | 41,194,440 | Ujenzi wa madarasa uko chini ya kiwango, kuna nyufa kwenye  |

|  |  |                                      |            |   |
|--|--|--------------------------------------|------------|---|
|  |  |                                      |            | ukuta.  |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Msata   | 41,194,440 | madarasa yamejengwa chini ya kiwango na kuna nyufa kwenye ukuta na sakafu                                 |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Dunda   | 41,194,440 | Madarasa yamejengwa chini ya kiwango na kuna nyufa kwenye ukuta na sakafu                                 |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Zinga   | 41,194,440 | Madarasa matatu yamejengwa chini ya kiwango na uchanganyaji wa saruji na mchanga ulikuwa chini ya kiwango |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Sanzale | 41,194,440 | Madarasa yamejengwa chini ya kiwango na kuna nyufa kwenye ukuta na sakafu                                 |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Ubena   | 41,194,440 | madarasa yamejengwa chini ya kiwango na kuna nyufa kwenye ukuta na sakafu                                 |
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari         | 41,194,440 | madarasa yamejengwa chini ya  |

|  |  |        |  |   |
|--|--|--------|--|---|
|  |  | Mdaula |  | kiwango na<br>kuna nyufa<br>kwenye ukuta<br>na sakafu |
|--|--|--------|--|---|

|  |  |                                      |             |  |
|--|--|--------------------------------------|-------------|--|
|  |  | Ujenzi wa shule ya Sekondari Vigwaza | 41,194,440  | Sakafu kwenye madarasa yote imeharibika na uchanganyaji wa saruji na mchanga ulikuwa chini ya kiwango. |
|  |  | Jumla                                | 542,753,470 |  |

Hii inaonesha mapungufu katika usimamizi na ufuatiliaji wa miradi katika ngazi za chini.

### 5.3 Utekelezaji wa Kilimo Kwanza

“Kilimo Kwanza” ni mkakati wa Serikali unaokusudia kuhuisha Sekta ya Kilimo nchini. Muundo wa utekelezaji wa nguzo za “Kilimo Kwanza” umeainisha wadau mbalimbali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kutekeleza mkakati ya Kilimo Kwanza. Tathmini ya utekelezaji wa “Kilimo Kwanza” katika sampuli ya Halmashauri ishirini (20) imebaini masuala yafuatayo ambayo yanarudisha nyuma na kuzuia utekelezaji wa Kilimo Kwanza kwa ufanisi.

#### 5.3.1 Hoja za Jumla

| Na. | Halmashauri                      | Hoja ya Ukaguzi  | Kiasi (Sh.) | Madhara/Msisi<br>itizo   |
|-----|----------------------------------|--|-------------|--|
| 1   | Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali | <ul style="list-style-type: none"> <li>Majosho katika Vijiji 28 sawa na 25% hayatumiki kwa muda mrefu.</li> <li>Sehemu mbili (2) kati nne (4) za kunyweshea</li> </ul> | -           | Hali hii inaonesha kuwa malengo ya Kitaifa ya kuondoa umaskini katika jamii hayataweza kufikiwa. |

|    |   |  |            |   |
|----|---|--|------------|---|
|    |   | mifugo<br>hazitumiki na<br>majosho<br>matatu (3)<br>kati ya manne<br>(4) pia<br>hayatumiki   |            |   |
| 2  | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Ulanga     | Vocha za<br>pembejeo za<br>kilimo 372<br>hazikutumika<br>hivyo kurudishwa<br>Wizara ya Kilimo<br>kupitia Kamati ya<br>vocha ya Mkoa. | 3,177,000  | Kamati za<br>vocha za<br>Vijiji<br>hazikuwa<br>makini katika<br>kuteua<br>mawakala na<br>walengwa.<br><br>Pia baadhi ya<br>wakulima<br>hawakuwa<br>tayari kutoa<br>mchango wao<br>ili wapate<br>vocha za<br>pembejeo. |
| 3  | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Mwanga     | Nyaraka<br>inayohusu<br>mkakati wa<br>utekelezaji wa<br>“Kilimo Kwanza”<br>haikutolewa kwa<br>Wakaguzi kwa<br>uhakiki.               | -          | Matarajio ya<br>utekelezaji<br>wa “Kilimo<br>Kwanza”<br>katika<br>Halmashauri<br>ya Mwanga<br>hayakuweza<br>kutathminiwa<br>.   |
| 4. | Halmashauri<br>ya Manispaa<br>ya Morogoro | Wizi wa vocha za<br>pembajeo za<br>kilimo.   | 34,055,000 | Jamii<br>haikupata<br>huduma<br>iliyokusudiwa<br>.  |
| 5. | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Babati     | Wakaguzi<br>walipotembelea<br>Halmashauri  | -          | Thathmini ya<br>mahitaji<br>inatakiwa   |

|    |   |   |            |   |
|----|---|---|------------|---|
|    |   | tarehe<br>29/11/2010<br>walibaini kuwa<br>Matrekta madogo<br>(Power tillers)<br>kumi na tatu (13)<br>bado yalikuwa<br>hayajagawiwa<br>kwa vikundi<br>husika.  |            | kufanywa<br>kwanza kabla<br>ya manunuzi<br>ya matrekta<br>madogo.   |
| 6. | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Iramba   | Vocha 21,847 za<br>mbegu za pamba<br>na dawa za<br>kuulia wadudu<br>waharibifu<br>hazikutumika.   | 98,311,500 | Matarajio ya<br>uzalishaji<br>katika msimu<br>wa kilimo<br>hayakuweza<br>kufikiwa<br>kinyume na<br>malengo ya<br>Kilimo<br>Kwanza. Hii<br>imetokana na<br>ucheleweshaji<br>wa kugawa<br>vocha za<br>pembejeo kwa<br>wakulima. |
| 7  | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Namtumbo | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa ya<br/>utekelezaji<br/>wa “Kilimo<br/>Kwanza”<br/>kama inavyo<br/>takiwa na<br/>mpango kazi<br/>wa<br/>Halmashauri<br/>haukutayaris<br/>hwa.</li> <li>• Wakulima<br/>wengi bado<br/>hawajaelewa<br/>madhumuni</li> </ul> |            | Kutokuwepo<br>kwa taarifa<br>ya<br>utekelezaji<br>wa “Kilimo<br>Kwanza”<br>kunafanya<br>kilio cha<br>jamii kuhusu<br>mafanikio<br>duni ya<br>utekelezaji<br>wa “Kilimo<br>Kwanza”<br>katika<br>maeneo yao                     |

|    |                                  |   |                          |  |
|----|----------------------------------|---|--------------------------|--|
|    |                                  | ya “Kilimo Kwanza”.   |                          | na hatua zilozochukuli wa na Uongozi wa Halmashauri hazikuweza kufahamika. |
| 8  | Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa  | <ul style="list-style-type: none"> <li>Vocha za pembejeo za kilimo 1,600 zimeibiwa.</li> <li>Vocha za pembejeo 608 zilizotolewa kwa Halmashauri hazikuweza kutumika.</li> </ul> | 32,300,000<br>11,994,000 | Malengo ya “Kilimo Kwanza” hayakuweza kufikiwa.                            |
| 9  | Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha  | Halmashauri haijaweza kuainisha vipaumbele na mbinu katika uzalishaji wa mazao.   |                          | Malengo ya “Kilimo Kwanza” hayakuweza kujulikana.                          |
| 10 | Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge | Vocha za mbegu za mahindi 1,981 hazikuweza kutumika na zimerudishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora.  | 16,838,500               | Malengo yaliyotarajiw a hayakufikiwa.                                      |
| 11 | Halmashauri ya Wilaya ya Bahi    | Mikopo ya Matrektu madogo bado kurejeshwa   | 34,423,140               | Kutorejeshwa kwa mikopo kunazuia walengwa wengine kutopata huduma          |

|    |                                |  |                          |  |
|----|--------------------------------|--|--------------------------|--|
|    |                                |  |                          | iliyokusudiwa .  |
| 12 | Halmashauri ya Wilaya ya Ileje | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Upotevu wa vocha 200 za ruzuku ya mbolea na Mbegu za mazao.</li> <li>• Katika miaka ya fedha 2007/2008 na 2008/2009, Serikali kwa kupitia Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Mbeya, Programu ya Msaada wa chakula kati ya Japan na Tanzania na Mpango wa Maendeleo wa Ileje zilikamilisha mradi wa umwagiliaji wa Sasenga uliogharimu kiasi cha Sh.452,346,71 0 ukiwa na ukubwa wa hekta 540. Pia katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 Halmashauri ilitumia kiasi</li> </ul> | 3,600,000<br>534,540,950 | Malengo yaliyotarajiw a hayakufikiwa.<br><br>Kukosekana kwa mipango madhubuti na kutokulinda mradi kutapelekea thamani ya fedha kutopatikana na mradi kutokuwa endelevu. |

|    |  |  |   |  |
|----|--|--|---|--|
|    |  | <p>cha Sh.<br/>82,194,240<br/>kwa ajili ya<br/>kujenga<br/>mfereji mkuu.<br/>Timu ya<br/>ukaguzi<br/>ilipotembelea<br/>mradi huo<br/>mnamo<br/>Augosti, 2010<br/>ilibaini kuwa<br/>eneo lote la<br/>mradi lilikuwa<br/>halitumiki<br/>kwani ni<br/>hekta 270 tu<br/>au 50% ndizo<br/>zilikuwa<br/>zinatumika<br/>kwa<br/>umwagiliaji.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Kumekuwepo<br/>na uchungaji<br/>wa mifugo<br/>katika eneo la<br/>mradi na<br/>uchomaji<br/>moto lakini<br/>hakuna hatua<br/>zozote<br/>zinazochukuli<br/>wa.</li> </ul> |   |  |
| 13 | Halmashauri<br>ya Wilaya ya<br>Kilombero | <p>Mawakala<br/>kuchelewa<br/>kusambaza<br/>pembejeo za<br/>kilimo kwa<br/>wakulima:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• KiJiji cha<br/>Kibaoni<br/>kilipokea</li> </ul>  | Pembejeo za<br>kilimo<br>hazikutumika<br>kama<br>ilivyopangwa<br>kutokana na<br>sababu<br>kwamba<br>zililetwa |  |

|     |                                 |   |            |   |
|-----|---------------------------------|---|------------|---|
|     |                                 | <p>vocha za pembejeo za kilimo mwezi Novemba, 2009 lakini mawakala walichelewa kuzisambaza kwa wakulima hadi mwezi Januari, 2010.</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Vocha za pembejeo za kilimo kutoka Halmashauri hazi kupokelewa katika Vijiji vya Mofu na Ikwambi.</li> </ul> | 21,900,000 | katikati ya msimu wa kilimo.  |
| 14. | Halmashauri ya Wilaya ya Songea | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Taarifa ya utekelezaji wa Kilimo Kwanza haikuandaliwa kama inavyotakiwa na mpango wa kazi wa Halmashauri.</li> <li>• Wakulima wengi kutokufahamu malengo na madhumuni ya “Kilimo Kwanza”.</li> </ul>   |            | Kukosekana kwa Taarifa za utekelezaji wa Kilimo Kwanza kunafanya kilio cha Jamii kuhusu mafanikio duni ya utekelezaji wa “Kilimo Kwanza” katika maeneo yao na hatua zilizochukuli wa na Uongozi wa Halmashauri kutoweza |

|     |                                   |   |            | kufahamika.  |
|-----|-----------------------------------|---|------------|--|
| 15  | Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro | Vocha 6,441 za pembejeo za kilimo hazikutumika hivyo kurudishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro.  | 33,090,000 | <ul style="list-style-type: none"> <li>• Baadhi ya Mawakala kushindwa kusambaza pembejeo za kilimo kwa wakati.</li> <li>• Baadhi ya mawakala kuwa na mitaji midogo.</li> <li>• Baadhi ya Wakulima kushindwa kuchangia gharama za ununuzi wa pembejeo.</li> </ul> |
| 16  | Halmashauri ya Wilaya ya Same     | Kati ya malengo 38 yaliyokuwemo katika mkakati wa “Kilimo Kwanza” malengo kumi na nane (18) yametekelezwa, kumi na tano (15) yapo katika hatua za utekelezaji wakati matano (5) bado kutekelezwa. |            | Malengo yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka husika haya kutekelezwa yote.  |
| 17. | Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma | Tathmini ya utekelezaji wa “Kilimo Kwanza” imebaini kuwa miradi ya  |            | Utekelezaji wa kiwango cha chini cha mipango iliyo kusudiwa.   |

|              |                                |  |                    |   |
|--------------|--------------------------------|--|--------------------|---|
|              |                                | maendeleo ya sekta ya kilimo bado ipo katika hatua za awali hivyo mchango wake haukuweza kuainishwa. |                    |   |
| 18.          | Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi | Upotevu wa vocha za ruzuku ya mbolea na mbegu za mazao.  | 130,800,000        | Huduma zilizokusudiwa hazikutolewa kwa Jamii. |
| <b>Jumla</b> |                                |  | <b>977,430,090</b> |   |

### 5.3.2 Upungufu wa mbolea katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi

Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi ilipanga kusambaza tani 40,184 za aina mbalimbali za mbolea kwa wakulima katika kata na Vijiji Wilayani humo. Hata hivyo, Halmashauri ilipokea tani 21,720 sawa na asilimia 54% ya malengo ya awali. Pia ilibainika kuwa, Halmashauri ilipokea tani 360 za mbolea ambayo haikuhitajika. Mchanganuo wa kina ni kama ufuatao:

| Na. | Aina ya mbolea | Kiasi kilichokisiwa (Tani) | Kiasi kilichopokewa (Tani) | Tafauti (Tani) |
|-----|----------------|----------------------------|----------------------------|----------------|
| 1.  | DAP            | 10,785                     | 6,050                      | 4,735          |
| 2.  | UREA           | 21,570                     | 13,650                     | 7,920          |
| 3.  | CAN            | 2,669                      | 861                        | 1,808          |
| 4.  | SA             | -                          | 330                        | 330            |
| 5.  | NPK            | 600                        | 71                         | 529            |
| 6.  | MRP            | 4,200                      | 728                        | 3,472          |
| 7.  | TSP            | -                          | 30                         | 30             |

### 5.3.3 Upungufu wa Pembejeo za Kilimo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya

Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilikuwa na mahitaji ya aina mbalimbali za pembejeo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima

waliopo katika Jiji hilo. Ukaguzi umebaini kuwa pembejeo hizo za kilimo hazikuweza kupatikana kulingana na mahitaji ya Halmashauri kama inavyooneshwa hapa chini.

| Aina ya Pembejeo           | Mahitaji (Tani) | Kiasi kilichopatikana (Tani) | Upungufu (Tani) | Asilimia ya Upungufu |
|----------------------------|-----------------|------------------------------|-----------------|----------------------|
| DAP                        | 1,000           | 750                          | 250             | 25                   |
| Mbolea ya Minjingu         | 1,800           | -                            | 1,800           | 100                  |
| UREA                       | 1,600           | 740                          | 860             | 54                   |
| Mbegu za mahindi - Chotara | 135             | 15                           | 120             | 89                   |

Kutokana na masuala yaliyojitekeza na kuhojiwa hapo juu, mfumo wa utoaji na usambazaji wa vocha za pembejeo za kilimo unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

- Kukosekana kwa uelewa wa taratibu za mfumo wa vocha za pembejeo kwa wakulima na Kamati za vocha pembejeo za Vijijini.
- Mawakala wa pembejeo za kilimo kuchelewa kusambaza vocha za pembejeo kwa wakati.
- Mawakala wa pembejeo kuwa na mitaji midogo hivyo kuwafanya washindwe kupeleka vocha nyingi Vijijini.
- Miundombinu mibovu husababisha usambazaji wa vocha kwenye baadhi ya Vijiji kuwa mgumu.
- Kukosekana kwa fedha za kutosha kwa ajili ya ufuutiliaji na kutoa elimu kwa Kamati za vocha za kilimo katika Vijiji.
- Kutokuwepo na udhibiti na ufuutiliaji wa karibu wa usambazaji wa vocha na pembejeo.

Ili kufanikisha kufikia matarajio ya “Kilimo Kwanza” ninapendekeza yafuatayo:

- Kamati zinazoshughulikia vocha za pembejeo za kilimo zinatakiwa kuwa na ufuutiliaji wa karibu na kuhakikisha

hatua za kisheria zinachukuliwa kwa wale waliohusika na upotevu wa vocha za pembejeo.

- Uongozi wa Mamlaka wa Serikali za Mitaa unatakiwa kuhakikisha kwamba mawakala wanaosambaza pembejeo wanafuata masharti yaliyomo katika mikataba.
- Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba usambazaji wa pembejeo unafanyika kwa wakati na kulingana na mahitaji ili kuhamasisha maendeleo ya kilimo katika Mamlaka hizo.

## SURA YA SITA

### 6.0 MATOKEO YA KAGUZI MAALUM 6.1 Utangulizi

Kifungu 36 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi maalumu. Sheria hii inaeleza kuwa, iwapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ataona kuwa kuna jambo lolote lihusulo fedha au mali ya umma ambalo inabidi Bunge llijulishwe pasipo kuchelewa, ataandaa taarifa maalumu kuhusiana na jambo hilo na kuwasilisha taarifa hiyo Bungeni kuitia kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- 6.2 Mtiririko wa mabadiliko baada Kaguzi Maalum**  
Katika mwaka uliopita wa 2008/09 taarifa za kaguzi maalumu nane (8) zilitolewa na mhutasari wa utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa umeelezwa katika sura ya tatu aya ya kumi na moja (11) ya ripoti hii. Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 kaguzi maalum tano (5) zilifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya kaguzi maalum tano (5) zilizofanyika, tatu ziliombwa na Halmashauri, na mbili zilianzishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mujibu wa Kanuni 78 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za 2009. Kaguzi maalum tano zilifanyika katika Halmashauri tano (5) ambazo ni Halmashauri za Wilaya za Rombo, Kilosa, Rorya, Tarime na Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga. Matokeo yaliyotokana na kaguzi maalum yameainishwa katika aya zifuatazo:
- 6.3 Muhtasari wa masuala yaliyojitokeza katika kaguzi maalumu zilizofanyika mwaka 2009/10**

#### 6.3.1 Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo ulihusu masuala yaliyojitokeza katika kipindi cha tarehe 1

Julai, 2007 hadi tarehe 30 Oktoba, 2009. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

- Vifungu vinne (4) vya Akaunti ya Amana vilitumia Sh.105,209,155 zaidi ya kiasi kilichowekwa. Hali hii inaathari katika fedha za waweka amana wengine ambazo zinatakiwa kurejeshwa katika vifungu vya Amana husika.
  - Mishahara isiyolipwa kiasi cha Sh.15,537,292 hajarejeshwa Hazina kwa kupitia kwa Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro. Kiasi hiki kimelipwa kimakosa kama mishahara kwa Watumishi ambao hawako kazini.
  - Uhamisho wenge shaka wa fedha kiasi cha Sh.15,868,475 toka Akaunti ya Amana kwa ajili ya matumizi ambayo uhalali wake haukuweza kuthibitika.
  - Malipo ya fedha taslimu kiasi cha Sh.13,499,945 ambayo yalitakiwa kulipwa moja kwa moja kwa Wazabuni lakini yalilipwa kwa watumishi wa Halmashauri kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa mbalimbali kutoka kwa Wazabuni hao.
  - Malipo yalifanyika mara mbili toka Akaunti ya Amana kwa ajili ya marejesho ya mikopo ya benki Sh.6,158,680 kwa watumishi wa Halmashauri.
  - Mifuko ya saruji yenye thamani ya Sh.4,795,000 iliyotolewa toka Stoo ya Halmashauri haikuweza kuthibitishwa kwamba imepokewa kwenye sekondari saba (7) husika.
  - Akauti tatu (3) za Halmashauri zimepata Ovadrafti bila idhini ya kamati ya Fedha na Utawala ya Halmashauri kinyume na matakwa ya Kifungu na. 12(1) cha Sheria Na.9 ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 na Agizo Na.183 ya Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997. Pia hapakuwepo na ushahidi kwamba Ovadrafti hiyo iliyotolewa na benki iliinufaisha Halmashauri.
- 
- **Malipo ya mishahara yenye shaka**
    - (i) Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao hawapo kazini Sh.2,493,240.
    - (ii) Ruzuku ya Serikali kutumika kulipia mishahara ya watumishi waliotakiwa kulipiwa toka Akaunti ya Mfuko mkuu wa Halmashauri Sh. 16,064,413.

- **Mapungufu katika usimamiaji wa vyanzo vya ndani vya Halmashauri**
  - (i) Mawakala wa ukusanyaji wa mapato kwa niaba ya Halmashauri kutowasilisha makusanyo Sh.20,306,000.
  - (ii) Mapato yasiyokusanya kutokana na ushuru wa zao la kahawa Sh. 56,234,011.
  - (iii) Ushuru wa zao la kahawa uliokusanya kwa kutumia stakabadhi za kugushi Sh.11,058,063.
  - (iv) Ushuru wa mazao ya misitu kiasi cha Sh.27,857,794 haukuingizwa kwenye daftari la mapato la Halmashauri wala kupelekwa benki. Hii imetokana na uzembe wa Mweka hazina wa kutokufuatilia makusanyo ya kila siku na upelekaji wake benki.
  - (v) Ushuru unaotokana na ukodishaji wa mashamba katika ukanda wa nusu maili wa msitu wa Halmashauri kiasi cha Sh.27,787,500 haujakusanya.
  - (vi) Malipo ya posho kwa watumishi na matumizi mengine Sh.11,090,000 zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa.
  - (vii) Posho ya kujikimu yenyе jumla ya Sh 7,280,000 iliyopwa kwa baadhi maofisa ilibainika kuwa ya mashaka kwani maafisa hao walisaini kwenye daftari la mahudhurio kwa siku walizolipwa wakiwa nje ya kituo chao cha kazi. Kuna udhaifu katika udhibiti wa ndani kuhusu ulipaji wa posho.
  - (viii) Katika miaka ya fedha ya 2007/2008 na 2008/2009, kulikuwa na matumizi ya ziada ya Sh.190,078,699 katika manunuzi ya mafuta ya magari.
  - (ix) Mafuta ya magari yenyе thamani ya Sh.64,581,030 yalinunuliwa na kugawanywa kwenye magari ya Halmashauri. Hata hivyo mafuta hayo haya kuthhibitika kuwekwa kwenye magari kutokana na taarifa hizo kutokuwa kwenye vitabu vya safari za gari.

- (x) Mafuta ya magari yenyе thamani ya Sh.4,024,500 yalitolewa na kutumika kwenye magari ya watu binafsi.
- (xi) Halmashuri imetumia vibaya fedha za Idara ya Elimu kiasi cha Sh. 31,020,000 kwa ajili ya manunuzi ya wino wa mashine ya chapa kiasi cha Sh.14,635,000 na wino wa mashine ya kutolea nakala kiasi cha Sh. 16,385,000.
- (xii) Kumekuwepo na ufujaji wa fedha kiasi cha Sh.18,699,000 katika manunuzi na matumizi ya karatasi za kutolea nakala, shajala na wino wa mashine ya kutolea nakala.
- (xiii) Ukaguzi maalum umebaini kuwa Halmashauri ililipa bei za juu katika ununuzi wa daftari za andalio la masomo na vitabu vya kumbukumbu za masomo katika mchakato wa manunuzi kwa Mzabuni wa Halmashauri kuweka kiwango cha juu cha bei ukilinganisha na bei katika soko na kupelekea kutumia matumizi ambayo yangeweza kuepukwa ya kiasi cha Sh.17,500,000.
- (xiv) Kulikuwepo matumizi yenyе shaka na yasiyofuata sheria husika kiasi cha Sh.7,949,204.
- (xv) Kiasi cha Sh.232,393,000 kilikusanywa kutokana na mauzo ya mahindi ya njaa na kupelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu lakini stakabadhi za kukiri mapokezi hazikuonekana wakati wa ukaguzi.
- (xvi) Mahindi ya msaada wa njaa hayakuwafikia walengwa Sh.9,866,726.
- (xvii) Fedha kiasi cha Sh.2,760,000 zilizotengwa kwa kusafirishia mahindi ya msaada wakati wa njaa hazikutumika kwa lengo lililokusudiwa na badala yake kutumika kwa ununuzi wa matairi ya magari ya Halmashauri.
- (xviii) Vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya Sh.14,238,000 vilivyotolewa toka Stoo Kuu ya Halmashauri havikupokewa katika sehemu ya ujenzi.

(xix) Fedha taslimu zilizopatikana kwa uuzaaji wa viwanja katika Mji wa Holili kiasi cha Sh.7,380,000 hakikuingizwa katika vitabu vyta Halmashauri.

### 6.3.2 Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa

Mapungufu yaliyobainika kwenye Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa uliohusu miaka ya fedha 2008/2009 na 2009/2010 ni kama yafuatavyo:

- (i) **Udhaifu katika Udhibiti wa mfumo wa ndani na uhasibu**  
Mapitio ya udhibiti wa ndani na uhasibu umebaini mapungufu yafuatayo:

- Imebainika kuwa mtumiaji mmoja wa mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha (IFMS) anaweza kuingiza, kuidhinisha na kurekodi miamala kwa kutumia akaunti ya msimamizi wa mfumo (sa) bila udhibiti.
- Marekebisho katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) yalifanyika bila kuidhinishwa na Mkurugenzi wa Halmashauri na Mweka Hazina kama inavyooneshwa kwenye Jedwali hapa chini:

| Mwaka     | Pokezi (Sh.)  | Toa (Sh.)     |
|-----------|---------------|---------------|
| 2007/2008 | 8,887,051,520 | 7,622,245,054 |
| 2008/2009 | 5,850,462,464 | 4,014,388,619 |

- Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya Wilaya ilibadilisha Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) kutoka toleo la 7.2 kwenda 7.3.5 bila kuwahusisha Wataalam wa Mifumo kutoka TAMISEMI hivyo kusababisha baadhi ya vifungu vya matumizi pamoja na bakaa zake kutokuingizwa katika toleo jipya kwa usahihi kwa kuonesha kwamba vifungu hivyo havina fedha kitu kilichosababisha matatizo katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2009/2010.

- Hati za malipo zenyenye thamani ya Sh.766,489,920 hazikuwasilishwa kwa Wakaguzi.
- Malipo ya Sh.838,990,537 yamekosa Stakabadhi za uthibitisho wa kukiri mapokezi.
- Kumekuwepo na matukio sita (6) ya wizi wa fedha katika akaunti za Halmashauri zenyenye jumla ya Sh.277,026,849 yaliyosababishwa na udhaifu ya udhibiti wa ndani wa watumishi wasio waaminifu na kutofanyika kwa usuluhisho wa vitabu kwa wakati.
- Katika kipindi cha mwaka 2008/09 Halmashauri ilifanya malipo zenyenye jumla ya Sh.7,966,372,050 toka Akaunti ya Amana bila kuonesha namba ya stakabadhi iliyopokea ili kuthibitisha kama malipo yalifanyika kwa mujibu wa malengo ya fedha hizo. Pia ilibainika kuwa hakuna rejista ya Akaunti za Amana kwa ajili ya udhibiti na hivyo kupelekea ufujaji wa fedha katika mfuko huo.
- Kutokuwepo kwa mgawanyo wa kazi katika Idara ya Uhasibu kwa miaka ya fedha 2007/2008 na 2008/2009 kinyume na kifungu Na. 10 cha Mwongozo wa Fedha wa Serikali za Mitaa wa mwaka 1997.
- Mawanda ya ukaguzi wa ndani kuwa finyu kwa kakagua zaidi miradi inayohusiana na shule badala ya kukagua miradi yote ya maendeleo kwa ujumla. Pia Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya kuchelewa kujibu hoja za Wakaguzi wa Ndani na wa Nje hivyo kusababisha hoja hizo kutojadiliwa katika vikao vya Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.
- Mweka Hazina alikuwa nje ya Ofisi kwa muda mrefu kwa sababu ya matatizo ya kiafya hivyo kusababisha utendaji usioridhisha katika Idara ya Fedha na Uhasibu.
- Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ilikuwa ikidaiwa kiasi kikubwa cha madeni ya Sh. 991,968,836.
- Katika kipindi cha mwaka 2007/08 na 2008/09 Halmashauri ilihamisha kiasi cha Sh.132,550,989 kutoka na kwenda akaunti mbalimbali na hadi wakati wa

ukaguzi maalum fedha hizo ziliwa hazijarejeshwa kwenye akaunti husika.

- Ukaguzi maalum umebaini kuwa Halmashauri ililipa kiasi cha Sh.29,041,360 katika kipindi cha mwaka 2008/2009. Fedha hizo zililipwa toka kwenye kasma zisizostahili.
- Ukaguzi maalum pia umebaini kuwepo kwa mashauri mbalimbali Mahakamani dhidi ya Halmashauri ya kiasi cha Sh.504,620,000. Pia Halmashauri inadaiwa kiasi cha Sh. 296,287,840.

**(ii) Udhafu katika udhibiti wa ukusanyaji mapato**

- Vitabu vya kukusanya mapato vipatavyo 394 havikuwasilishwa kwa wakaguzi vilipohitajika.
- Imebainika kuwa makusanyo ya fedha taslimu hutumika kwa kubadilishana malipo ya hundi na kusababisha kiasi cha Sh.34,913,620 kutopelekwa benki.
- Kumefanyika Oparesheni ya ukusanyaji ushuru wa mazao usiozingatia gharama za kukusanya mapato ambapo Halmashauri ilitumia gharama ya kiasi cha Sh.119,614,000 katika kukusanya mapato ya Sh.57,226,690 hivyo kusababisha hasara ya Sh.62,387,110.
- Halmashauri ilikusanya kiasi cha Sh. 217,358,920 zilizotokana na mapato ya operasheni ya mifugo iliyofanyika kati ya tarehe 29/1/2009 hadi tarehe 29/2/2009. Kiasi hicho kilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo matumizi yake hayakuweza kuthibitika.
- Katika kipindi cha miaka fedha ya 2007/2008 na 2008/2009, Mradi wa Ukodishaji wa magari ya Halmashauri uliingiza hasara ya Sh.6,723,143 iliyosabishwa na kukusanya mapato ya Sh.42,650,000 lakini matumizi yalikuwa kiasi cha Sh.49,373,141.
- Halmashauri haikuweza kuzingatia Sheria ndogo ndogo za ukusanyaji wa mapato hivyo kushindwa kukusanya

kiasi cha Sh.727,562,725 kutoka kampuni ya Sukari Kilombero kulikotokana na uzembe wa Idara ya Fedha kutoza ushuru wa miwa wa kiwango cha Sh.200 kwa tani ya miwa badala ya 5% na 3%.

**(iii) Mapungufu katika masuala ya Rasilimali Watu na malipo ya posho**

- Ukaguzi maalum umebaini mapungufu katika masuala ya rasilimali watu kama vile kusimamishwa kazi kwa watumishi na baadhi ya watumishi kukaa katika kituo kimoja cha kazi kwa muda mrefu wa kati ya miaka 7 hadi 36.
- Malipo ya posho ya kujikimu yalibainika kuwa yenyе shaka kutokana na tarehe za madai kusigana na zile zilizoonyeshwa kwenye mahudhurio ya kazi katika vitabu vya mahudhurio vya Halmashauri kwa ajili ya watumishi wake. Pia gharama za usafirishaji wa mizigo kulipwa mara mbili na vilevile kukosekana kwa daftari ya kumbukumbu za mahudhurio ya kila siku kumesababisha baadhi ya malipo ya posho za kujikimu kutohakikiwa na wakaguzi. Jumla ya malipo ya posho mbalimbali batili na yenyе mashaka ni Sh.196,099,000.
- Ukaguzi maalum umebaini kuwa kulikuwa hakuna rejista ya mishahara isiyolipwa kinyume na kanuni za fedha za umma zinavyotaka na kusababisha taarifa za watumishi zinazohusu kustaafuli, kufariki na kuachishwa kazi kutowasilishwa kwa wakati, hivyo kupelekeea mishahara ya watumishi wasiokuwepo kazini ya Sh.94,786,202 kuendelea kulipwa katika Akaunti zao binafsi.
- Malipo ya mishahara ya Walimu wapya iliyolipwa kama posho ya kujikimu kiasi cha Sh.11,200,000 bado kurejeshwa.
- Kuchelewa kulipa makato ya kisheria, mikopo ya wafanyakazi na wadai mbalimbali kumesababisha hundi zenyе jumla ya Sh.77,909,218 kuchacha. Pia kumekuwepo na makato kupita kiasi kwenye mishahara ya watumishi

kulikopelekea baadhi ya watumishi kupokea mishahara chini ya 1/3 ya mishahara yao.

- (iv) **Kutozingatia Sheria na Kanuni za manunuzi ya Umma**  
Halmashauri haizingatii Sheria na Kanuni za manunuzi ya Umma hivyo kusababisha mapungufu yafuatayo:
- Halmashauri ilifanya matengenezo ya magari yake ya jumla ya Sh. 34,572,145 lakini Ubou/Magonjwa ya Magari yaliyotengenezwa haukuweza kuthibitika kwa sababu ya kutowekwa kumbukumbu katika daftari la matengenezo ya magari na kutokaguliwa na Mhandisi wa Mitambo kabla na baada ya matengenezo.
  - Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilifanya manunuzi ya kompyuta kwa Sh. 6,400,000 bila kufafanua viwango vytaalam kwenye nyaraka za manunuzi.
  - Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ilifanya manunuzi yenye shaka na matengenezo ya mashine ya kutolea nakala kiasi cha Sh.22,275,400.
  - Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. 12,431,600 vilivyoagizwa na kulipiwa, vimegundulika kutoingizwa katika leja na hivyo kutothibitishwa kupokelewa.
  - Jumla ya lita 47,689.6 za mafuta ya dizeli yenye thamani ya Sh.78,623,015 yametolewa katika magari bila kuwepo na udhibiti na kuingizwa kwenye daftari la matumizi ya magari hivyo kutothibitika kama yalitumika katika shughuli zikizokusudiwa.
  - Manunuzi mbalimbali yamefanyika kwa kutumia masurufu (Imprests) Sh.28,980,060 kinyume na Sheria na Kanuni za fedha.
  - Utata wa utoaji wa zabuni ya ununuzi wa vivunge vyasayansi vytaalam Sh.47,380,000.
  - Manunuzi ya bidhaa yaliyokiuka taratibu na kanuni za manunuzi Sh.39,400,805.
  - Manunuzi yaliyofanyika bila kuwa na idhini ya bodi ya zabuni na yaliyozidi kiwango kinachotakiwa kuidhinishwa na Afisa Masuuli Sh.663,899,454.
  - Manunuzi yasiyokuwa na ushindanishi wa bei Sh.14,423,805.

- Vifaa viliyyonunuliwa vyenye thamani ya Sh.214,660,229 havikuweza kuhakikiwa kwa sababu ya kukosekana kwa kitabu cha leja ya kupokelea vifaa na kuonesha matumizi ya vifaa hivyo katika Idara ya Kilimo.
- Magari 6 yaliyozuiliwa katika gereji mbalimbali kwa muda mrefu kati ya miezi mitano hadi miaka miwili kwa sababu ya deni la Sh.164,159,267.
- Kutokuwepo kwa rejista ya mali na vifaa chakavu.

**(v) Mapungufu yaliyoonekana katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

- Salio la fedha za VVU/UKIMWI kiasi cha Sh.117,242,851 kimetumika kwa matumizi yasiyo kusudiwa kama vile matayarisho ya bajeti na mambo mengine yasiyo kuwemo katika mpango kazi.
- Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Halmashauri ya Wilaya ilihamisha kiasi cha Sh.42,465,000 toka Akaunti ya Mpango wa Maendeleo ya Kilimo wa Wilaya (DADPS) kwenda katika Akaunti ya Mfuko Mkuu kwa ajili ya kugharamia manunuzi ya magari na matumizi ya mikutano ya Kamati za Uchumi, Ujenzi na Mazingira lakini kiasi hicho bado hakijarejeshwa katika Akaunti husika.
- Kuchelewa kukamilishwa kwa miradi ya nyuma ingawa fedha zote za kugharamia miradi hiyo zilikwishatolewa. Sababu za kutokamilisha miradi hiyo ni kushindwa kwa Wakandarasi kumaliza kazi kulingana na muda uliowekwa kwenye mikataba.
- Baadhi ya makandarasi kulipwa malipo ya awali kwa kiwango cha juu cha 30% hadi 70% ya bei ya mkataba kinyume na kiwango cha 15% kilichopendekezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma.
- Miradi mbalimbali iliyotekelizwa katika ngazi za Vijiji/kata haikufuata Miongozo iliyotolewa na Serikali kwa sababu Halmashauri haitoi ushauri wa kiufundi kwa kamati za Miradi hali iliyosababisha baadhi ya miradi kukamilika chini ya viwango vinavyotakiwa.

- Kiwango kidogo cha uchangiaji wa wananchi kwenye miradi na shughuli za maendeleo kunasababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati uliopangwa.
- Kiasi cha Sh.264,159,900 kilichopangwa kutumika katika kutekeleza shughuli mbalimbali katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kilihamishiwa katika miradi ya maendeleo ambayo haikuidhinishwa wala kuwemo katika mpango kazi. Pia katika kipindi hicho kiasi cha Sh.119,000,000 kilitumika zaidi ya makisio/bajeti.
- Kuna kasoro katika utunzaji wa mafaili yenyе kumbukumbu za mikataba, matumizi yasiyozingatia shughuli za maendeleo zilizokusudiwa kama vile malipo ya posho na mafuta ya magari. Pia imebainika kuwa kiasi cha Sh.51,656,253 kilichotakiwa kupelekwa kutekeleza miradi ya maendeleo katika ngazi za Vijiji hazikupelekwa.
- Baadhi ya mikataba iliyoingiwa kati ya Halmashauri na Wakandarasi ilikuwa na upungufu wa vifungu muhimu vyta mikataba kama vile muda wa mkataba, tozo la kuchelewa kukamilisha kazi katika muda uliomo kwenye mkataba na dhamana kwa ajili ya kinga kwa malipo ya awali kwa wakandarasi.
- Mradi wa maji wa Meshungi uliogharimu kiasi cha Sh.160,261,190 ulianza mwaka wa fedha wa 2001/2002 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Hata hivyo hadi kufikia mwaka wa fedha 2010/2011 hakuna dalili ya kukamilika kwa mradi.
- Mradi wa maji wa Mtumbatu uliogharimu Sh.267,247,007 ulianza mwaka 2000 na kufadhiliwa na Benki ya Dunia katika Miradi ya maji ya dharura. Hata hivyo ilibainika kuwa Mradi huo umeachwa kwa muda mrefu bila ya kufanya kazi kutokana na wananchi kushindwa kununua lita za mafuta ya dizeli lita 400 zinazohitajika kuendeshea mashine ya kusukuma maji kila siku ili kujaza tanki la maji, jambo linalohatarisha miundombinu hiyo kuweza kuibiwa au kuharibiwa.

### **6.3.3 Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga**

Muhtasari wa Matokeo ya ukaguzi maalum na uchunguzi wa ujenzi wa barabara za Mjini - 5.9 KM

- Mradi wa ujenzi wa barabara haukuwa katika mpango wa manunuzi kinyume na kifungu Na. 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya 2004. Hii imeathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.
- Zabuni ilitangazwa tarehe 3 Januari 2008 kabla ya idhini ya Bodi ya Zabuni tarehe 14 Januari 2008 kinyume na Kifungu Na. 30 cha Sheria ya manunuzi wa Umma Namba 21 ya 2004. Hii inaashiria ufinyu wa mawanda ya bodi ya zabuni ya Halmashauri.
- Kitengo cha usimamizi wa manunuzi cha Halmashauri (PMU) hakikushirikishwa katika uteuzi wa timu ya tathmini kinyume kifungu Na. 37 (2) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.21 ya 2004. Hii inaingilia uhuru wa PMU katika kutimiza majukumu yake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria.
- Makubaliano binafsi yalifanyika baada ya kukamilika tathmini ya Mradi kinyume cha kifungu na. 37 (6) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya 2004. Ukosefu wa maslahi binafsi haukuweza kuthibitika.
- Mkandarasi alipewa ongezeko la muda wa kufanya kazi kwa mwezi mmoja bila kuwa na barua ya maombi ya nyongeza ya muda wa kazi iliyoidhinishwa na bodi ya zabuni. Hii inadhihirisha udhaifu kwa upande wa Kitengo cha Manunuzi wakati maandalizi ya nyaraka za mkataba.
- Mkataba uliingiwa na Halmashauri bila kuwepo na dhamana ya utendaji ya kiasi cha 15% ya bei ya mkataba kinyume na kifungu 55.1 cha masharti ya mkataba. Kutokana na ukosefu wa dhamana ya utendaji, Halmashauri ilikuwa katika sehemu ambayo si salama kimkataba.
- Kuna utata kati ya kipindi cha kukamilika kwa mradi cha miezi tisa (9) kilichotajwa katika barua ya kukubali kazi na kipindi cha miezi nane (8) iliyoainishwa katika fomu

ya zabuni. Hii imesababisha uchelewaji katika utoaji wa huduma iliyokusudiwa kwa jamii ambao ni walengwa.

- Kipindi cha dhima ya ujenzi wa barabara ya lami kilikuwa ni miezi sita (6), hii ni chini ya kiwango kinachokubalika cha mwaka mmoja kwa ajili ya kuruhusu barabara kuweza kujaribiwa wakati wa vipindi mbalimbali vyatia hewa.
- Kuna mkanganyiko kati ya kifungu Na. 23 cha masharti maalum ya mkataba ambacho kinahitaji kiwango atakachotozwa mkandarasi pindi akichelewesha kazi kuwa 0.15% ya jumla ya mkataba kwa siku zote atakazochelewa hadi kufikia kiwango cha juu cha siku 100, wakati kifungu Na. 29 cha masharti maalum ya mkataba kinataja kiwango cha juu cha kutoza kuwa ni siku 45. Huu ni udhaifu wa PMU wakati wa maandalizi ya nyaraka za mkataba, ambayo inaweza kusababisha migogoro kati ya mkandarasi na mwajiri endapo mkandarasi atachelewesha kazi.
- Malipo ya awali yaliyotolewa kwa mkandarasi bila dhamana ya malipo ni kinyume na kifungu Na. 25 cha masharti maalum ya mkataba.
- Michoro ya Mradi haikuandaliwa vizuri ili kuweza kutofautisha bayana tabaka la barabara ya zamani na matabaka yaliyojengwa katika viwango mbalimbali vyatia ujenzi. Huu ni udhaifu kwa upande wa Mhandisi wa Manispaa, hali iliyosababisha kuwa na barabara isiyo na mlingano.
- Kiasi cha Sh.37,486,156 kililipwa kwa ziada kama malipo ya awali wakati mkandarasi akiwa tayari yuko kwenye mradi. Malipo ya awali hutakiwa kulipwa kwa mkandarasi ambaye hajaanza kazi ili kumuwezesha kufanya maandalizi ya awali. Aidha, mkandarasi huyu awali alishalipwa malipo ya awali ya Sh.134,860,015 yaani 15% ya bei ya mkataba.
- Uchunguzi wa kifusi kwa ajili ya tabaka la msingi uliofanywa maabara ulionesha kuwa kifusi hakikufikia viwango vinavyotakiwa. Kwa mujibu wa matokeo ya vipimo vyatia maabara yaliyofanyika katika maabara za

TANROADS-Rukwa, ubora wa tabaka la msingi lililowekwa halikukidhi viwango, hivyo ujenzi haukutakiwa kuendelea hadi marekebisho yafanyike. Hii inaweza kusababisha barabara kuharibika kwa haraka.

- Kiasi cha Sh.43,006,210 zilitumika kutoka akaunti ya mfuko wa barabara bila idhini ya bodi ya mfuko wa barabara. Fedha hizo zilizidi kiwango kilichoidhinishwa.

#### **6.3.4 Halmashauri ya Wilaya ya Rarya**

Lengo kuu la ukaguzi huu maalum lilikuwa ni kuangalia juu ya uwajibikaji wa fedha zilizotengwa na kutumiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rarya.

##### **(i) Matokeo ya ukaguzi maalum**

- Katika miaka ya fedha 2007/2008 na 2008/2009, Halmashauri ilihamisha jumla ya Sh.98,927,500 kutoka Akaunti ya Maendeleo kwenda Mfuko mkuu wa Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa jengo la muda la ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri bila ya ujenzi huo kuwepo kwenye bajeti. Hakuna ushahidi wa marejesho ya fedha hizo kwenda kwenye akaunti ya maendeleo.
- Jumla ya Sh.13,138,500 zililipwa kwa wafanyakazi vibarua bila kusaini kwenye karatasi ya mahudhurio.
- Kulikuwa na matumizi ya ziada ya Sh.7,790,167 katika bajeti kwa ajili ya manunuzi ya vifaa vyta ujenzi.
- Katika mwaka 2006/2007 Halmashauri ilipokea Sh.90,000,000 kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa ajili ya miradi ya maji katika Vijiji vya Masonga, Gabimori na Shirati. Hata hivyo, Mradi wa maji wa Gabimori haukukamilika kwa kuwa jumla ya Sh.23,345,050 zilizotengwa kwa ajili ya mradi huo zilitumika kwa ajili ya shughuli nyingine.
- Kiasi cha Sh.9,308,611 ambacho ni 20% ya mapato ya ndani kilipelekwa Vijijini katika mwaka 2008/09. Hata hivyo hapakuwa na stakabadhi za kukiri mapokezi ya fedha hizo. Aidha, jumla ya Sh.3,710,789 hazikupelekwa kabisa Vijijini.

- Jumla ya Sh.39,610,000 kati ya Sh.84,895,923 zilizohamishwa kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine hazikuthibitika kurejeshwa katika akaunti husika.
- Jumla ya Sh.54,585,923 zilihamishwa kutoka akaunti moja kwenda akaunti nyingine bila idhini ya kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ya Halmashauri.

**(ii) Gharama za mithiani ya darasa la VII - 2007/2008**

- Kulikuwa na hati za malipo zenyе thamani ya Sh.108,299,500 kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Tarime ambazo hazikupatikana wakati wa ukaguzi huu maalum.
- Malipo ya jumla ya Sh.7,318,000 hayakuwa na viambatisho sahihi.
- Masurufu ya kiasi cha Sh.4,096,500 hayakuwa yamerejeshwa hadi kipindi cha ukaguzi.
- Nyaraka za kuthibitisha matumizi ya mafuta ya gari na vilainisho ya Sh.12,438,000 havikuweza kuwasilishwa wakati wa ukaguzi
- Mafaili binafsi 35 ya watumishi wa Halmashauri hayakuweza kuwasilishwa kwa ukaguzi ili kuwezesha uhakiki wa mishahara ya watumishi.

### 6.3.5 Halmashauri ya Wilaya ya Tarime

#### Matokeo ya ukaguzi maalum

- Kiasi cha Sh.12,699,800 kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa bwawa la Weigita zililipwa kwenye akaunti binafsi ya Mratibu wa TASAF badala ya akaunti ya mkandarasi. Mradi ulijengwa chini ya kiwango hivyo kukataliwa na jamii.
- Ukarabati wa wodi Na.1 na 2 na ujenzi wa jengo la Maabara ya katika Hospitali ya Wilaya ya Tarime uliogharimu kiasi cha Sh.300,000,000 ulikuwa wa chini ya kiwango. Hii ni dhahiri kwamba Mhandisi wa Wilaya hakufanya ukaguzi wa mwisho baada ya ukarabati kukamilika.

- Halmashauri ya Wilaya ya Tarime iliingia mkataba na Benchmark Investment Co. Ltd kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Mto Mori kwa mkataba wa Sh.145,566,200, lakini timu ya ukaguzi maalum imebaini mapungufu yafuatayo: Kiapo cha Wachambuzi wa Zabuni kufanywa baada ya kazi ya uchambuzi kumalizika, Benchmark Investment kutumia Mhandisi Msimamizi asiyé na sifa, Mkandarasi kufanya kazi pasipo dhamana ya utendaji, Kutoa nyongeza ya kazi/gharama bila ridhaa ya Bodi ya Zabuni na kubadilishwa kwa kipindi cha matazamio.

#### **6.3.6 Muhtasari wa Matokeo ya kaguzi maalum na uchunguzi**

Matokeo ya kaguzi maalum tano (5) ziliyofanyika katika mwaka 2009/10 kama ilivyoainishwa kwa ufupi hapo juu, ninaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba Halmashauri zinafanya vitendo vya ulaghai na rushwa. Mifano ni matumizi mabaya ya mikataba kama vile mikataba ya ujenzi, malipo ya awali kwa wakandarasi kulipwa kati ya 30% na 70% ya mkataba kinyume na kiwango kilichoidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ambayo inaruhusu kiwango cha juu 15% ya bei ya mkataba. Aidha, utekelezaji wa malipo bila hati za malipo au nyaraka sahihi, kutowasilisha vitabu vya kukusanya mapato kwa madhumuni ya ukaguzi na matumizi mabaya ya fedha kutokana na usuluhisho wa fedha usio sahihi ni sababu nyingine inayochangia. Pia kulikuwa na matukio ambayo baadhi ya vifungu vya amana vililipwa zaidi, na fedha zilitumika kwa madhumuni yasiyokusudiwa.

Kwa upande mwingine manunuzi ni moja ya maeneo nyeti yaliyopewa kipaumbele kuwa maeneo hatarishi. Udhafi ulionekana zaidi katika maeneo ya manunuzi kama vile manunuzi bila nukuu ya bei, manunuzi bila idhini ya bodi za zabuni, kutopokelewa kwa vitu vilivyoipiwa toka kwa wazabuni, manunuzi yaliyozidi kiwango na matumizi mabaya ya mafuta.

Halmashauri bado zina safari ndefu sana kuelekea kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani ambayo hatimaye kupunguza hatari ya vitendo ulaghai na rushwa.

#### **6.3.7 Hitimisho juu ya Ukaguzi Maalum**

Wakati wa kuandika taarifa hii, kaguzi Maalum nyingine mbili (2) zilikuwa zinaendelea, moja katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido na nyingine katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema. Matokeo yake yataripotiwa katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka ujao pamoja na taarifa za kaguzi nyingine zitakazoendelea kufanyika katika mwaka huu kama moja ya hatua ya kuimarisha uwajibikaji katika Serikali za Mitaa. Ofisi itaendelea kupokea maombi ya Kaguzi Maalum kutoka pembe zote lakini kwa kuzingatia sheria zilizopo kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu hawajibiki wala kulazimika kukubali maombi yote lakini atayapokea na kuchagua kutokana na umuhimu na faida yake.

## SURA YA SABA

### 7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Sura hii inahusika na hitimisho na mapendekezo juu ya matokeo muhimu ya ukaguzi ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele na kuchukuliwa hatua na Serikali kuu na Serikali za Mitaa kama ilivyoainishwa katika sura zilizotangulia za ripoti hii. Kama ilivyoainishwa katika sura ya utangulizi ni kwamba, ripoti ya mwaka ni muhtasari wa yale yaliyoriipotiwa kwenye ripoti zilizotolewa kwa kila Halmashauri. Ripoti hizo ndani yake pia kuna mapendekezo katika kila suala lillobainishwa lenye kuhitaji kuboreshwa. Maafisa Masuuli wa Halmashauri wanatakiwa kuandaa muundo wa majibu juu ya matokeo ya ripoti ya Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na mapendekezo yaliyotolewa humo, na kuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu na. 40 cha Sheria ya Ukaguzi ya Umma Na.11 ya mwaka 2008 na Kanuni 86 na 94 za Kanuni ya Ukaguzi ya Umma ya mwaka 2009. Ili kuweza kukabiliana na udhaifu uliotajwa katika ripoti hii kwa ufanisi, nina mapendekezo kadhaa ambayo kama yatakelezwa yataongeza uimara wa usimamizi wa fedha ndani ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

#### 7.1 Hitimisho

##### 7.1.1 Hati za ukaguzi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa

Kwa mwaka wa fedha 2009/2010 idadi ya hati za ukaguzi zenyenye mashaka kwa Serikali za Mitaa zimeongezeka kutoka 55 sawa na 41% katika mwaka 2008/2009 na hadi 65 sawa na 48.5% katika mwaka 2009/2010.

Matokeo haya ni kutokana na kupanua mawanda ya ukaguzi na ni kiashiria cha kutosha kuonesha udhaifu katika usimamizi wa fedha na udhibiti wa ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mapendekezo mengi yaliyotolewa katika ripoti ziliyopita za kila Halmashauri hayakuzingatiwa, hali ambayo ni kiashiria kuwa Halmashauri zimekosa umakini katika utekelezaji wa mapendekezo hayo.

Katika mwaka huu wa ukaguzi, Halmashauri 129 zilikuwa na mambo yaliyosalia kutoka miaka ya nyuma yenyе thamani ya Sh.122,128,377,615 ikiongozwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa yenyе Sh.8,992,407,355 ikifuatiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Same yenyе Sh.8,176,961,278, Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa ni ya tatu kwa jumla ya Sh.7,242,561,049 na ya nne ni Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Sh.6,097,936,644. Pia, kuna masuala ya ubora yasiyothaminika kwa fedha kama vile mifumo duni ya uhasibu, ufanisi duni wa Kamati za Ukaguzi, ukosefu wa sera ya usimamizi wa majanga na utendaji usiokidhi wa wakaguzi wa ndani na mapungufu katika udhibiti wa manunuzi.

#### **7.1.2 Ukosefu wa mwongozo kwa ajili ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani**

Kwa miaka kadhaa sasa, nimekuwa nikitoa mapendekezo juu ya udhaifu ulioonekana katika mifumo ya udhibiti wa ndani wa Halmashauri mbalimbali, hata hivyo hali hiyo haijaweza kurekebishwa. Udmaifu huu ni pamoja na yale yanayohusiana na mfumo wa kurithi wa Teknolojia ya Habari kama vile ukosefu wa sera za Teknolojia ya Habari inayopelekea udhaifu wa udhibiti wa kutosha katika kuzuia kupata ruhusa ya kuingia kwenye mifumo, ukosefu wa mpango endelevu na mipango ya kujikinga na majanga ambayo itahakikisha upatikanaji wa taarifa katika matukio ya maafa. Kutumia mfumo kwa kiwango kidogo au kutotumia kabisa mfumo wa Epicor ambao umelipiwa fedha kamilifu ni udhaifu mwingine ulioonekana.

Maeneo mengine muhimu ambayo yanahitaji ufuatiliaji na mwongozo rasmi kutoka OWM-TAMISEMI kuhusu udhibiti wa

ndani ni pamoja na udhibiti wa majanga, rushwa na ubadhilifu wa mali. Imebainika wakati wa ukaguzi kwamba Halmashauri nyingi hawana nyaraka za mifumo ya usimamizi wa majanga katika hali ambayo itahakikisha kwamba Halmashauri zinafikia malengo makuu ya kuwepo kwa kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

#### **7.1.3 Utofauti wa ripoti za fedha na kuitwa na wakati kwa Sheria za Serikali za Mitaa**

Baada ya kuingia kwenye mfumo wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma, OWM-TAMISEMI iliandaa mafunzo yaliyofanyika kwa baadhi ya wafanyakazi wa Serikali za Mitaa mwezi Agosti, 2009 kama msingi wa kuandaa taarifa za fedha zinazofuata mfumo wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma. Watumishi waliohusika walikuwa ni Waweka Hazina wa Halmashauri, Wakaguzi wa Ndani na Wahasibu wanaohusika katika uandaaji wa taarifa za fedha za kila Halmashauri. Hata hivyo, licha ya mafunzo hayo mazuri kufanyika, nimebaini utofauti wa taarifa za fedha zinazoandaliwa na uongozi wa Halmashauri kwa ajili ya kuwasilisha kwa madhumuni mbalimbali. Hii inatokea kwa sababu ya ushiriki na usimamizi duni katika mchakato wa kuandaa taarifa za fedha husika kwa madhumuni mbalimbali. Ni lazima ieleweke kwamba, Menejimenti ina wajibu wa kuandaa kumbukumbu zote za fedha na taarifa zote zinazowahusu kwa ajili ya ukaguzi.

Ukosefu wa miongozo inayoendana na Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma ni moja ya maeneo ambayo bado yana changamoto. Kama ilivyoelezwa katika ripoti ya ukaguzi iliyopita, miongozo iliyopo imepitwa na wakati na haina msaada katika kutoa ushauri wa kuridhisha unaoendana na misingi ya Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma. Miongozo hiyo iliyopitwa na wakati ni pamoja na Mwongozo wa Uandaaji Hesabu za Serikali za Mitaa wa 1993 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, 1997. Miongozo hii

miwili pamoja na mfumo mzima wa kisheria unaoongoza uendeshaji wa Serikali za Mitaa unatakiwa kuboreshwa kwa haraka.

#### **7.1.4 Ukopaji uliokithiri kwa watumishi wa Halmashauri ambao haukudhibitiwa na uongozi**

Wakati wa ukaguzi wa mishahara, mbali na Halmashauri kulipa mishahara ya wafanyakazi ambao hawako tena katika utumishi wa umma, nilibaini pia idadi kubwa ya wafanyakazi wa Halmashauri ambao wamekuwa wakilipwa mishahara yao ya kila mwezi kwa chini ya 1/3 ya stahili zao. Katika hali mbaya zaidi, baadhi ya wafanyakazi walikuwa hawalipwi chochote (mshahara ulikuwa sifuri). Mfano ni Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, kati ya mishahara ya wafanyakazi 198 iliyokaguliwa, wafanyakazi 45 sawa na 23% walikuwa hawalipwi kabisa. Hii ni kinyume na Waraka wa Utumishi wenye Kumb. Na.CCE.45/271/01/87 wa tarehe 19/03/2009 ambao unataka makato ya mishahara ya wafanyakazi yasizidi 2/3 ya mshahara wa msingi wa mtumishi. Utaratibu huu ambao haujadhibitiwa unaweza kuathiri utendaji wafanyakazi na hivyo kuathiri utendaji wa Halmashauri kwa ujumla. Hii inaashiria udhaifu wa Halmashauri katika usimamizi na kuhakikisha maslahi ya wafanyakazi yanalindwa.

#### **7.1.5 Kutoandaliwa kwa Taarifa za Fedha na Ukaguzi wa Hesabu za Vijiji**

Changamoto zimebainika juu ya usimamizi wa fedha zilizohamishiwa na zilizokusanywa katika ngazi ya chini ya serikali hasa katika Vijiji. Kwa kiwango kikubwa utunzaji wa vitabu vya fedha katika ngazi hii si mzuri. Halmashauri ambazo zina wajibu wa kuanzisha mfumo wa usimamizi wa fedha kulingana na kifungu na. 45 (3) cha Sheria za Fedha za serikali za mitaa ya mwaka ya mwaka 1982 hazitimizi wajibu wao inavyopaswa. Nimebaini idadi kadhaa ya matukio ambapo taarifa za fedha katika ngazi za chini za serikali hazikutunzwa vema. Utunzaji mbovu wa taarifa za fedha katika ngazi ya Vijiji unavunja moyo wananchi

kuchangia katika miradi ya maendeleo hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi hiyo ya chini ya serikali.

#### **7.1.6 Ukosefu wa Kujenga Uwezo katika Usimamizi wa Fedha katika Serikali ya ngazi ya chini**

Imebainika wakati wa ukaguzi kwamba miradi mbalimbali imekuwa ikitekelezwa katika ngazi za Vijiji. Masharti katika utekelezaji wa miradi hiyo ni kwamba viongozi wa Vijiji wanapaswa kuchukua jukumu la kuongoza katika utekelezaji wa miradi hii. Mantiki nyuma ya utaratibu huu ni kuhakikisha umiliki mkubwa wa miradi hii hata baada ya kukamilika, hii ni muhimu sana kwa sababu ya kuwa na miradi endelevu.

Hata hivyo, ilibainika kuwa viongozi wa Vijiji hawana mbinu za msingi na uelewa kwa ajili ya kusimamia miradi iliyopangwa. Ukosefu wa uwezo imekuwa moja ya sababu kuu ya kutokufikia lengo la miradi, hivyo kuikosesha jamii husika kupata huduma iliyokusudiwa.

#### **7.1.7 Udhaifu uliodhihirika katika kaguzi maalum**

Katika kaguzi maalum zilizofanywa kwa mwaka huu, nimebaini matukio mbalimbali yenye sura ya udanganyifu na rushwa. Taarifa hizo zilikabidhiwa kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Ofisi ya Mkuu wa upepelezi wa makosa ya jinai (DCI) kwa mujibu wa Kifungu 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Masuala haya ni pamoja na mikataba mibovu, mfano kwenye mikataba ya ujenzi, wakandarasi walikuwa wakilipwa malipo ya awali kati ya 30% na 70% ya mkataba kinyume na kiwango kilichoruhusiwa kwenye miongozo ya Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma ambayo inatamka kuwa malipo ya awali hayapaswi kuwa zaidi ya 15% ya bei ya mkataba. Suala jingine ni pamoja na kufanya malipo bila hati za malipo au kufanya malipo bila nyaraka za kutosha, kutokuwasilisha ukaguzi vitabu vya kukusanya

mapato na wizi utokanao na usuluhisho wa benki usio sahihi.

Halmashauri bado zina changamoto kubwa katika kazi za manunuizi, ambapo niliona kuna hila zinazosababisha kutoendana na matakwa ya Sheria ya Ununuzi Na.21 ya mwaka 2004. Udmaifu unaojitokeza mara kwa mara ni pamoja na ununuizi bila ya taratibu za ushindani kwa zabuni, ununuizi bila idhini ya bodi za zabuni, manunuizi ya vitu bila kuvipeleka katika eneo lililokusudiwa, manunuizi ya mafuta ya magari yaliyokithiri na matumizi mabaya ya mafuta. Eneo jingine lenye udhaifu mkubwa ni katika usimamizi wa mikataba.

Hii ni baadhi ya mifano ambayo inaonyesha kwamba kwenye usimamizi wa Halmashauri bado kuna changamoto katika kuhakikisha kuwa kuna mifumo sahihi katika usimamizi wa fedha katika mchakato mzima wa manunuizi.

#### **7.1.8 Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo (CDCF)**

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa Julai mwaka 2009 kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika kila Jimbo la uchaguzi. Mapato yote, akiba, na madeni ya Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo katika mwisho wa kila mwaka ni fedha zinazotakiwa kubakia kwa ajili ya shughuli Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.

Fedha za CDCF kwa mwaka wa ukaguzi hazikutumika kama ilivyokusudiwa. Katika baadhi ya Halmashauri, ukaguzi umegundua kuwa fedha hizo hazikutumika kabisa. Sababu zilizopelekea hayo ni pamoja na kutofunguliwa kwa akaunti maalum katika baadhi ya Halmashauri, pia fedha zilitolewa mwisho wa mwaka wa fedha yaani kati ya mwezi Mei na Juni 2010. Naweza kuhitimisha kwa kusema kwamba lengo la kuwa na mfuko huu katika mwaka wa fedha wa 2009/10 halikutimia kikamilifu.

Katika maeneo machache ambapo fedha zilitumika, Halmashauri hazikuwa zikiandaa na kuwasilisha kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa rekodi ya kiasi kilichopokelewa na kutumika kwa kila Kamati ya kuharakisha Maendeleo ya Jimbo. Hii ni kinyume na matakwa ya kifungu na. 7 (3) cha sheria ya mfuko wa kuharakisha Maendeleo ya majimbo, 2009.

#### **7.1.9 Ucheleweshaji wa ukamilishaji wa miradi na miradi iliyokamilika ambayo haitumiki**

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa, baadhi ya miradi ya ujenzi ilikuwa bado haijakamilika na idadi nyingine ya miradi ya ujenzi katika Halmashauri mbalimbali ilikamilika lakini ilikuwa haitumiki, sababu zikiwa ni pamoja na ukosefu wa michango ya jamii hasa pale ambapo michango ya fedha taslim na nguvu za wananchi zilitakiwa ukosefu wa wafanyakazi wa afya kwa ajili ya vituo vya afya/zahanati zilizokamilika na ukosefu wa huduma kama vile maji. Katika matukio yote, thamani ya fedha iliyowekezwa haikuweza kufikiwa.

Katika hali isiyo ya kawaida kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma iliweka mkandarasi wa kujenga nyumba kwa ajili ya watumishi wa shule ya Sekondari Mkigo kwa mkataba wa kiasi cha Sh.30,258,000. Ujenzi ulikuwa umekamilika lakini mkandarasi hakuwa amekabidhi nyumba kwa mwajiri (Halmashauri) ingawa kulikuwa hakuna nyumba yoyote nyingine kwa ajili ya walimu katika shule hiyo. Sababu za kutokabidhi nyumba hiyo ni kwamba, kuna migogoro kati ya mkandarasi na mlinzi wake katika suala la malipo jambo ambalo si sehemu ya mkataba. Funguo za nyumba hiyo zimekuwa zikikaa kwa mlinzi, naye kwa kuona hajalipwa akaondoka na funguo. Mlinzi huyo hajaonekana shuleni kwa muda mrefu sasa hivyo kupelekea malengo ya ujenzi wa nyumba kutofikiwa kwa sababu nyumba haikaliwi na mtu pamoja na  
Kuwa imeisha.

Sababu hizi zote zinaonyesha ukosefu wa usimamizi wa kutosha wa mikataba na usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

#### **7.1.10 Uwajibikaji usioridhisha katika mfuko wa LGDG na NMSF**

Ilibainika wakati wa ukaguzi wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGDG) kwamba katika sampuli ya Halmashauri zilizochaguliwa, kiasi kilichotajwa kupokelewa katika ngazi ya Halmashauri kilitofautiana na kiasi kilichorekodiwa kwamba kimelipwa kwa Halmashauri kwa mujibu wa hesabu za Mpango wa Maboresho wa Serikali za Mitaa (LGRP) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

Hitimisho ambalo linaweza kufikiwa ni kwamba tofauti iliyobainishwa imetokana na ukosefu wa mawasiliiano sahihi na usimamizi; fedha zinazohamishiwa katika Halmashauri hazifuatiliwi. Aidha, Halmashauri hazipati taarifa ya kutumiwa fedha katika akaunti zao za benki kwa wakati ili kuweza kujua kiasi walichotumiwa na madhumuni ya fedha hizo. Pia, kuna ukosefu wa usuluuhisho wa mara kwa mara wa taarifa baina ya mtoaji na Mpokeaji wa fedha hizo.

